Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA NNE

**Kikao cha Ishirini na Saba – Tarehe 18 Julai, 2011**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua*

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati ifuatayo iliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012.

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 248

### Utozaji wa Ushuru wa Mazao Katika Halmashauri

**MHE. HALIMA J. MDEE (K.n.y. MHE. REGIA E. MTEMA)** aliuliza:-

Mnamo wa tarehe 3 Mei, 2002 Serikali kupitia kwa aliyekuwa Waziri wa TAMISEMI Mheshimiwa Brig. Hassan Ngwilizi alitoa tangazo la kufuta ushuru wa mazao katika Halmashauri za Wilaya lakini hadi leo Wilaya ya Kilombero bado kuna mageti mawili yanatoza ushuru wa mazao ya kilimo kinyume na tangazo hili la Serikali:-

Je, Serikali inatoa tamko gani kufuatia hali hiyo kwa wananchi wa Kilombero?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Regia Estelatus Mtema, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa kilichofanywa na Mheshimiwa Brig. Hassan Ngwilizi mnamo mwaka 2002 siyo kufuta ushuru wa mazao na badala yake Serikali ilitoa utaratibu wa kukusanya ushuru huo pale zao linapozalishwa na kununuliwa *(Payable at Source).*

Mheshimiwa Spika, ushuru wa mazao unatozwa kwa mujibu wa kifungu 7(1) (g) cha Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa Sura Na. 290. Sheria hii haijafutwa hadi sasa isipokuwa kama nilivyosema hapo juu ushuru huu unatozwa mahali ambapo mazao yanazalishwa na siyo katika mageti au vizuizi.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Kilombero ina mageti mawili ambayo ni geti la Mkamba na geti la Idete. Mageti haya yamewekwa kwa mujibu wa Sheria ya Misitu Na. 14 ya mwaka 2002 pamoja na Kanuni namba 46(b) iliyowekwa kwa lengo la kudhibiti mazao ya misitu na utoroshaji wa Nyara za Serikali. Aidha Halmashauri hii inatumia vizuri hivyo katika kudhibiti na kukagua kuona kama ushuru wa mazao yanayosafirishwa umelipwa kwenye Kata kulingana na Sheria ya Fedha niliyoitaja hapo juu pamoja na Sheria Ndogo zilizowekwa na Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa wakati Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi anawasilisha Bajeti ya mwaka 2010/2011 katika aya ya 64(ii) ya marekebisho ya Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa Sura 290 alitamka kuwa kiwango cha kutoza ushuru wa mazao shambani kiwe kati ya asilimia 3 na asilimia 5 ya bei ya kuuza mazao shambani ili kuzipa fursa Halmashauri na Serikali za Mitaa kutoza ushuru huo kulingana na uwezo na rasilimali walizonazo.

**MHE. HALIMA J. MDEE**: Mheshimiwa Spika, nashukuru. Katika paragraph ya tatu ya jibu la Mheshimiwa Waziri amekiri kwamba ushuru huu unatozwa mahali ambapo mazao yanazalishwa na sio katika mageti au vizuizi. Sasa Serikali inatoa tamko gani kwa watu ambao wanakusanya huu ushuru katika mageti ama vizuizi?

Swali la pili, tunafahamu kwamba Sheria za Serikali za Mitaa na zinazoongoza pia Serikali za vijiji zinataka mapato yanayopatikana katika maeneo husika yawekwe wazi ili wananchi wajue na hatima ya matumizi.

Katika Jimbo la Kilombero kumekuwa na matatizo ya wahusika ama wenye mamlaka wanaokusanya hayo mapato kuyafanya kwa usiri mkubwa kiasi kwamba wananchi hawajui kimekusanywa nini na kimetumika vipi. Serikali inatoa tamko gani kuhusiana na hili?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)**: Mheshimiwa Spika, mimi naomba nilisaidie Bunge lako Tukufu hapa kinachofanyika katika haya mageti sio kutozwa ushuru ni *check point*. Huwezi kusimama barabarani kila basi na gari linalopita unasimamisha

unataka kicheki. Idete hii inayozunguzwa hapa mkiiondoa Idete na Mkamba nyara zote za Serikali mtazikuta ziko Hong Kong. *(Kicheko)*

Halmashauri zetu hizi na mmetuambia tujenge shule za Sekondari za *A'level* kila Tarafa na zahanati kila kijiji, niseme hapa, mimi nimekwenda, Mkuu wa Mkoa Kanali Machibya amekwenda pale ameona na mimi nimezungumza na Wabunge pamoja na Madiwani wanaohusika na jambo hili mmetupa jukumu kubwa la kusimama pale, geti hili wanakusanya pale ni *1.8 billion.* Geti la Idete na Mkamba ni *1.156 billion* ndizo zinakusanywa katika hili geti. Pale kinachofanyika ni *check point* tu, vijana wa mjini wanasema tunachungulia *deal,* tunaangalia na kama hajalipa tunarudisha mpaka huko.

Halmashauri ya Wilaya ya Kilombero kama hamtozi ushuru mjue wenzenu Kilosa watatoza ushuru na watalipa. Kibaya zaidi ni kwamba mazao yetu yanatoka hapa yanapelekwa Sudan, Somalia watajenga shule, maabara na watajenga kila kitu sisi tutabaki hivi hivi tu bila kitu. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nimwombe sana Mheshimiwa Mdee nawezake kwa suala hilo. Aidha analozungumzia hapa *the Member of Parliament is making a very valid point*. Hii siwezi kumkatalia, nimemwagiza Mkurugenzi Mtendaji kwamba kunafununu kwamba hela hizi zinaweza zikawa zinapita kwenye mifuko ya watu kwa kutengeneza vibutu ambavyo vinaonekana kwamba sihalali tutakwenda kuvi-*check* kujua kwamba vinakwenda wapi.

Suala la mapato na matumizi ya Halmashauri ni Baraza la Madiwani ni lazima lidai kila baada ya miezi mitatu na lazima mseme mletewe taarifa. *That is the bottom line,* naomba unisamehe sauti yangu hii nina maslahi nayo kwa sababu Halmashauri zetu zinafanya kazi hiyo. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Halima Mdee tutakwenda kusimamia jambo hili na tutamwagiza Mkurugenzi Mtendaji na tutakwenda kumpigia simu sasa hivi kumwambia nimepata habari kwamba hutoi taarifa ya mapato na matumizi kuhusu haya mageti yanayozungumzwa hapa. Naomba Wabunge mjue kwamba mmetupa majukumu makubwa ya kujenga maabara, hospitali, mtuache tukusanye ushuru ili Halmashauri ziweze kusimama.

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Ninaomba kumwuliza Naibu Waziri kwamba kuna maeneo sasa hivi ushuru unatozwa mara mbili na Sheria inasema ushuru utozwe mara moja tu. Unatozwa mpunga, ukikobolewa mchele unatozwa na mwaka huu kwa sababu bei imepanda ushuru badala ya kuteremka ili wananchi waliovuna kidogo kwa sababu bei ya mahindi ikiwa ni shilingi 40,000/- wanatozwa shilingi 1,200/- kuliko ile ya zamani ya shilingi 20,000/- ambayo walikuwa wamezoea ushuru wake ni shilingi 600/- tunaomba Serikali itoe tamko kwa hilo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)**: Mheshimiwa Spika, labda nieleze kwamba Sheria nimekuja nayo hapa na kila kitu ninanacho hapa. Kwanza asilimia inayozungumzwa hapa ni kati ya asilimia 3 hadi 5 ya mazao ndiyo tunayozungumzia hapa. Sisi tunachoangalia hapa mchele ni matokeo ya mpunga, akipita mtu na mchele tunamwambia tupatie risiti anasema mimi nimelipia Hanang tunamwambia tupe risiti ya

Hanang akitupa risiti ya Hanang tunam-*clear* anaenda zake, hatumtozi tena mara ya pili. Asipotoa risiti ya Hanang hata kama Hanang hawakumtoza sisi tunajua pale Babati tunalima mpunga, hatuwezi kupambanua mpunga unaotoka Hanang na unaotoka Babati, Mpunga ni mpunga na mchele ni mchele, tunachotaka lipa ushuru wa Serikali. *(Makofi)*

Kwa hiyo namwomba Ndugu yangu Jitu na tumekwenda wote mpaka kwenye Halmashauri yako tutoke nje tukae tuzungumze ili tuweze kupambanua hapa. *the bottom line is* imekuja na mchele wako hapa ukaniambia nimelipia mpunga nakwambia nipatie risiti ya mpunga.

Na. 249

**Ujenzi wa Barabara ya Kibiti – Nyamisati**

**MHE. ABDUL J. MAROMBWA** aliuliza:-

Mheshimiwa Rais kwenye kampeni zake za Uchaguzi Mkuu 2005 aliahidi ujenzi wa kiawngocha Changarawe barabara kutoka Kibiti-Ruaruke-Nyamisati.

(a) Je, ni sababu zipi zinazochelewesha kukamilika kwa ahadi hiyo?

(b) Je, ni lini sasa ahadi hiyo itakamilika?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Abdul J. Marombwa, Mbunge wa Kibiti, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa Mheshimiwa Rais alitoa ahadi ya kusaidia ujenzi wa barabara ya Kibiti – Ruaruke – Nyamisati, kwa kiwango cha changarawe.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia ahadi hiyo ya Mheshimiwa Rais, Serikali kupitia wakala wa barabara *TANROADS* katika mwaka 2009/2010 ilifanyika ukarabati barabara ya Kibiti –Ruaruke urefu wa km10 kwa kiwango cha changarawe kwa gharama ya shilingi milioni 186. Hata hivyo, Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji imetumia shilingi milioni 39.9 kwa ajili ya kufanya matengenezo ya sehemu korofi katika barabara ya Kibiti – Ruaruke - Nyamisati sawa na umbali wa km. 24. Aidha, katika mwaka 2010/2011 Halmashauri ilitenga fedha kiasi cha shilingi milioni 19.1 kwa ajili ya matengenezo ya barabara kutoka Kibiti – Ruaruke, sawa na km. 20.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2011/2012 Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji imetengewa shilingi milioni 634.2 kutoka Mfuko wa Barabara ambapo jumla ya shilingi milioni 30.7 zitatumika kwa ajili ya matengenezo ya barabara ya Kibiti – Ruaruke – Nyamisati ili iweze kupitika wakati wote.

**MHE. ABDUL J. MAROMBWA**: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu yasiyoridhisha ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa ahadi zote za Rais hutengewa Mfuko Maalum kwa ajili ya kuzikamilisha inakuaje ahadi hii ya Rais kwa mwaka huu kutenga milioni 30 ambazo ni mali ya Halmashauri ya Wilaya katika mradi wake ule wa *Road Fund,* hilo la kwanza.

La pili, Mkoa wa Pwani kwa miaka yote ahadi alizozitoa Rais utekelezaji wake unakuwa mgumu sana na hatuelewi sababu ni kitu gani. Inakuaje ahadi ya Rais aliyoitoa mwaka 2005 ya kujenga kwa kiwango cha lami kuunganisha barabara ya Makao Makuu ya Mkoa wa Pwani, mpaka hivi sasa utekelezaji wake haujaanza kuna nini katika utekelezaji wa ahadi za Rais kwa Mkoa huu wa Pwani?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)**: Mheshimiwa Spika, kwanza naomba niiweke vizuri hapa. Ninyi wote mnajua mimi hapa ubavu wa kushindana na ahadi ambazo zimetolewa na Rais sina la sivyo baada ya hapa kazi inakuwa imekwisha. Nikiambiwa Rais ameahidi kwangu mimi ni agizo, Mheshimiwa Waziri Mkuu ni agizo na Mheshimiwa Mkuchika ni agizo na hapa tumekuwa tunatoa majibu kuonyesha jinsi ambavyo tumekuwa tunatekeleza ahadi za Rais.

Nataka nimwondoe hofu Mheshimiwa Marombwa la kwanza ambalo tumelifanya *TANROADS* walipokutana kwenye Kamati ya Barabara Mkoa wa Pwani walipeleka maombi maalum kumwomba Waziri wa Ujenzi na bahati nzuri Mheshimiwa Magufuli yupo hapa, kumwomba barabara hii ichukuliwe. Ukiangalia majibu niliyotoa hapa kilomita karibu kumi zimefanywa na Wizara ya Ujenzi na napenda nichukue fursa hii kumshukuru Waziri wa Ujenzi kwa kazi nzuri ambayo ameifanya kwa sababu barabara ile wala si ya kwao na bado hajatoa tamko kwamba barabara ile imekuwa ni ya kwao. Ombi letu sisi tumwombe Waziri wa Ujenzi akubali kuchukua barabara hii. *(Makofi)*

Hili la pili analozungumza hapa kwamba Mkoa wa Pwani wote inaonekana kwamba ahadi za Rais zimeachwa, jamani kwa niaba ya Serikali nataka niseme hii si kweli na itahitaji kufanya utafiti kuangalia zahanati, barabara tukaangalie maji na kila kitu ili tuweze ku-*confirm* yanayozungumzwa hapa.

Kwa hiyo namwomba ndugu yangu Marombwa ni kweli kabisa ukiangalia barabara hii na pesa zilizotengwa bado ni kidogo kwa sababu ahadi iliyotolewa pale ni barabara ya changarawe. Tutakwenda kuangalia sisi wote kuangalia mpaka yale maombi maalum ambayo mmepeleka kule wote kwa pamoja tushirikiane na Wilaya na Wizara ya Ujenzi tuone jinsi ambavyo tutakwenda kutekeleza ahadi ya Rais.

**MHE. SUBIRA K. MGALU**: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Je, Serikali ipo tayari kutoa tamko la mwisho na kwamba ni lini kipande cha barabara ya Somanga Ndundu kitakamilika ili kuwaondolea adha wakazi wa Kati ya Mbwela, Nambuchi na Mikoa ya Lindi na Mtwara?

**WAZIRI WA UJENZI**: Mheshimiwa Spika, barabara hii Mkandarasi yuko kwenye *site* na gharama za ujenzi wa kilomita 60 karibu shilingi bilioni 59. Tulipotembelea mwezi mmoja uliopita tulitoa maagizo kwa Mkandarasi kwamba barabara hiyo awe ameikamilisha kabla ya mwezi wa kumi na moja mwaka huu. Ni mategemeo yetu tutaendelea kumbana Mkandarasi ili kusudi aweze kukamilisha barabara ile kwa kiwango cha lami kama tulivyomwagiza na kulingana na mkataba uliopo. *(Makofi)*

Na. 250

**Zanzibar Kushughulikia Masuala ya Ushirikiano wa Kimataifa**

**MHE. MARIAM S. MSABAHA (K.n.y. MHE. MWANAMRISHO T. ABAMA)** aliuliza:-

Ushirikiano wa Kimataifa si mambo ya Muungano, japokuwa masuala ya mambo ya nje ni miongoni mwa mambo ya Muungano hata hivyo mambo yote mawili yapo kwenye Wizara moja ya Muungano.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba Zanzibar inashughulikia yenyewe masuala ya ushirikiano wa kimataifa?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mwanamrisho Taratibu Abama, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Ni kweli kwamba suala la Ushirikiano wa Kimataifa hushughulikiwa na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa ambayo ni miongoni mwa Wizara za Muungano. Aidha kwa kuwa mambo ya Nje huhusisha Ushirikiano wa Kimataifa, Serikali zetu mbili zilikubaliana na mapendekezo yaliyotolewa na Kamati ya Shellukingo kwamba mambo ya Ushirikiano wa Kimataifa yawe ya Muungano. Katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, pande zote za Muungano zimekuwa zikishirikishwa katika masuala ya Kimataifa kama vile makongamano ya biashara, uwekezaji, nafasi za elimu ya juu na mikutano ya kikanda na kimataifa. Aidha katika kuhakikisha kwamba Zanzibar inashirikiana na Taasisi za Nje, mwongozo wa namna ya kuishirikisha Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika suala yote ya Kimataifa kuanzia hatua za awali umeandaliwa. Mwongozo huo umeandaliwa na Kamati ya Wataalam kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Wizara za Katiba na Sheria za Serikali Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa

Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar pamoja na Ofisi za Wanasheria Wakuu wa Serikali zetu mbili.

Mwongozo huo umezingatia maeneo ya ziara za viongozi wa Kitaifa; Mikutano ya Kimataifa, nafasi za masomo ya Elimu ya Juu Nje ya Nchi; na Utafutaji fedha za misaada au mikopo za kutekeleza miradi kutoka nje ya nchi. Mwongozo huu utaiwezesha Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kushiriki kikamilifu katika masuala mbalimbali ya Kimataifa kuanzia hatua za awali.

**MHE. MARYAM SALUM MSABAHA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa kuwa kero za Muungano zimekuwa zikilalamikiwa na Wazanzibari wengi. Je, Serikali ya Tanzania Bara na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar haioni kuna haja sasa ya kutenga muda muafaka wa kutatua kero hizo? Na kwa kuwa Wazanzibari wengi wamekuwa wakilalamikia misaada ambayo inatolewa na wafadhili haiwafikii mara nyingi…

**SPIKA:** Usisome!

**MHE. MARYAM SALUM MSABAHA:** Pesa hizo zinabaki Tanzania Bara. Je, Waziri atahakikishaje Wazanzibari nao wanapatiwa haki zao kwa muda muafaka?

**SPIKA:** Haya, Mheshimiwa Msabaha hatusomi! Haya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, majibu!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO:** Mheshimiwa Spika, kwanza, naomba kidogo nimsahihishe ndugu yangu Mheshimiwa Mariam kwamba hakuna Serikali ya Tanzania Bara, lakini ni Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu muda muafaka wa kutatua kero za Muungano, kama nilivyojibu wakati nasoma Bajeti au kama nilivyoeleza kwamba kero za Muungano zina muda mrefu wa kufanyiwa kazi na kuna vikao kadhaa ambavyo tunafanyia kazi. Kwa sasa hivi mwelekeo ni kwamba tunakaribia kuzimaliza na kama zitabaki, ni chache sana baada ya kumaliza kipindi cha awamu ya nne.

Mheshimiwa Spika, kuhusu misaada ya wafadhili, Zanzibar inapata fungu lake kwa ile inayokuja chini ya mwamvuli wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwenye sekta za Muungano. Lakini, bado kuna utata kwa sekta ambazo siyo za Muungano, na suala hili tunalifanyia kazi.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Mheshimiwa Spika, Waziri wakati anajibu swali alisema kwamba ni kweli mambo ya Ushirikiano wa Kimataifa si suala la Muungano, lakini kutokana na mapendekezo ya Mheshimiwa Shellukindo au Kamati ya Shellukindo, ndiyo utaratibu umetolewa. Je, sasa tunafuata Katiba au tunafuata mwongozo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO:-** Mheshimiwa Spika, ilivyo katika kuongoza mambo ya Muungano, tufuate Katiba ilivyotuelekeza. Lakini, inawezekana kabisa kwamba wakati wa Tume ya Shellukindo, Serikali mbili zilivyokuwa zikijadiliana hili lilikubalika. Na ikiwa tunahisi kwamba, au wananchi wanahisi kwamba na hili nalo limeingizwa kinyemela, basi wakati wa Marekebisho ya Katiba, ni wakati muafaka kufanyia marekebisho haya. *(Makofi)*

Na. 251

**Kudhibiti Hali ya Kuyeyuka kwa Barafu Mlima Kilimanjaro**

**MHE. MUSTAPH B. AKUNAAY (K.n.y. MHE. JOSEPH R. SELASINI)** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kudhibiti hali ya uyeyukaji wa theluji juu ya Mlima Kilimanjaro?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MAZINGIRA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Joseph Roman Selasini, Mbunge wa Rombo, naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, barafu juu ya kilele cha Mlima Kilimanjaro imepungua kwa kiasi kikubwa na kumethibitishwa na tafiti mbalimbali ndani na nje ya nchi kuanzia mwaka 1987.

Ripoti ya Nne ya Kimataifa Kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi ya mwaka 2007 *(IPCC – Intergovernmental Panel on Climate Change Fourth Assessment Report)* imethibitisha kuyeyuka kwa barafu katika Mlima Kilimanjaro kunakotokana na mabadiliko ya tabianchi kutokana na ongezeko la joto Duniani.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Joseph Roman Selasini, Mbunge wa Rombo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imechukua hatua mbalimbali ambazo ni pamoja na:-

(i) Kuufanya Mlima huu kuwa Hifadhi ya Dunia. Kwa muktadha huo, miradi mbalimbali ya Serikali na wafadhili inatekelezwa ili kusaidia kuhifadhi mazingira ya eneo hili. Kwa mfano Serikali kwa kushirikiana na NEPAD chini ya ufadhili wa Mfuko wa Mazingira ya Dunia inaanza kutekeleza mradi wenye jumla ya Dola za Kimarekani milioni tatu kwa lengo la kuhifadhi Mlima Kilimanjaro na Mkoa mzima.

(ii) Serikali kwa kushirikiana na Umoja wa Nchi za Ulaya inatarajia kuanzisha Kituo cha Kitaaluma cha Mabadiliko ya Tabianchi *(Climate Change Centre of Excellency)* na Makao Makuu yatakuwa Mjini Moshi.

(iii) Kutekeleza mkakati wa kuhifadhi mazingira ya ardhi na vyanzo vya maji kwa upandaji miti Mkoani Kilimanjaro na nchini kote ikiwa ni pamoja na kuwataka watumiaji wakubwa wa kuni na mkaa, kuanzisha mashamba yao ya miti kwa ajili ya uvunaji wa kuni na mkaa na kuacha kuvamia misitu hasa ya hifadhi.

Kupitia mkakati huu, Serikali imeanzisha Tuzo ya Rais ya Kuhifadhi Mazingira kwa kupanda na kutunza miti ili kuhamasisha zaidi wananchi. Tuzo hii hutolewa Siku ya Mazingira Duniani inayoadhimishwa tarehe 5 Juni, kila baada ya miaka miwili.

(iv) Kuongeza ushirikiano wa Kimataifa na kuchagiza nchi zinazoendelea kukubali kupunguza mlundikano wa gesijoto angani zinazosababisha kuyeyuka kwa barafu katika Mlima Kilimanjaro na milima mingine mirefu Duniani. Aidha, nchi zinazoendelea zinahimizwa kutoa fedha kwa ajili ya kusaidia nchi zinzoendelea kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi kwa mujibu wa Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi.

Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kuiomba Serikali ya Mkoa wa Kilimanjaro na Mheshimiwa Mbunge kusaidia juhudi za utunzaji wa Mlima wa Kilimanjaro na Mkoa mzima kwa kuelimisha wananchi ili kuona umuhimu wa Mlima Kilimanjaro ki-Dunia, hivyo kuwa na wajibu mkubwa wa kuhifadhi Mlima huo kwa kutovamia hifadhi na kukata miti ovyo, kutochoma misitu, ili kuacha uoto wa asilia uendelee kukua katika Mlima Kilimanjaro.

**MHE. MUSTAPH B. AKUNAAY:** Mheshimiwa Spika, katika jibu la Mheshimiwa Waziri, sehemu ya tatu, amesema kwamba Serikali kwa kutekeleza mkakati wa kuhifadhi mazingira ya ardhi na vyanzo vya maji kwa upandaji wa miti Mkoa wa Kilimanjaro na nchini kote ikiwa ni pamoja na kutaka wakataji wakubwa wa kuni na mkaa kuanzisha mashamba yao ya miti kwa ajili ya uvunaji na…

**SPIKA:** Mheshimiwa, ndivyo alivyosema, sasa wewe unasemaje?

**MHE. MUSTAPH B. AKUNAAY:** Mheshimiwa Spika, ndiyo nasema, kutokana na jibu hilo, hilo ni jibu la jumla. Je, Serikali ina *marshal plan* kwa ajili ya kuhifadhi mlima huo ambao umaarufu wake umeifanya Tanzania ijulikane Duniani kote?

Mheshimiwa Spika, pili, kwa kuwa tafiti nyingi za *University* ya Australia na huko Ohio zimesema kwamba mlima unaweza ukaisha theluji mwaka 2020. Je, hizo tafiti zingine zinathibitisha hivyo au siyo kweli?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, jibu nililolitoa siyo jibu la jumla, nina uhakika kwa sababu kila Halmashauri ina kiwango maalum cha kupanda miti kila mwaka. Labda, nimwombe

Mheshimiwa Selasini aende kwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Moshi akahakikishe kila mwaka wanapanda miti mingapi. Lakini sisi tunaripoti na pia tunapita kufuatilia kwamba kila Halmashauri, kila mwaka ina kiwango cha miti ambacho kinatakiwa kupanda. Sula la pili kuhusu tafiti; tafiti ziko nyingi sana siwezi kuzisema hapa, anaweza kuja ofisini tukampa tafiti mbalimbali. Lakini utafiti wa mwisho kabisa ni wa mwaka 2007 ambao ni utafiti wa Kimataifa na ndio huo nimeutolea taarifa. Lakini, tafiti ziko nyingi sana. Ahsante.

**MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa matatizo ya tabianchi yaliyosababisha theluji ya Mlima Kilimanjaro kuyeyuka, ni sawa na tabianchi iliyosababisha fukwe za Bahari zetu kuwa na joto na samaki wakatoweka na kusababisha watu kutumia miti kwa kutengeneza mkaa na chokaa.

Je, Mheshimiwa Waziri, ofisi yako itakuwa tayari kiasi gani kuvisaidia hasa Visimwa vya Unguja na Pemba ambavyo vimekuwa *affected* sana tatizo hili ili watu wapate kazi mbadala badala ya kukata miti wakazidi kuharibu mazingira?

**SPIKA:** Aha! Kutoka Kilimanjaro mpaka ufukweni! Waziri wa Nchi nawe unajua tu haya mambo! *(Kicheko)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, mabadiliko ya tabianchi yana athari nyingi sana. Moja, ni theluji ya Mlima Kilimanjaro kuyeyuka. Pili ni maporomoko mbalimbali na kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge fukwe za Zanzibar pia zimeharibika. Siyo hivyo tu, mwezi uliopita tu tumeona tetemeko kubwa sana Dar es salaam limetokea kama mara mbili. Hayo yote ni matokeo ya mabadiliko ya tabianchi kutokana na kuharibu mazingira. Ninachoweza kusema ni kwamba, tujisaidie wote na kuelimisha wananchi kwamba tunavyoendelea kuharibu mazingira ndivyo mabadiliko ya tabianchi yanavyozidi kuwa makubwa zaidi. Kwa hiyo, ninachoweza kukuthibitishia tu Mheshimiwa Mbunge, ni kwamba tutakuja Zanzibar, nitakuja na watalaam tuangalie namna gani hali imebadilika na pia tusaidiane kuwaelimisha wananchi wasikate mikoko kwa sababu mikoko ndiyo inayosaidia sana kutunza fukwe zetu za Bahari yetu. Kwa hiyo, kama wamekata hiyo mikoko, basi tutajua namna gani tuwaelimishe ili kurudisha hiyo mikoko. Ahsante sana. *(Makofi)*

Na. 252

**Azma ya Kuwalea, Kuwatunza na Kuwaendeleza Watoto Yatima**

**MHE. AGNESS E. HOHORORO (K.n.y. MHE. VICKY P. KAMATA)** aliuliza:-

Kutokana na matamshi ya viongozi wetu wa juu, Taifa limedhamiria kupambana na changamoto ya kuwatunza, kuwasomesha, kuwaendeleza Watoto Yatima:-

(a) Je, ni kwa kiwango gani azma hii ya kulea, kuwatunza na kuwaendeleza Watoto Yatima imefanikiwa Kitaifa kuanzia mwaka 2005 mpaka sasa?

(b) Je, Serikali inaweza kuwasomesha na kuwaendeleza watoto wangapi katika Mkoa wa Mwanza na Geita?

(c) Je, Serikali inatoa tamko gani juu ya kuendeleza juhudi na wajibu wa kuwatunza, kuwalea, kuwasomesha na kuwaendeleza Watoto Yatima?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Vicky Paschal Kamata, Mbunge wa Viti Maalum wa Geita, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kuanzia mwaka 2005 hadi sasa Serikali imefanya mpango wa utambuzi wa huduma na malezi kwa Watoto Yatima na wanaoishi katika mazingira hatarishi katika Halmashauri 89 kati ya Halmashauri 133 hapa nchini ikiwa ni pamoja na Halmashauri za Mwanza na Geita. Watoto waliotambuliwa kuwa wanaishi katika mazingira hatarishi ni 802,077 (wakiwemo asilimia 53% wa kiume na 47% watoto wa kike). Kati ya watoto hao, watoto 668,022 wanapata huduma mbalimbali kulingana na mahitaji yao ikiwemo chakula, mavazi, malazi, huduma za afya, huduma za kisaikolojia na kijamii pamoja na elimu.

(b) Mheshimiwa Spika, katika Mkoa wa Mwanza, Serikali kupitia Bajeti za Halmashauri za Wilaya na Mfuko wa Elimu wa Mkoa wa Mwanza *(Mwanza Children Education Fund*) na wadau mbalimbali wa Maendeleo imeweza kuwasomesha na kuwaendeleza watoto 12,000 waliotambuliwa kuwa na mahitaji ya kielimu kati ya watoto wote 45,830 waliotambuliwa. Aidha, katika Mkoa mpya wa Geita, Serikali kupitia Bajeti za Halmashauri za Wilaya na Wadau mbalimbali wa Maendeleo imeweza kuwasomesha na kuwaendeleza watoto 8,000 waliotambuliwa kuwa na mahitaji ya kielimu kati ya watoto wote 38,271 waliotambuliwa.

(c)Mheshimiwa Spika, matamko ya Serikali kuhusu suala zima la upatikanaji wa elimu kwa watoto yamekwishatolewa kupitia Sera ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi na hatimaye kusisitizwa zaidi katika Sheria ya Mtoto Na. 21 ya mwaka 2009 katika sura inayohusu haki na ustawi wa watoto.

Hivyo, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri, wadau, jamii pamoja na walezi wa watoto hao, itaendeleza juhudi za kuwatunza, kuwalea, kuwasomesha na kuwaendeleza Watoto Yatima walio katika mazingira hatarishi kwa kuhakikisha kuwa wanapatiwa mahitaji yao ya msingi yakiwemo ya kielimu pamoja na kufuatilia maendeleo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda nichukue fursa hii kuwashukuru Wadau wote wanaoshirikiana na Serikali katika kutoa huduma kwa watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi.

**MHE. AGNESS E. HOHORORO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, napenda kuuliza maswali mawili kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa katika majibu ya msingi ametuambia kuwa ni watoto 8,000 tu kati ya watoto 12,000 waliotambuliwa wenye mahitaji ya kielimu Mkoani Mwanza.

Je, Serikali haioni kwamba hawa wengine wanaobaki bado wanaendelea kukosa mahitaji yao ya msingi?

Pili, kwa kuwa suala la Watoto Yatima ni suala la Kitaifa na mazingira yake yanafanana. Serikali haioni ni wakati muafaka sasa kuelekeza watu wanaofungua taasisi za kulea Watoto Yatima zinaonekana nyingi kumea kama uyoga Jijini Dar es salaam, kuelekeza wafungue taasisis hizo katika Mikoa mingine ikiwemo Mtwara? *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, Majibu! Angalau huyu amekuwa mwaminifu, kaulizia Mwanza halafu na Mtwara. *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba watoto waliotambuliwa ni 12,000. Na katika utambuzi, hatutambui tu tukasema kwamba aha, Juma ana tatizo! Hapana! Walikuwa wanatambuliwa kwamba huyu mtoto yuko kwenye mazingira hatarishi, anaangaliwa matatizo yake. Halafu kwa mtindo huo wa kuangalia tunaangalia waliozidiana zaidi, wanapangwa kwa mfumo huo.

Sasa, tunapopata rasilimali, tunaangalia kwamba tuanze na wale ambao wana matatizo zaidi. Halafu pale ambapo hela inaishia tunaachia kusudi atakapokuja tena mfadhili mwingine, anaendelea kuongeza wale watoto. Kwa hiyo, siyo kwamba hao wengine wataachwa, ila bado tunatafuta rasilimali za kuendelea kuwasaidia kwa sababu waliobaki walikuwa na ahueni kuliko wale ambao tulianza nao toka mwanzoni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Ni kweli kwamba kuna utitiri wa *NGOs* ambazo ziko Dar es salaam zinazoshughulikia watoto wanaoishi kwenye mazingira hatarishi kwa sababu, nafikiri ambao wamepata huo mvuto wengi wao wako Dar es salaam na watoto wengi ambao wanaishi kwenye mazingira hatarishi hasa watoto wa mitaani wako pia kwenye Jiji la Dar es salaam na Majiji mengine makubwa pia.

Mheshimiwa Spika, lakini nafikiri Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto yenye dhamana ya kusajili Mashirika yasiyokuwa ya Kiserikali imekuwa inajaribu kutoa ushauri nasaha na msukumo wa pekee kuhakikisha kwamba inawahamasisha wanaoanzisha *NGO* hasa zile ambazo zinataoa huduma kwa watoto ziende Vijijini kwa sababu nako kuna watoto, na sisi kupitia Ustawi wa Jamii tutahakikisha kuwa tunaendelea kuwashauri na kuwahimiza ili waende wakasaidie katika hayo maeneo mengine ambayo ni muhimu kwa maendeleo ya nchi yetu.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa watoto wanaotambuliwa na Serikali ni wale ambao walezi wao hupeleka taarifa kwenye *Ward C*, *Ward C* inajadili inapeleka Halmashauri. Kwa kuwa si watoto wengi wenye walezi, wako wengine hawana walezi kabisa.

Je, Serikali haioni kwamba kuna kila sababu sasa kufanya sensa kwa nchi nzima kila wanafunzi wanapomaliza darasa la saba ili kuwapata wanafunzi wote ambao wanaishi kwenye mazingira magumu na hawana walezi waweze kupata msaada huu wa Halmashauri pamoja na Serikali? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kuna watoto wengi kwenye Halmashauri zetu na mtindo uliokuwa unatumika kuwasaidia ni kwamba watambulike kupitia kwenye *Ward C*.

Ninaomba nimkumbushe Mheshimiwa Mbunge kwamba, kwenye kila kijiji kuna Kamati ya Watoto Wanaoishi kwenye Mazingira Magumu, ndiyo ambao wana jukumu la kuwatambua na kuwapeleka kwenye Halmashauri ili waweze kupata huduma. Kwa hiyo, ninaamini kwamba, mfumo huo unafaa, ninaomba nitoe wito kwa Halmashauri ziweze kuwapa mafunzo juu ya majukumu yao ili wakiyatekeleza vizuri, waweze kutambua watoto wengi watakaoweza kusaidiwa kwenye ngazi ya jamii na kwenye ngazi za Halmashauri.

Na. 253

**Mpango wa Kitaifa wa Kuzuia Ukatili Dhidi ya Wanawake**

**MHE. AGNESS E. HOKORORO** aliuliza:-

Serikali kwa kutambua kwake ukatili unaofanywa dhidi ya wanawake imeweka Mpango wa Kitaifa wa Kuzuia Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto (2001 – 2015):-

(a) Je, ni kwa kiwango gani Serikali imetekeleza Mpango huo na ni Wanawake wangapi waliotambulika kufanyiwa ukatili na wangapi sheria imechukua mkondo wake dhidi ya waliofanya ukatili huo?

(b) Je, Serikali inaweza kubainisha kuwa tatizo hili la ukatili limekwisha au bado na kama bado ni kwa nini?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Agness Elias Hokororo, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Mpango wa Kuzuia na Kuondoa Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto wa Mwaka 2001 – 2015, umefanyiwa kazi kwenye maeneo yake makuu manne katika viwango tofauti kulingana na uwezo, uelewa na rasilimali zilizopo. Sisi wenyewe ni mashuhuda wa marekebisho ya sheria na sera mbalimbali zilizokuwa zinawakandamiza Wanawake na Watoto na bado kazi hii inaendelea. Mifuko mbalimbali imeanzishwa kuwawezesha Wanawake kiuchumi. Pia uwepo wa ongezeko la ushiriki wa nafasi za wanawake katika maamuzi, uboreshaji huduma za afya kwa Wananwake na Watoto na uhamasishaji na utoaji wa elimu kuhusu kupiga vita ukatili wa kijinsia. Utekelezaji wa Mpango huu unatekelezwa na Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali, zikiwemo asasi zisizokuwa za Kiserikali, Mashirika ya Dini, Taasisi za Serikali na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa *Tanzania Demographic and Survey - TDHS 2010*, takwimu zinaonesha kuwa, asilimia 39 ya Wanawake wenye umri kati ya miaka 15 - 49 wamewahi kufanyiwa ukatili toka wakiwa na umri wa miaka 15; na kwamba, theluthi moja au asilimia 33 ya Wanawake hao, wamefanyiwa ukatili wa kijinsia kwa kipindi cha mwaka 2009. Kwa kuwa ukatili dhidi ya Wanawake unajumuisha makosa mbalimbali ya jinai, makosa haya yanaripotiwa polisi na kupelekwa mahakamani kwa mujibu wa sheria.

(b) Mheshimiwa Spika, ninaomba nimfahamishe Mheshimiwa Mbunge kuwa, tatizo la ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto, bado halijaisha katika jamii zetu. Hivyo, juhudi za pamoja kati ya Serikali na wadau mbalimbali zinahitajika ili kuhakikisha kuwa tunatokomeza tatizo hili.

**MHE. AGNESS E. HOKORORO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza maswali ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Waziri, ninapenda kumwuliza maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa Mpango huu moja ya jukumu lake kuu katika eneo la kisheria lilikuwa ni pamoja na kurekebisha sheria zinazokandamiza Wanawake na Watoto; na kwa kuwa katika *timeframe* inaonekana kuwa suala hilo lingetekelezwa kuanzia 2005 mpaka mwaka 2008 lakini mpaka sasa halijafanyika:-

(a) Je, Wizara na Serikali kwa ujumla haioni kwamba Mpango huu wa Kitaifa unatekelezwa chini ya kiwango?

(b) Kwa nini Serikali isione umuhimu wa kutafuta takwimu kwa kesi ambazo tayari zimeshahukumiwa ili tuweze kujua tupo katika hatua gani na kama kweli matukio hayo yanachukuliwa sheria sahihi katika jamii zetu?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO**: Mheshimiwa Spika, kwanza, ninampongeza sana Mheshimiwa Agness Hokororo, kwa

kuwa mmojawapo wa majemedari katika Bunge lako Tukufu, ambao wamejitolea kutetea haki za Wanawake, Wasichana na Watoto. Wanawake wa Mtwara hawajafanya makosa.

Mheshimiwa Spika, Mpango unatekelezwa kama nilivyosema, kutokana na uwepo wa rasilimali na uwezo; Mpango huu ni mpaka mwaka 2015. Kweli tulisema kwamba, *by 2008* tungeweza kurekebisha Sheria za Ndoa na Mirathi, ambazo zinawakandamiza Wanawake, lakini ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, tumeelekezwa na Ilani ya Uchaguzi ya CCM, aya ya 187, kwamba, tutafanyia marekebisho sheria zinazokandamiza Wanawake. Ninamthibitishia hadi kufikia 2015, kabla Mpango huu haujakwisha, tutakuwa tumeleta kwenu sheria zilizofanyiwa marekebisho za ndoa na mirathi.

Mheshimiwa Spika, katika swali lake la pili kuhusu takwimu za kesi zilizohukumiwa; ukatili dhidi ya Wanawake unajumuisha makosa mbalimbali; kulawiti, kubaka, kusafirisha Wanawake kwa ajili ya masuala ya ngono na vipigo; kwa hiyo, itakuwa ni ngumu sana kusema nimpe takwimu kwamba ni kesi ngapi zilizofikishwa mahakamani na kesi ngapi zimeamuliwa. Ninamwomba tukitoka hapa tuonane, nina takwimu ambazo nimezipata kutoka Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, zinaonesha ni kesi ngapi za ubakaji zimefunguliwa na ni kesi ngapi sasa hivi zinaendelea mahakamani. Ninakushukuru sana.

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa Wanawake wengi wanaofanyiwa ukatili huwa wanaficha kwa kuogopa kufanyiwa ukatili zaidi: Je, Serikali inashauri nini Wanawake wanaofanyiwa ukatili kama huo?

**SPIKA**: Mheshimiwa Naibu Waziri jibu, Mwanamke akipata ngeu anasema nilianguka jikoni! (*Kicheko*)

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, kwa kweli Wanawake wengi wanaofanyiwa ukatili hawafichi, kumekuwa na matukio mengi ya kuripoti vitendo vya ukatili, hii ni kutokana na kwamba, tumejenga mwamko na hamasa katika jamii.

Mheshimiwa Spika, tatizo ninaloliona ni kwamba, Wanaume wanaofanyiwa vitendo vya ukatili, ndiyo wanaoogopa na wanaficha. Ninaomba nitumie Bunge lako Tukufu kuwaambia Wanaume wote kuwa wasiogope, sasa hivi kwenye Vituo vya Polisi tumeanzisha Madawati ya Jinsia kwa ajili ya kuchukua makosa mbalimbali yanayohusu vipigo. Kwa hiyo, ninatoa wito kwamba, hata Wanaume mnaofanyiwa ukatili msijifiche nendeni mkaripoti. *(Kicheko/Makofi)*

**SPIKA:** Kuna wakati fulani takwimu zilionesha kwamba, Wanaume wanapata kipigo kutoka kwa wake zao kuliko hata Wanawake wenyewe. (*Kicheko*)

Na. 254

**Kuweka Lami Barabara ya Bunda – Kisorya – Masonga**

**MHE. SALVATORY N. MACHEMLI** aliuliza:-

Barabara kubwa ya kutoka Bunda Kupitia Kisorya kwenda Rugezi -Nansio hadi Masonga haiko katika hali nzuri licha ya kwamba inategemewa sana katika kusafirisha mazao ya samaki na mbao kutoka Rubya Forest:-

Je, ni lini Serikali itaitengeneza kwa kiwango cha lami au angalau hata lami nyepesi ili iweze kupitika nyakati zote?

**WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Salvatory Naluyaga Machemli, Mbunge wa Ukerewe, kama ifuatavyo:-

Serikali tayari imeanza maandalizi ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa Barabara ya Bunda – Kisorya – Rugenzi hadi Nansio (km 118), kwa kuifanyia usanifu. Kazi za usanifu zinaendelea na zinatarajiwa kukamilika katika Mwaka wa Fedha wa 2011/12. Baada ya usanifu kukamilika, Serikali itaanza kutafuta fedha toka vyanzo mbalimbali ili ujenzi wa Barabara hiyo kwa kiwango cha lami uweze kuanza.

Mheshimiwa Spika, wakati kazi ya maandalizi ya ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami yakiendelea, Wizara yangu itaendelea kutenga fedha kila mwaka kwa ajili ya kuifanyia matengenezo na ukarabati barabara hiyo ili iweze kupitika bila shida wakati wote wa mwaka.

**MHE. SALVATORY N. MACHEMLI:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru sana kwa majibu mazuri ya Waziri wa Ujenzi na kwa kulitaja vizuri jina langu.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa umuhimu wa Barabara kwa Kisiwa cha Ukerewe ni kusafirisha mazao ya samaki kutoka katika Ziwa Ilangala na mazao ya mbao katika Msitu wa Rubya; na kwa kuwa katika jibu la msingi Waziri ametaja kwamba upembuzi yakinifu unaanzia Bunda, Mwibara hadi Nansio, lakini umuhimu zaidi wa Barabara hii ni Visiwa vya Ilangala kwa mantiki ya mazao ya samaki kutoka katika visiwa vile na zao la mbao kutoka msitu wa Rubya:-

(a) Je, ni lini Serikali itaitengeneza Barabara hii kwa kiwango cha lami kuanzia Nansio Mjini, kupitia Mahande, Rubya kwenye msitu mpaka Masonga?

(b) Kwa kuwa katika Kisiwa cha Ukerewe kuna utalii wa asili wa jiwe linalocheza kwa amri ya Babu; je, Serikali haioni kwamba sasa ni muhimu kuipandisha hadhi Barabara ya Bwisha - Nyang’ombe - Nyamanga hadi Kombe kuipeleka kwa Wakala wa Barabara?

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, umuhimu wa barabara hii siyo kwa Ukerewe tu, umuhimu wa barabara hii ni pamoja na Bunda ambapo anatoka Mheshimiwa Wasira; Mwibara anakotoka Mheshimiwa Lugola; Nansio na Wananchi wote wa Mkoa wa Mwanza, pamoja na Mara, kwa sababu wanaitumia katika kufanya biashara. Kwa kutambua umuhimu huu, hata Rais wakati akinadi Sera za CCM, akiwa Mwibara alitoa ahadi ya ujenzi wa Barabara hii katika kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya CCM, ndiyo maana tumeanza kuchukua hatua za kufanya usanifu ili ianze kujengwa kwa kiwango cha lami na ina urefu wa kilomita 118.

Mheshimiwa Spika, ni mahali gani panaanziwa kwa kilomita 118; tunaweza tukaanzia Bunda, tunaweza tukaanzia Mwibara, tunaweza tukaanzia Ukerewe, kitu kikubwa kinachohitajika hapa ni kuhakikisha kilomita zote 118 zinakamilika kwa kutengenezwa kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, kwenye jiwe la Babu linalocheza, mimi ninafikiri swali hili watasaidia vizuri wenzetu wa Utalii; wakalione hilo jiwe linavyocheza na nina uhakika masuala haya yanaweza yakazingatiwa.

**MHE. ALPHAXARD K. LUGOLA:** Mheshimiwa Sika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ili niulize swali la nyongeza. Kwanza, nimefarijika sana na majibu ya Waziri na ninaomba nimpigie makofi.

*Hapa (Mhe. Alphaxard K. Lugola) Alipiga Makofi*

**MHE. ALPHAXARD K. LUGOLA:** Nina swali moja la nyongeza kama ifuatavyo:- (*Kicheko*)

Kwa kuwa Barabara hii iliwekwa kwenye Mpango wa Miaka Mitano; na kwa kuwa kwenye Ilani ya Uchaguzi wa CCM hii ni barabara namba moja katika orodha: Je, Waziri anaendelea kuwaambia Wana-Mwibara kwamba hata ujenzi wake na kutengewa fedha itakuwa ni namba moja hivyo hivyo haitabadilika?

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, kwanza, ninakubaliana kabisa na Mbunge wa Mwibara kwamba, Barabara hii imetajwa kwenye Ilani ya Uchaguzi ya CCM. Ninapenda kupongeza Mbunge Lugola, kwa juhudi zake zote anazozifanya katika kuhakikisha kwamba, Barabara hii inatengenezwa kwa kiwango cha lami, kwa kushirikiana na Wabunge wengine wa Ukerewe na Bunda.

Ninataka kuwahakikishia Wananchi wanaopita katika maeneo haya, kwa sababu tumeshaanza kufanya *design* na kuna kampuni inayofanya *design* ya *Interconsult Limited* ya Dar es Salaam, wakishamaliza kufanya *design* tunahakikisha tutatafuta fedha ili Barabara hii itengenezwe kwa kiwango cha lami.

Wakati tunasubiri kutengenezwa kwa kiwango cha lami, tutahakikisha kwamba Barabara hii inatengewa fedha kupitia Mfuko wa Barabara ili iweze kupitika wakati wote.

Na. 255

**Bajeti ya Kutengeneza Barabara**

**MHE. MCH. ISRAEL Y. NATSE** aliuliza:-

Serikali ilikwishapitisha bajeti ya kutengeneza barabra toka Njia Panda ya Karatu – Mangola – Matala – Meatu hadi Lalago:-

(a) Je, Serikali haioni kuna haja ya kuwaeleza Wananchi sababu za kutotumia bajeti iliyokwishapitishwa kwa kazi hiyo?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kukamilisha barabara hiyo hadi Lalago?

**WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Mchungaji Israel Natse, Mbunge wa Jimbo la Karatu, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Barabara ya Karatu Junction – Mang'ola – Matala – Meatu hadi Lalago, yenye urefu wa kilomita 266.8, inapita katika Mikoa mitatu ya Arusha, Singida na Shinyanga. Sehemu ya Barabara hiyo ya Karatu – Mang'ola – Matala, yenye urefu wa kilomita 129.1 ambayo ipo Mkoa wa Arusha, ipo kwenye hali nzuri na imekarabatiwa kwa jumla ya shilingi bilioni 1.709 kati ya 2007/2008 na 20010/2011.

Sehemu nyingine ya Barabara hiyo ya Sibiti - Mwanhuzi hadi Lalago, yenye urefu wa kilomita 112.2 ambayo ipo katika Mkoa wa Shinyanga, ipo kwenye hali nzuri vilevile na imekarabatiwa kwa jumla ya shilingi bilioni 1.046 kati ya 2007/2008 na 20010/2011.

Mheshimiwa Spika, lakini sehemu ya Matala – Sibiti, yenye urefu wa kilometa 25.5 ambayo ipo Mkoa wa Singida na ambayo inahitaji ujenzi wa Daraja la Sibiti, linalounganisha Wilaya ya Iramba na Mkoa wa Shinyanga, imechukua muda mrefu kukamilika kutokana na kazi za kitalaamu za awali za usanifu na kumpata mkandarasi kushindwa kufikia vigezo vilivyotakiwa katika utekelezaji wa Mradi huo. Hatua hizo zitakamilika katika Mwaka wa Fedha wa 2011/2012, kwa kutangaza *tender* na kuanza ujenzi wa sehemu hii, pamoja na Daraja la Sibiti.

**MHE. MCH. ISRAEL Y. NATSE:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Waziri, nina swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa Barabara hii hupitika vizuri nyakati za kiangazi na kupitika kwa tabu nyakati za masika; na kwa kuwa Barabara hii huunganisha Mikoa mitatu ya Arusha, Singida na Shinyanga kwa umuhimu wake; je, Serikali haioni kwamba ni muda mwafaka sasa kuijenga Barabara hii kwa kiwango cha lami?

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa kwamba, Barabara hii ni muhimu na tungependa sana itengenezwe kwa kiwango cha lami, lakini kama unavyojua kupanga ni kuchagua; katika bajeti ya mwaka huu, tumepanga kuzikamilisha zile kilomita 25 pamoja na Daraja la Sibiti. Tukishamaliza kufanya hivyo, zitafuata taratibu zingine za baadaye za kuanza kufanya *feasibility study*, *detail design*, hata kumpata mkandarasi katika kiwango cha lami, itategemea upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Spika, lakini hatua ya hivi sasa ni kuhakikisha Barabara hii inayounganisha Mikoa mitatu inapitika kikamilifu, ikiwa ni pamoja na kutenga fedha za kutosha katika bajeti ya mwaka huu ili kuanza kutengeneza Daraja la Sibiti, ambalo limechukua muda mrefu.

**MHE. DKT. TITUS M. KAMANI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza.

Kwa kuwa Serikali imesitisha sasa ule mpango wa kujenga Barabara Kuu kupitia Hifadhi ya Taifa ya Serengeti ili kuhifadhi na kulinda maliasili muhimu tulizonazo Tanzania:-

Je, sasa siyo wakati mwafaka kuijenga Barabara hii iliyoulizwa kama Barabara Kuu ili iunganishe Bandari ya Tanga, Arusha hadi Ukanda wa Ziwa kwa sababu vilevile wafadhili wanaosaidia uhifadhi wa ulinzi wa wanyamapori wako tayari kusaidia katika upembuzi yakinifu?

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, kwanza, siyo kweli kwamba, tumesitisha barabara inayokwenda Musoma kujengwa kwa kiwango cha lami. Tulichoeleza ni kwamba, hatutajenga kwenye eneo la Serengeti, lakini kutoka Mto wa Mbu hadi Loliondo tutajenga kwa kiwango cha lami. Sehemu ya kutoka Mugumu na kilometa zingine 100 nazo tutazijenga kwa kiwango cha lami, lakini kwenye eneo la Serengeti ndani ndipo tutaacha kwa kuzingatia mazingira.

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana katika bajeti ya mwaka huu, tumeweka fedha kwa ajili ya kufanya *design* kwa ajili ya kuijenga barabara ya kutoka Mto wa Mbu hadi Loliondo kwa kiwango cha lami. Wakati tukiendelea na hilo, tutakuwa tunaangalia mipango mingine kwenye barabara hii muhimu, ambayo inapitia Jimbo la Mheshimiwa Kamani.

Mheshimiwa Spika, kwa hivi sasa, Jimbo la Mheshimiwa Kamani kuna kilometa 71 zinajengwa kwa kiwango cha lami kutoka Lamadi hadi Bariadi na Mkandarasi yupo kule na hivi karibuni tutakwenda kuweka jiwe la msingi. *(Makofi)*

Na. 256

**_TANESCO_ Kufuta Deni la _ZECO_**

**MHE. RUKIA KASSIM AHMED** aliuliza:-

Tanzania inafidiwa madeni yake na nchi za nje; je, kwa nini *TANESCO* isiifutie *ZECO* deni ikiwa ni hatua ya kusaidiana sisi wenyewe?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Rukia Kassim Ahmed, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mhehsimiwa Spika, utaratibu wa kufutiana madeni baina ya Tanzania na nchi ya taasisi ambazo tumekopa kwao, unafuata makubaliano yaliyotokana na majadiliano kati ya Serikali na wakopeshaji hao. Makubaliano hayo yatafafanua Sekta za Kiuchumi na Kijamii zinazokusudiwa kunufaika na kufutwa kwa madeni haya.

Madeni ya *ZECO* kwa *TANESCO* yanayotokana na uhusiano wa kibiashara, unaotokana na makubaliano ya Kimkataba baina ya Taasisi hizo mbili.

Mheshimiwa Spika, mpaka sasa deni la *ZECO* kwa *TANESCO* limefikia shilingi 50,408,062,812.44. Deni hilo lilitokana na uhusiano kati ya *TANESCO* na *ZECO,* kutawaliwa na misingi ya kibiashara kama nilivyosema kupitia Mkataba Maalum wa Kuuziana Umeme. Baada ya *EWURA* kuanzishwa na kuanza kufanya kazi mwaka 2005, Serikali kupitia Wizara ya Nishati na Madini, ilifikia ukomo wa kuidhinisha bei ya umeme na jukumu hilo kuhamishiwa EWURA kisheria. Ongezeko la bei lililoidhinishwa na *EWURA* na kuanza kutumika Januari, 2008 la asilimia 21.7 ndiyo chimbuko la kulimbikiza deni kwa *ZECO,* kwani hawakukubaliana na *Order* ya *EWURA*. Kwa mazingira yaliyopo, inakuwa vigumu kwa *TANESCO* kusamehe *ZECO* madeni yake, kwani sheria zilizopo haziruhusu kufanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, zimeanza mchakato wa kulitafutia ufumbuzi suala hili ili madeni ya *ZECO* kwa *TANESCO* yapatiwe ufumbuzi kwa malengo ya kuwezesha *TANESCO* na *ZECO* yenyewe kumudu kwa ufanisi majukumu yake ya kuwahudumia wateja wao.

**MHE. RUKIA KASSIM AHMED:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali ilijibu hapa Bungeni kuwa umeme umeanzia Kidatu kwenda Zanzibar ndiyo maana *ZECO* ikaongezewa bei ya umeme kwa asilimia 168 wakati Tanzania Bara imeongezeka kwa asilimia 21.7:-

(a) Je, umeme unaotumika Dar es Salaam haukuanzia Kidatu?

(b) Kwa kuwa mchakato wa kutafuta ufumbuzi wa suala hili umeanza; na kwa kuwa tuna uzoefu wa mifano mingi ambayo imeanza mpaka leo haijapatiwa ufumbuzi kwa mfano suala la kufungua akaunti ya pamoja ya Muungano; je, Mheshimiwa Waziri ataniambia mchakato huu utakamilika baada ya muda gani?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, hili la kwamba, umeme kwa sababu unatokea Kidatu ukienda mpaka Zanzibar ndio hiyo bei imepangwa hivyo; mimi sijui hiyo imetokea wapi! Ninachojua ni kwamba, *EWURA* ina vigezo vyake ambavyo inapanga bei kutokana na gharama za uzalishaji, gharama za usafirishaji na kadhalika; ikishafika huko inakokwenda, ina vigezo vya usambazaji.

*EWURA* wamepanga bei kutokana na vigezo vyao mbalimbali walivyopanga. Hata hivyo, nimesema kwamba, mpaka sasa hivi deni hilo limefika bilioni hamsini. Umeme unaendelea kwenda Unguja na maeneo yote. Hili suala linafanyiwa kazi baina ya hizi Wizara mbili na pia kwenye Tume ya Pamoja ya Waziri Kiongozi na Waziri Mkuu. Kwa kuwa tunasema lipatiwe ufumbuzi, ninakuomba tuvute subiri kwa sababu kiwango chenyewe ni kikubwa, lakini pia jambo la kufikisha umeme Zanzibar halina hiari.

Mheshimiwa Spika, suala la kufungua Akaunti ya Pamoja sikumwelewa.

**SPIKA:** Alikuwa anatoa moja ya mifano kuwa suala hilo halijafanyika.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, hilo kwa ruhusa yako, ninadhani lipo katika mambo ya *Joint Finance Commission*. Sasa ni Akaunti ya Pamoja, lipo huko.

**SPIKA:** Yaani alikuwa anatoa mfano kwamba, hayo mambo yenu mnayokubaliana, moja ya mfano ni Akaunti ya Pamoja, ambayo haijafanyika na hili nalo mnaahidi nini?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, labda nimsaidie Mheshimiwa Rukia; hili jambo la deni linaiathiri *TANESCO* kama linavyoiathiri *ZECO*, kwa sababu umeme huu umepelekwa na umetumika na umeingia gharama za kuzalishwa. Tunasema kwa sababu yapo masuala mazito ya Muungano, ambayo inabidi yapewe kipaumbele, suala la kupatia ufumbuzi jambo hilo ambalo ni zito kidogo, linafanyiwa kazi na tutalipatia ufumbuzi. Katika muda huu, tumekubaliana huduma itaendelea kwenda Unguja.

Na. 257

**Tatizo la Umeme – Kilombero**

**MHE. ALBERT O. NTABALIBA (K.n.y. MHE. ABDUL R. MTEKETA)** aliuliza:-

Pamoja na kuwa na Gridi mbili za Taifa katika Jimbo la Kilombero, maeneo ya Mgeta, Chita, Mbingu na Idete Gerezani yana matatizo makubwa ya umeme:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka umeme maeneo hayo?

(b) Je, ni sababu zipi zinakwamisha umeme kufikia maeneo hayo?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Abdul Rajabu Mteketa, Mbunge wa Kilombero, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, katika swali lake, Mheshimiwa Abdul Rajabu Mteketa, amezungumzia suala la kuwa na Gridi mbili za Taifa katika Jimbo la Kilombero. Ninaomba kumfafanulia kwamba, Gridi ya Taifa ni moja, hakuna Gridi mbili za Taifa katika Jimbo la Kilombero, bali kuna vyanzo viwili vya kuzalisha umeme vinavyopeleka umeme wake kwenye Gridi ya Taifa. Kuna chanzo cha Kidatu Mw 204 kinachopeleka umeme Dar es Salaam, Iringa na Morogoro na chanzo cha Kihansi Mw 180 kinachopeleka umeme Morogoro, Iringa na *Kidatu Substation*. Chanzo cha Kidatu kilikamilika mwaka 1975 na Kihansi mwaka 1999.

Katika vipindi hivyo, mahitaji ya umeme katika vijiji alivyovitaja Mheshimiwa Mbunge, kusema kweli hayakutosheleza kuteremsha umeme huo katika maeneo hayo.

Kwa sasa mahitaji ya umeme katika maeneo hayo, yameongezeka sana kiasi cha kuhitaji umeme huo kuteremshwa. Serikali kupitia Wakala wa Nishati Vijijini *(REA)*, wakishirikiana na *TANESCO*, wameshafanya upembuzi yakinifu na kujua vijiji vyote kutoka Kihansi kupitia Chita JKT, Mbingu, Namawala – Idete, umbali wa kilomita 150, ambapo kuna vijiji 16. Gharama za kupeleka umeme kwenye vijiji vyote 16 imekadiriwa kuwa shilingi bilioni 1.6.

(b) Mheshimiwa Spika, sababu kubwa inayokwamisha umeme kushuka maeneo hayo ni Serikali kukosa fedha za kugharimia utekelezaji wa mradi wa kushusha umeme kutoka kwenye njia za kusafirishia KV 220, ambazo ni *high tension*, kuupooza umeme huo na kuusambaza kwa mfumo wa KV 0.4. Hata hivyo, jitihada zinafanywa kufikisha umeme katika maeneo yaliyotajwa na Mheshimiwa Mbunge, ikiwa ni pamoja na kuwasiliana na wafadhili mbalimbali kwa nia ya kuwashawishi kutoa fedha za kugharamia utekelezaji wa Mradi huo.

**MHE. ALBERT O. NTABALIBA:** Mheshimiwa Spika, kwanza, ninashukuru kwa majibu mazuri ya Naibu Waziri. Kwa kuwa Miradi yote inayotakiwa kufanyiwa kazi inakuwa imewekwa kwenye mipango ya Wizara; na kwa kuwa kwenye Hotuba yake hakuna mahali panapoonesha kwamba hivi vijiji vinataka kupewa umeme:-

(a) Je, kwenye Hotuba yake iko ukurasa gani?

(b) Swali hilo la umeme linafanana kabisa na la Mkoa wa Kigoma; Kigoma imepewa jenereta mbili; Wilaya ya Kibondo na Wilaya ya Kasulu. Sababu kubwa wanayoambiwa ni kwamba, hawapati umeme pale kwa sababu ya waya. Sababu nyingine kwenye Mradi huu wa kupewa umeme Kigoma uliokuwa umefadhiliwa na *MCC* tulisema ni konokono. Je, Tanzania hii matatizo ya waya yako Mkoa wa Kigoma tu au sehemu zote umeme haupelekwi? (*Makofi*)

**SPIKA:** Majibu kwa kifupi, kwa sababu tunaendelea na Wizara yenyewe.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, nilichosema kwenye majibu ya msingi ni kwamba, Mradi huu wa kutoka Kihansi kwenye uzalishaji mpaka mwisho kule Mgeta, kupitia Vijiji vyote hivi vya Chita na kadhalika, umefanyiwa tathmini; kuna vijiji 16; pana umbali wa kama kilomita 150; gharama yake ni kama bilioni 1.6; ufadhili unatafutwa.

Sasa kwa maana tumeshaingia gharama za kuufanyia upembuzi yakinifu, lakini sasa tunaingia kwenye hatua ya pili ya *financial closure*, ambayo ni kutafutia fedha za kukamilisha Mradi huu. Kwa hiyo, huwezi kuiona kwenye Hotuba hiyo kwa sababu bado tupo kwenye mchakato wa kutafutia fedha; fedha itakapopatikana zitaingia huko mbele.

Mheshimiwa Spika, hili suala la waya kwa Kasulu na Kibondo, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Obama kuwa, siyo kwa Kasulu na Kibondo tu au ni kwa Mkoa wa Kigoma; suala la waya lilikuwa limekithiri hapa katikati katika Miradi mingi ya *TANESCO* pamoja na vifaa vingine vya kuunganisha na kufanya usambazaji, lakini katika miezi miwili, mitatu, hii kuna vifaa vimeingia. Ninaamini kazi zenyewe ni nyingi, lakini usambazaji utajaribu kufanywa *equitably* maeneo yote ili kazi ziweze kuendelea kidogo kidogo kwenye maeneo yote.

Nimeshakwambia Mheshimiwa Obama na Wabunge wengine wa Kigoma kwamba, tuwasiliane ili tuone utekelezaji wa Kasulu na Kibondo, kwa kukamilisha vifaa utakamilika lini. Ninashukuru.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tumechukua muda mwingi ambao siyo wa kwetu, kwa hiyo, maswali yamekwisha na muda umepita.

Waheshimiwa Wabunge, tuna wageni wachache tulionao hapa ambao nimepewa majina yao. Kuna huyu aliyekuwa Mbunge wa Kilwa, Dkt. Samson Mpanda, tunamkumbuka aliyekuwa Mbunge katika Bunge la Tisa; ameambatana na Ndugu Clepasi Mtalemwa, msaidizi wake. Ninaomba asimame Dkt. Mpanda, alikuwa Mbunge mwenzetu wa Jimbo la Kilwa, kuna mwingine ameshachukua nafasi yake. Dkt. Mpanda tulikuwa naye kwa muda mrefu, bahati mbaya katika kipindi chake akapata matatizo ya kushindwa kuona, lakini alikuwa anashirikiana vizuri sana na sisi hapa. Tunakukaribisha sana na tumefurahi kukuona tena ukiwa na afya nzuri. *(Makofi)*

Nina wageni wengine kutoka Ujerumani wamekuja kwa ajili ya uwekezaji kwenye Miradi ya Umeme wa jua. Hawa ni wageni wa Mheshimiwa Kabwe Zitto. Sasa hawa wageni kutamka majina itakuwa tatizo, lakini hivyo hivyo; kuna Mkurugenzi wa *People's Home Association* ya Ujerumani, Ndugu Ulrich Creshma; *I don't know where you are;* ahsante sana. Kuna Mkurugenzi wa *African BID* ya Ujerumani, Ndugu Tumenta Kennedy; huyu ni mwenzetu ndiyo maana tumeweza kutamka. (*Makofi*)

Kuna Walimu 35 kutoka Shule ya Msingi ya Mazengo Dodoma; karibuni sana. Halafu tuna Mke Mpendwa wa Naibu Waziri wa Nishati na Madini, Mheshimiwa Kigoma Malima. Huyu mama anaitwa Naima Chonde Malima na mtoto wao mdogo. Haya mama simama tukuone. Anasema amekuja kumpa moyo mtakapokuwa mnamsulubisha hapa. Ahsante sana. Vilevile wageni wengine wote mnakaribishwa Bungeni kwa ajili ya watu wote. *(Makofi)*

Taarifa za kazi; Mheshimiwa John Mnyika, yeye ni Katibu wa Wabunge wa CHADEMA, anaomba niwatangazie Wabunge wa CHADEMA kuwa, leo tarehe 18 saa 9.00 mchana, kutakuwa na kikao katika Chumba Namba 219.

Nina tangazo kutoka kwa Mheshimiwa Dkt. Titus Kamani, yeye ni Katibu wa Wabunge wa Mkoa wa Mwanza wanaolima pamba. Anasema kwamba, niwajulishe Wabunge wote wanaotoka Mkoa wa Mwanza kuwa, leo saa saba mchana, kutakuwa na kikao chao katika Ukumbi wa Msekwa B.

Waheshimiwa Wabunge, katika *pigeon holes* zetu tumeweka Hotuba ya Rais juu ya Mpango wa Kwanza wa Maendeleo ya Miaka Mitano (2011 na 2015) wa utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2025. Pia kuna *The Public Private Partnership Act, 201*0; halafu kuna *National Public Private Partnership (PPP) Policy;* halafu kuna *The Public Private Partnership Act Regulations.* Kwa hiyo, hizi ndiyo *documents* ambazo ziko kwenye *pigeonhole* zetu mnaweza kuzichukua na kuzisoma.

Ninapenda kuwaarifu Waheshimiwa Wabunge wote kuwa, matokeo ya michezo iliyochezwa Jumamosi kati ya Timu ya Waheshimiwa Wabunge na *PSPF* ni kama ifuatavyo:-

Mpira wa Miguu, Timu ya Waheshimiwa Wabunge, walifunga magoli mawili na *PSPF* walifunga goli moja na kikombe wanacho lakini sikileti hapa. Mpira wa Pete, Timu ya Waheshimiwa Wabunge ilifunga magoli 30 na *PSPF* walifunga magoli sita.

Kwa hiyo, nyota wa michezo hiyo ni Mheshimiwa Amos Makalla, kwa timu ya miguu na Mheshimiwa Asha Mshimba Jecha, kwa timu ya pete. Nikiwataja mnatakiwa kusimama si mko humu ndani; hongera sana. Aidha, kwa ushindi huo, Timu ya Waheshimiwa Wabunge, imefanikiwa kutwaa zawadi ya vikombe vyote viwili vilivyoandaliwa na *PSPF* kwa michezo hiyo, lakini hatutavileta humu ndani.

Waheshimiwa Wabunge, tuna tangazo lingine la tanzia; Mheshimiwa Naibu Spika, Job Ndugai, amefiwa na bibi yake mzaa mama, ambaye ndiye aliyemlea. Amefariki juzi huko Kongwa na mazishi yatafanyika huko huko Kongwa, kesho tarehe 19 Julai, 2011, Saa 9.00 alasiri, yakitanguliwa na ibada ya mazishi saa 7.00 mchana. Huyu bibi yake alikuwa kama mlezi wake, maana baada ya kufariki mama yake, basi ndiyo alikuwa anamtunza.

Mama yake alikuwa anamtunza bibi, mama yake ametangulia na sasa bibi naye ametangulia hivi juzi. Kwa hiyo, kwa wale watakaokuwa wanakwenda, basi Ofisi yetu itakuwa na utaratibu. Ahsanteni sana.

Waheshimiwa Wabunge, ninajua kuna wengi wangependa kuchangia Wizara hii, lakini haitawezekana, kila kitu lazima kiwe na mwisho. Kutokana na uzoefu tulioupata toka tumeanza, tutachangia mpaka saa 7.00, saa 11.00 wataanza kujibu hoja na kuingia kwenye kazi inayofuata; ndiyo hali itakavyokuwa.

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2011/2012
### Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi

*(Majadiliano yanaendelea)*

**SPIKA:** Watakaoanza kuchangia sasa ni Mheshimiwa Omary Badwel, Mheshimiwa Eustace Katagira, Mheshimiwa Rebecca Mngodo na Mheshimiwa Dkt. Hamisi Kigwangala.

Mheshimiwa Naomi Kaihula, Mheshimiwa Silvestry Koka, Mheshimiwa Lolesia Bukwimba, Mheshimiwa Beatrice Shellukindo wamebadilishana nafasi na Mheshimiwa Anastazia Wambura na Mheshimiwa Faith Mitambo.

**MHE. OMARY A. BADWEL:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuwa mtu wa kwanza siku ya leo, kuchangia Hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini.

Mheshimiwa Spika, ninayo mambo mengi ya kuchangia katika Wizara hii, lakini nitaanza na jambo muhimu katika Wilaya yangu kuhusiana na madini ya *uranium,* kwa maana ya uchimbaji wa madini ya *uranium* katika Wilaya yangu ya Bahi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwaka 2007 wakati ulipokuwa umeanza utafiti, tulimwita Mheshimiwa Waziri, kwa sababu hatukuwa na taarifa zozote, aje katika Wilaya ya Bahi kutoa ufafanuzi juu ya uchimbaji wa madini ya *uranium*.

Ninataka nikwambie na niliarifu Bunge hili kuwa, mpaka leo Mheshimiwa Waziri, hajatoa taarifa zozote baada ya kukubaliana juu ya suala zima la uchimbaji wa madini katika Wilaya yangu.

Hivyo, kutokana na suala hilo, ninakusudia kuungana na Wananchi zaidi ya 6,000 ambao tayari wameniandikia barua ya kupinga uchimbaji wa madini hayo ili nilete hoja binafsi ndani ya Bunge hili kupinga uchimbaji huo kutokana na kutokushirikishwa kikamilifu kwa Wananchi wa Jimbo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika**,** katika jambo hili Serikali imekuwa kama haipo, imeachia baadhi ya *NGO*, imeachia baadhi ya wanasiasa kwenda kuwatia hofu wananchi, kwenda kuwashawishi ili kufanya fujo juu ya suala la kupinga uchimbaji wa madini ya *uranium.* Lakini mimi niwaambie wachimbaji wa Jimbo la Bahi, mimi ndiye Mbunge wao, ndiye walionichagua kwa kura zao tena za kutosha na kupata zaidi asilimia 94.6. Naomba waendelee kuniamini, niko pamoja nao katika suala zima la uchimbaji wa madini ya *uranium* mpaka kieleweke. *(Makofi)*

Hao wanaokwenda kuwashawishi wana Majimbo yao, wana maeneo yao, wakafanye kazi walizotumwa na wananchi katika maeneo yao na siyo katika Jimbo langu la Bahi. Mimi nina uwezo wa kutosha, mimi ni Mbunge ninayetosha na niliyekamilika na ndiyo maana wananchi wakanichagua. Sina sababu ya kuja kusaidiwa na mtu yeyote ndani ya Jimbo langu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kuwasisitiza na kuwaomba sana wananchi kwa ridhaa waliyonipa kuwa Mbunge wao ili waendelee kuniamini, na nitafanya kazi hii vizuri na wenyewe wataamini hatima ya suala zima ya madini ya *uranium* itakavyokuwa baada ya mimi kushirikiana nao kikamilufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili, nachukua nafasi hii kutoa shukurani kwa Serikali kwa sababu katika Wilaya ya Bahi mpaka mwaka 2007 tulikuwa tuna kijiji kimoja tu chenye umeme na umeme huo ulidumu katika kijiji hicho Mndemu kwa miaka 20, lakini hivi karibuni Serikali imetupelekea umeme katika Makao Makuu yetu ya Wilaya na umeme huo ukashuka katika kijiji kimoja cha Ibihwa. Lakini hili nimeshalizungumza na narudia kulisema kwa Waziri kwamba ahadi ya kushusha umeme unaokwenda Wilayani ilikuwa ni pamoja na kuushusha katika Kijiji cha Kigwe na Kijiji cha Mpamantwa ambao mpaka sasa umeme huo haujashuka. Kwa hiyo, nilikuwa naomba, pamoja na mazuri ambayo nimepewa, nilikuwa nasisitiza suala zima la umeme huo kushuka katika vijiji hivi.

Mheshimiwa Spika, katika miradi ya *MCC*, suala la Wilaya yangu ya Bahi nasikitika sana kwa sababu katika Mkoa wa Dodoma ziko Wilaya sita. Ukiangalia katika miradi iliyokwenda miradi ya MCC, Wilaya ya Kondoa - vijiji sita, Wilaya ya Mpwapwa - vijiji 14, Kongwa 13, Chamwino 10 na Dodoma Mjini 14, lakini Wilaya ya Bahi tumepewa vijiji viwili tu jambo ambalo mimi silikubali. Kwa kweli ni uonevu kwa wananchi wa Wilaya ya Bahi. Mpaka sasa Wilaya nzima yenye vijiji 56 tuna umeme katika vijiji vitatu tu, lakini leo bado tunapewa vijiji viwili kwa ajili ya miradi ya *MCC*. Kwa hiyo, nilikuwa naomba nipate maelezo juu ya kwa nini Wilaya yangu imepata vijiji hivyo viwili na sio zaidi au ilingane na Wilaya nyingine?

Mheshimiwa Spika, sisi Wabunge tumesisitiza hapa suala la kupeleka umeme vijijini, lakini kuunganisha umeme ni ghali, ukiachilia ile bili yake ya mwezi ya kawaida. Wananchi wengi wa vijijini kwa kweli uwezo wao wa kuunganisha umeme umekuwa duni na mimi namtaka Mheshimiwa Waziri akafanye utafiti katika kijiji changu Mndemu tu ambacho kina umeme zaidi ya miaka ishirini iliyopita na kuna nyumba nyingi za kisasa, lakini wananchi waliounga umeme katika miaka hiyo ishirini, hawafiki asilimia 10. Hii inatokana na ughali wa uunganishaji. Napendekeza kwamba Serikali iangalie upya utaratibu hasa vijijini kama wata-*charge* asilimia 100 mijini, basi angalau wapunguze asilimia 60.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tunahitaji utulivu ndani ya nyumba.

**MHE. OMARY A. BADWEL:** Mheshimiwa Spika, katika maeneo ya vijijini ipunguze ifike angalau ifike asilimia 60 ya gharama nzima ya uunganishaji umeme na tena ziandaliwe namna ambavyo zinaweza kulipwa kwa awamu ili wananchi wengi ambao kwa kweli vijijini hawana uwezo wa kutosha, waweze kuunganisha umeme pia na wao waweze kunufaika na hii hali ya kuwepo na umeme katika ameneo yao. Kwa hiyo, ni matumaini yangu kwanba Serikali itapokea rai hiyo, itafanya utafiti na kuona namna ambavyo inaweza ikawasaidia wananchi wa vijiji katika kuwapunguzia bei, lakini pia kuwawekea walipe kwa awamu ili wengi wao waweze kuunganisha umeme katika maeneo ya vijijini.

Mheshimiwa Spika, pia nilikuwa nataka nizungumzie habari ya mawe ambayo yamekuwa yakichukuliwa na wajenzi wa barabara katika maeneo yetu mbalimbali. Hili nataka niseme tu kwamba limekuwa utaratibu wa Wizara na sheria mbalimbali ambazo zimekuwepo, zimekuwa haziendi kuwashirikisha wananchi na ndiyo maana katika hili suala la *uranium* tunapiga kelele. Kwa mfano, leo mkandarasi anataka kuchukua mawe ya kujenga barabara ya lami. Kwa mfano, barabara inayotoka Dodoma kwenda Kondoa anakwenda katika kijiji anataka mawe, achukue pale. Lakini wananchi wanamwambia, haya ni mawe yetu, tukubaliane mara moja, Wizara inakuja inasema yale mawe ni ya Serikali Kuu na mawe yale yatachukuliwa bila kijiji kile kupata manufaa yoyote. Kwa mfano, katika Kijiji cha Mndemu sasa hivi tunao mgogoro pale, wananchi wanataka walipwe kwa ajili ya mawe yao, lakini Mkandarasi anakataa na wa Wizara wamekwenda pale wanasema kwamba mawe yale ni ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, sisi katika vile vijiji tuna matatizo mengi, mbona sementi hamwapi kutoka Serikalini? Mbona *material* mengine wananunua? Kwa nini mawe wasinunue katika maeneo yetu na mimi naamini mkandarasi anapoambiwa jenga barabara hii ya lami kutoka Dodoma kwenda Kondoa analipwa na fedha za kununua mawe na kokoto. Kwa nini sasa mawe yale ya kijijini kwetu yachukuliwe bure eti kwa sababu ni mawe ya Serikali Kuu? Nilikuwa nashauri lazima jambo hili tupatiwe majibu, tujue ni kwa nini mawe yetu yachukuliwe bure na mchanga na bidhaa nyingine wakati wakandarasi wanapojenga barabara za lami au barabara nyingine?

Mheshimiwa Spika, pia nizungumzie habari ya chumvi. Katika maeneo ya Bahi tunavyo vijiji ambavyo kimsingi wanatengeneza chumvi, lakini sijawahi kuona hata siku

moja Serikali inatambua kwanza uwepo wa viwanda vile ingawaje vinatengeneza kienyeji, lakini vinatoa tani za chumvi, zinakwenda kuuzwa, lakini hakuna utaratibu mzuri wa uwekaji wa madini ya *iodine,* kwa hiyo, ile chumvi inaondoka pale kienyeji. Lakini pia hakuna utaratibu wowote wa kuwasaidia wananchi wa maeneo yale ili waweze kutengeneza hizo chumvi kwa mbinu za kisasa ambazo zitawapunguzia gharama ili waweze kupata faida kubwa wakati wanatengeneza hizo chumvi.

Mheshimiwa Spika, nimesikia kuna mitambo, kuna utaratibu mpya za uchimbaji wa chumvi na ukaushaji wa chumvi katika maeneo mbalimbali. Nilidhani kwamba umefika wakati katika Wilaya yangu ya Bahi, wananchi wanaochimba chumvi katika vijiji vya Igongo, Chaligongo, Ilindi na Kijiji cha Chipanga ‘B’ ili na wao waweze kupata utaratibu mzuri wa namna ya kuweza kutengeneza hizo chumvi zao bila kupata gharama kubwa.

Mwisho, nimalizie kwa kusema kwamba Serikali imetoa ahadi nzuri sana katika suala zima la kutatua tatizo la umeme katika nchi yetu. Lakini kauli hizi zimetolewa kwa muda mrefu, tunalo tatizo sasa kwa miaka kadhaa ya suala la kutokuwepo umeme katika nchi yetu na kumekuwa na manung’uniko makubwa, wananchi wamepata hasara, ajira zimepungua, wananchi wanaendelea kuwa na manung’uniko na inafika mahali sasa wanapoteza imani kwa Serikali yao juu uwezo wa kutatua matatizo yao kwa haraka. Nilidhani wakati wa maneno umekwisha, lazima sasa Serikali ichukue hatua na ifanye maamuzi na ikiwezekana ifanye maamuzi magumu juu ya suala la kumaliza tatizo la umeme katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo hii watu hawana amani na biashara zao, hawana amani na ofisi zao, hawana amani na makazi yao, tunaogopa usiku ukifika taa zimezimika, ujambazi unaongezeka na uhalifu unaongezeka. Kwa kweli ni vizuri sana Serikali ikaliona hili na ikasaidia kuhakikisha kwamba inatatua tatizo la umeme katika nchi yetu. Haipendezi wala haiwatii moyo wananchi kuendelea kupata maneno. Wananchi wa leo hawataki maneno, wanataka vitendo na hili tutaliona, kama hatukufanya bidii tutaliona mwaka 2015. Ni lazima kujipanga sasa na kuhakikisha kwamba muda mfupi ujao, suala la umeme na tatizo la umeme katika nchi yetu linabaki kuwa historia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia katika suala hili, lazima tuiambie Serikali Kuu, ukiangalia katika utaratibu mzima wa Wizara ya Nishati na Madini katika mwaka unaokwisha haikupata fedha za kutosha. Serikali yenyenye ambayo tumepitisha bajeti hapa Bungeni asilimia 50, zaidi kidogo imeipa Wizara ya Nishati na Madini. Tunategemea nini? Mara nyingine tutamlaumu sana Mheshimiwa Ngeleja, lakini atafanya nini? Hapati fedha tulizokuwa tumempitishia hapa Bungeni. *(Makofi)*

Kwa hiyo, tunapitisha fedha hapa Bungeni, lakini Serikali haifanyi bidii ya kuzipeleka fedha hizo katika maeneo hayo. Hii siyo katika Wizara hii tu ya Nishati na Madini, tumeona hata katika maeneo mengine Serikali imeshindwa kupeleka fedha za kutosha. Viongozi mbalimbali wanaosimamia kazi za maendeleo, wameanza kukata tamaa juu ya udhaifu wa Serikali katika kupeleka fedha za maendeleo kama ambavyo tumezipitisha kwenye Bunge na tulivyopitisha kwenye Halmashauri zetu. Kwa hiyo,

hatuwezi kuisaidia Wizara hii kwa mtindo huu ambao tunaendelea nao wa Serikali kutokuipa kipaumbele. Tunaitaka sasa Serikali katika hii bajeti tunayopitisha itoe kipaumbele cha kuhakikisha kwamba Wizara hii inapewa fedha zake asilimia mia moja na kwa kweli tutakuja kuibana vizuri, hatutakubaliana kabisa. Safari hii tutapitisha bajeti hii ya Wizara ya Nishati na Madini, lakini mwakani hatutaipitisha Wizara hii kama hatukupata majibu ya kutosha na fedha hazikwenda za kutosha katika Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. EUSTACE O. KATAGIRA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia fursa ya kuchangia katika hoja hii ya Wizara ya Nishati na Madini. Sina haja ya kurudia kusisitiza umuhimu wa umeme katika uchumi wa Taifa hili. Wengi wameongelea, ieleweke tu kwamba kuwa na upungufu wa umeme kunasababisha kudorora kwa uchumi, kunasababisha uzalishaji mbaya, kunafanya bei za bidhaa zipande na hivyo kuleta *inflation* ambayo mwisho wake ni kufanya maisha ya Watanzania yadorore na maisha bora yasipatikane.

Mheshimiwa Spika, napenda nisisitize kabisa kwamba jitihada ziendelee kufanywa kwa nguvu kabisa ili tatizo hili tuondokane nalo ili maisha ya Mtanzania yaweze kuboreka na uchumi uweze kusonga mbele.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Kagera, ardhi ambayo inapatikana katika maeneo mengine ya Tanzania, kule Mkoani Kagera, tuna ahuweni kidogo kwa sababu tunapata umeme kutoka majirani wetu wazuri wa nchi ya Uganda. Lakini mswahili husema kwamba: “Titi la mama ni bora kuliko titi la mama wa kambo.” Titi la mama ni titi lako, unanyonya unapotaka na una uhakika kuwa utaendelea kuwepo. Lakini titi la mama wa kambo, inawezekana siku nyingine akakunyima, inawezekana akazaa mtoto wake mwenyewe na ukawa huwezi kunyonya. Kwa hiyo, tunaomba juhudi za Serikali za kuhakikisha kwamba Mkoa wa Kagera unaunganishwa katika umeme unaotokana na nchi yetu ya Tanzania uendelezwe na utiliwe mkazo ili hatimaye tuweze kuwa tunapata umeme katika nchi yetu, mtandao wa nchi ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, ninaposiama hapa nikaongelea habari ya adhaa ya mgao wa umeme nina hakika baadhi ya wananchi katika Wilaya ya Kyerwa wananishangaa maana katika Wilaya nzima ya Kyerwa hakuna hata nguzo moja ya umeme. Maana katika Wilaya ya Kyerwa hakuna friji. Ukipeleka friji leo katika Wilaya ya Kyerwa watakushangaa, wataweka nguo humo ndani wakidhani kwamba ni sanduku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nasimama kuleta masikitiko makubwa ya wananchi wa Wilaya ya Kyerwa kwa kutotendewa haki. Wananchi wa Wilaya ya Kyerwa kuna ahadi ambazo zimetolewa mara mbili na Mheshimiwa Rais. Mara ya kwanza katika ziara yake katika Mkoa wa Kagera amekwenda mpaka sehemu ya Murongo inaitwa *casket* ambapo aliahidi baada ya kutembelea na kuangalia na kuona kwamba umeme utaweza kuzalishwa. Katika Mkutano wa hadhara pale Murongwa alisimama akawaahidi wananchi kwamba sasa juhudi zitaanza za kuzalisha umeme pale mpakani na Uganda ili

ule uweze kutumika na kusambazwa katika vijiji vya Wilaya ya Kyerwa. Lakini katika ziara yake yote katika Wilaya ya Kyerwa alieleza kabisa hata pale Isengiri, kila mahali kwamba umeme utazalishwa pale Murongo na utasambazwa katika Wilaya ya Kyerwa na Wilaya ya Karagwe.

Mheshimiwa Spika, mpaka mwezi Oktoba, 2010, katika Mkutano Mkuu wa pale Nkwenda, Mheshimiwa Rais alirudia akayaeleza na akawaahidi wananchi katika Mkutano mkubwa sana akasema umeme unakuja. Lakini zaidi ya hayo, aliambatana na Waziri wa Nishati na Madini - Mheshimiwa Ngeleja. Baada ya kueleza, Mheshimiwa Rais alimwomba Mheshimiwa Ngeleja ayaseme mwenyewe. Nikapanda naye kwenye jukwaa Mheshimiwa Ngeleja akashangiliwa sana na wanawake na watoto wa Kyerwa, akawaahidi akasema siyo ahadi tu, ni kwamba mikakati imeshaanza. Leo ninapoangalia kwenye kitabu chake habari ile ya Kyerwa haipo.

Pia akumbuke Mheshimiwa Waziri kwamba sasa hivi kuna teknolojia, mimi nimekuwa nazunguka katika Wilaya ya Kyerwa, Jimbo la Kyerwa na nikienda wazee na watoto, jambo la kwanza kabla ya Mkutano wananiwekea *speech* yake, wanasema umeme unakuja na mimi nawapa ahadi nasema Serikali ya CCM haidanganyi, mlimwona Waziri mwenyewe alisimama pale akaahidi kwamba umeme unakuja, siyo kwamba anatafuta pesa, alisema pesa zipo.

Mimi naomba wakati nikirudi kule Kyerwa wazee wanaomba Mheshimiwa Waziri niende naye kwenye Mkutano mmoja tu asimame awaelezee hatima ya umeme ambao alisema siyo suala la kutafuta pesa, kwamba ni suala la kuanza mradi kuutekeleza. Umeme huu ulikuwa ufaidishe Kata zote za Kyerwa, Kata ya Murongo, Kaishoki, Kaisingiro, Kyerwa, Nkendwa, Kimuli, Kamuli, Mabira na Kata nyingine zote wanajiandaa.

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri aliweke maanani asinifanye mimi mwongo, lakini yeye asije akadhaniwa kwamba aliwadanganya, lakini zaidi alinde heshima ya Serikali ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia kuhusu wachimbaji wadogo. Mwaka jana wananchi wa Kata ya Murongo walipata msiba wakaenda wakaanza kuchimba kaburi. Walipofika nusu ya kaburi, wakakuta kuna *tin* nyingi sana, madini ya *tin*. Masikini marehemu wakamweka pembeni wakaanza kushughulikia *tin* kuitoa, lakini kwa ukarimu wao na uzuri wao baadaye marehemu alizikwa pia. Katika maeneo hayo yote wananchi wanaweza kuchimba *tin,* wachimbaji wadogowadogo. Natoa rai, naiomba Serikali isije sasa ikaanza kwenda kuwafukuza na kuwafurumisha kwamba waondoke kwamba ni wachimbaji wakubwa, kwamba ni kampuni Fulani. Haya madini ya *tin,* wameyatafuta wenyewe, wameelewana wenyewe. Naomba Serikali kupitia kwa Ofisi ya Madini ya Kagera, watendeeni haki, watende ambayo wanapaswa kutenda, wawaelimishe, wawasaidie ili na wenyewe waweze kufaidika na madini haya ya *tin,* lakini wasiende na makaratasi kwamba hili ni eneo la fulani, la kampuni fulani na wenyewe waachwe wafaidike na madini yaliyo katika eneo lao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wilaya wa Karagwe, kuna mradi wa kusambaza umeme umeanza. Huu mradi katika eneo ambalo Mbunge mwenzangu, jirani yangu Mheshimiwa Blandes tunashirikiana sana katika kutetea maendeleo katika eneo letu, anayafuatilia kwa karibu. *(Makofi)*

*Speed* ya mradi huu, haipendezi, haitii nguvu. Tarehe 6 Aprili, 2011 Mheshimiwa Waziri alikuwa anajibu swali la Mheshimiwa Blandes, Mbunge mwenzangu, jirani yangu ambaye tunasukuma wote maendeleo katika Wilaya ya Kyerwa na Wilaya ya Karagwe. Alijibiwa na Mheshimiwa Waziri kwamba umeme wa kwenda Kiruruma, Nyakagoyegoye, Nyakaiga, Rwambaizi kwamba pesa zipo ziko tayari. Leo tunaangalia katika kitabu cha Mheshimiwa Waziri, hamna kitu, hamna pesa za kupeleka umeme Kiruruma, Nyakaiga, Rwambazi. Tuseme tarehe 6 Aprili, 2011 Mheshimiwa Waziri ambaye ni makini kabisa tunamfahamu katika kujibu swali hili la Mheshimiwa Blandes, Mheshimiwa Waziri alikuwa anatudanganya? Wazee kule wanatuuliza, walisikia, wakashangalia, wakanywa rubisi kidogo wakasema umeme unakuja, pesa zipo. Sasa leo twende tuwaambie nini?

Mheshimiwa Spika, naomba wakati Mheshimiwa Waziri anakuja kuelezea Wanakyerwa kwamba umeme upo, mradi upo, apitie pia katika Jimbo la Karagwe aende ayaseme mwenyewe aliyoyasema katika jibu la swali la Mheshimiwa Blandes ili mambo yote yawe sawa, ili wananchi warudiwe na imani yao katika Waziri wao, katika Serikali yao.

Mheshimiwa Spika, napenda kukushukuru tena kwa kuniruhusu niweze kuongea na niseme nitasubiri *messages* za wananchi wangu wa Jimbo la Kyerwa wakiniruhusu niunge mkono hoja, nitaunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

**SPIKA:** Ahsante. Sasa namwita Mheshimiwa Rebecca Mngoda.

**MHE. REBECCA M. MNGODO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia hotuba hii ya Waziri wa Nishati na Madini. Lakini kabla ya kuchangia, naomba nieleweshe jina langu, naitwa Rebecca Mngodo. Ni Mngodo.

**SPIKA:** Mngodo!

**MHE. REBECCA M. MNGODO:** Ndiyo.

**SPIKA:** Kule kwetu kuna Mngoda, kwa ndiyo maana ninachanganya.

**MHE. REBECCA M. MNGODO:** Ahsante.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, nataka nichukue nafasi hii nimshukuru Mungu, kwamba ni mwingi wa rehema na ameweza kunipa neema yake na kunijalia mimi kuwa Mbunge katika Bunge hili lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda pia nimpongeze Mwenyekiti wetu, Mheshimiwa Freeman Mbowe, ambaye ni Mwenyekiti wa Chama chetu cha *CHADEMA* na Mbunge wa Hai na pia Kiongozi wa Kambi ya Upinzani kwa ujasiri mkubwa aliokuwa nao ya kwamba licha ya kuwekwa ndani, ameweza kukiongoza chama chetu na chama kinaendelea kupendwa na kupata wafuasi kila siku. *(Makofi)*

Pia napenda nimshukuru Dkt. Wilbroad Slaa aliyekuwa mgombea wa Urais mwaka 2010 kwa kazi kubwa sana aliyoifanya kwa safari nyingi alizozifanya katika Tanzania katika Mikoa, Wilaya na Vijiji licha ya ubovu wa barabara. Lakini Mheshimiwa Dkt. Slaa aliweza kufanya kazi kubwa na Wabunge wengi wakapatikana wa majimbo na viti maalum na mimi nikiwa mmojawapo na kwa sababu hiyo namshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Wilbroad Slaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Tanzania ni nchi nzuri, inapendeza, ina madini mbalimbali, na raslimali nyingi. Nilipokuwa naangalia ile hotuba ya Mheshimiwa Ngeleja, niliona katika jedwali za aina za madini yanayopatikana katika nchi yetu na sehemu ambayo madini yanapatikana, nilishangaa kuona kwamba karibu Tanzania nzima kuna madini ya aina mbalimbali na mengine hata kwa majina nilikuwa sijawahi kuyasikia. Lakini cha kushangaza ni jinsi ambavyo Serikali yetu imeweza kuifikisha nchi yetu katika hali tuliyonayo sasa hivi ya kwamba ni watu wachache wanafaidi madini wakati wananchi wengi wakiendelea kuteseka, wakiendelea kupata taabu hasa wanawake na watoto. *(Makofi)*

Nitatoa mfano mmoja na hasa nikishukuru pia Chama chetu kwa mpango wake mzuri wa Operesheni Sangara. Mwezi wa Tatu 2011 tulipokuwa kule Shinyanga, kuna sehemu inaitwa Maganzo, nilishangaa kuona pale tulipokuwa tumesimama palipokuwa na jukwaa kulikuwa kuna machimbo madogo madogo mengi. Lakini cha kushangaza ni kwamba wananchi wa pale Maganzo hasa vijana ni wachovu, wamepigika huku ardhi yao ya Shinyanga ikiwa imejaa almasi na isitoshe tukaambiwa kwamba pale pana ubaguzi, na nataka kujua kwa nini ubaguzi katika karne hii ya leo miaka 50 tangu tupate uhuru kuna ubaguzi wa rangi?

Mheshimiwa Spika, Vijana wenye rangi nyeusi kama mimi wameshikwa, wamewekwa ndani kwa sababu eti wamechimba almasi. Lakini watu wenye rangi nyeupe wenye asili ya Kiasia, uongozi wa Kijiji cha Maganzo umewaruhusu watu wale wenye asili ya Kiasilia kuchimba madini ya almasi pale Maganzo tena bila kuwa na leseni.

Mheshimiwa Spika, huu ni ubaguzi na tungependa kujua kwa nini ubaguzi unaendelea mpaka leo? Ndiyo maana CHADEMA tukasema katika Sera yetu ya kwamba elimu bure inawezekana. Kwa sababu tunajua nchi yetu ni tajiri, ina raslimali nyingi na endapo zile raslimali zingeweza kugawanywa katika usawa, wananchi wengi wangeweza kuendelezwa kielimu, elimu ikapatikana bure, tukawa na barabara bora zaidi,

tukawa na reli, tukawa na huduma za afya ambazo ni bora, lakini mpaka wakati huu ambapo tunakaribia kuadhimisha miaka hii 50 watu wanaendelea kuteseka na ubaguzi bado unaendelea katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hii haiwezekani na siyo njia nzuri. Tunahitaji kubadilika, tunahitaji kuwa na uzalendo, tunahitaji kuwafikiria wengine wanaoteseka, tunahitaji kuweka utaratibu ambao kila Mtanzania ataweza kufaidika na zile raslimali tulizonazo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, siyo bahati mbaya sisi kuzaliwa hapa Tanzania na kwamba madini haya yapo hapa Tanzania, lakini ni ushahidi tosha kwamba ni urithi ambao Mungu ametupa ili tuweze kufaidi wote. Siyo watu wachache kufaidi na wengine kuendelea kuteseka. Kwa sababu hiyo, nakubaliana na usemi unaosema kwamba: “Taifa linaweza kuangamia kama hakuna maarifa.” Taifa letu linaweza kuendelea kuangamia ikiwa hatutaweza kuwa na maarifa.

Nikiingia upande wa umeme, sasa ni miaka 19 sasa tangu nchi yetu imeingia katika janga la ukosefu wa umeme. Mwaka 1992 ambapo nchi yetu ilikumbwa na ukame mkubwa, wanyama walikufa na chakula kilikosekana. Umoja wa Mataifa ukawa na Mkutano kule *Rio De Janeiro Brazil,* Tanzania ikapeleka Wajumbe 40. Kilichozungumzwa kule, kilikuwa ni tabia nchi na waliporudi badala ya kuleta mawazo ya kubuni mradi ambao utaisaidia *TANESCO* kuweza kuwa na umeme ikabuniwa miradi ambayo ilikuwa ni miradi ya kifisadi, miradi ya kiunyonyaji na ambayo mpaka leo hii ni miaka 19 bado nchi yetu tunaendelea kuwa gizani. *(Makofi)*

Ikaja Richmond ambayo haikuwa na fedha ya kujiendeleza wala ujuzi wa kazi iliyoombwa. Baadaye ilipoonekana kwamba makelele ya wapinzani na waandishi wa habari yanazidi, ikabadilishwa ikawa *Downs* na hivi karibuni tumesikia tena kitu kinaitwa *Symbion Power*. Sasa mimi wakati ninajaribu kusoma Katiba ya nchi yetu ili kujua ni nani huyu anayepitisha mikataba?

Mheshimiwa Spika, nikakuta katika kipengele cha Ibara ya 63, kwa ridhaa yako naomba kusoma Ibara ile ya 63(3)(e) kwamba: “Kwa madhumuni ya utekelezaji wa madaraka yake, Bunge laweza kujadili na kuridhia mikataba yote inayohusu Jamhuri ya Muungano na ambayo kwa masharti yake inahitaji kuridhiwa.”

Sasa mimi nikawa najiuliza kwamba ni nani huyu anayeridhia mikataba kama siyo Bunge letu hili? Hili la Simbioni tumelisikia mimi nikiwa hapa, sasa sielewi ni nani anayeridhia hii mikataba na kuipitisha na kwa vile ni mikataba inayokuwa ya siri inaweza kuwa ndiyo sababu inaendelea kudidimiza nchi yetu na tunaendelea kuishi katika giza. Umefika wakati sasa tuweze kuingiza sekta binafsi pia.

Mheshimiwa Spika, wenzetu wa Kenya, walikuwa na tatizo la umeme pia mwaka 1992. Nao pia walikuwa na ukame kama uliokuwa umetupata sisi. Lakini kwa sasa hivi kwa vile wao wameshirikisha sekta binafsi, hata kuna vijana wameweza kujiunga pamoja, wakaweza kuzalisha umeme na wale vijana wanauza umeme. Nchini Kenya mtu

yeyote anaweza akapewa kibali akazalisha umeme. Imefika mahali na sisi Watanzania tuwaingize wafanyabiashara ambao ni wa sekta binafsi na wao pia waweze kuzalisha umeme. Pengine wanazuiwa. Kwa sababu wakiweza kuingizwa na wao itazuia wale ambao wana mawazo ya kiunyonyaji na kiufisadi. Kwa hiyo pengine wanawazuia watu binafsi ili wao waendelee kutunyonya na waendelee kutupeleka katika giza. Sijui kama Serikali ina dhamira iliyo njema.

**TAARIFA**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, UWEKEZAJI NA UWEZESHAJI:** Mheshimiwa Spika. Taarifa.

**SPIKA:** Nini Mheshimiwa Waziri?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, UWEKEZAJI NA UWEZESHAJI:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni namba 68 (8) "Mbunge yeyote anaweza akasimama na kutoa taarifa hapa." Naomba kwa heshima na taadhima na kwa ruhusa yako nimpe taarifa Mheshimiwa Mbunge aliyekuwa anaongea hapa kwamba kwa mujibu wa Sheria tuliyoleta hapa na Bunge lako Tukufu likapitisha, suala la ubia kati ya Sekta Binafsi na Sekta ya Umma, Serikali ya Tanzania na Bunge lako limeruhusu na sekta binafsi ishiriki katika kujenga uchumi. Kwa hiyo naomba apate taarifa hii na ajue kwamba sisi tumekwenda mbele kama ilivyo Kenya.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mngodo, ni kweli kwamba tumetunga sheria kuruhusu watu binafsi pia kuendeleza na kuleta umeme. Naomba uendelee na mchango wako.

**MHE. REBECCA M. MNGODO:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Lakini hiyo taarifa kwa kweli ...

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, unasema unakubali. Endelea na shughuli zako.

**MHE. REBECCA M. MNGODO:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Badala ya Serikali kutafuta miradi ya uhakika kulisaidia Shirika la *TANESCO* kupata fedha za kutosha kutoka kwa wadaiwa wake sugu, nataka kukumbusha kwamba mwaka 2002 Serikali ilileta *management* ya *Net Group Solution.* Ilipoleta ile *Net Group Solution,* ninataka kusema kwamba wakati ule hakuna chochote kilichotokea, wananchi wengi walikataa kuja kwa *Net Group,* lakini walipokataa waliingizwa kwa nguvu, wananchi wakagandamizwa katika nchi yao wenyewe na kwa kutumia silaha wakaingizwa *Net Group*.

Mheshimiwa Spika, nimegusia *Net Group* kwa sababu Serikali kwa nini haikujifunza? Kwa sababu *Net Group* hakuna lolote ambalo lililetwa na *Net Group Solution* badala yake wale *Net Group Solution* walivuna tu. Tunaambiwa kwamba Mkurugenzi Mkuu alikuwa anapata shilingi milioni 25, Mkurugenzi wa Fedha shilingi milioni 23 na Mkurugenzi wa Utumishi shilingi milioni 22. Hiyo ndiyo ilikuwa mishahara na mpaka baada ya miaka minne walipoondoka hakuna lolote walilokuwa

wamelifanya. Serikali haikujifunza chochote mpaka sasa ni miaka 19 tunaendelea kuteseka kukaa gizani ambapo tungeweza wakati huu tukawa na miradi mbalimbali ya umeme ya kutumia vyanzo vyetu wenyewe na kutumia wataalam wetu tulionao na tukaweza kuwa na umeme wa uhakika.

Mheshimiwa Spika, kuna wakati Fulani, sikumbuki ni mwaka gani, lakini kuna Watanzania walitaka kuzalisha umeme wa upepo, lakini wakazuiliwa. Watanzania wanapotaka kufanya mradi wanazuiliwa. Lakini wageni, wao wanapata *favour* na hii siyo nzuri. Tunahitaji sasa kubadilika, tunahitaji kuwa na moyo wa uzalendo na tunahitaji kujua kwamba kama sisi hatutabadilika na kuipenda nchi yetu na kuhakikisha kwamba tunakuwa na miradi inayoeleweka, la sivyo, basi wale ambao wamefanya makosa, wanahitaji kuadhibiwa au kuondolewa. Hakuna haja ya kuwa na watu wale wale wanaendelea kufanya kazi wakati hatuoni mabadiliko na badala yake ni kukaa na kuendelea kuteseka gizani.

Mheshimiwa Spika, viwanda vingi sasa hivi vimefungwa. Tumeambiwa kwamba viwanda 50 vimefungwa kwa kukosa umeme na pia tumesikia kwamba *TRA* imesema huenda shilingi bilioni 840 za makusanyo zitakosekana kwa kukosekana kwa umeme. Ni wakati muafaka kwamba tukae na kujua kwamba tunahitaji kubadilika, sisi binafsi tubadilike na tuwe na moyo wa uzalendo wa kuipenda nchi yetu na kila mtu katika nafasi yake kuifanya kazi ile ambayo amekusudiwa kuifanya.

Mheshimiwa Spika, kwa hayo machache, mimi siungi mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba nianze kwa kushukuru sana kwa kupata fursa hii adhimu na mimi leo hii nichangie hotuba hii ya Wizara ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Spika, ili nisije nikasahau kule mwisho, naomba nianze kabisa kwa kusema kwamba mimi sitaunga mkono hoja ya kupitisha bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini. Naomba nitumie fursa hii kuwashauri na kuwashawishi Wabunge wenzangu katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tuliokaa hapa leo hii, tusikubali kupitisha bajeti hii kwa sababu ni bajeti ambayo inakwenda kupitishwa wakati nchi yetu ikiwa imetanda katika giza kuu, wakati nchi yetu ikiwa inatumia vibatari, wakati nchi yetu ikiwa inatumia majenereta ya Kichina na wakati tukiwa katika giza kuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi binafsi na ninaomba nitumie fursa hii pia kuwashawishi wenzangu tusikubali kupitisha bajeti hii kwa sababu tupo katika giza na hatuoni ubunifu wa aina yoyote ile, hatuoni *innovation* ya aina yoyote ile katika bajeti ya kuweza kututoa hapa katika giza ambapo tumo.

Mheshimiwa Spika, sababu za kuliingiza Taifa katika giza zinajulikana, waliotufikisha hapa wanajulikana, lakini hawachukuliwi hatua. Serikali imenyamaza na sisi Watanzania tumechoka kuendelea kuishi katika giza huku waliotufikisha hapa wanajulikana na hawachukuliwi hatua zozote zile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumeingia katika mikataba mingi sana mibovu na mikataba yote hii ina kitu kinaitwa *Tax Stability Clauses* ambazo kwa hali yoyote ile hizi *clauses* zinawekwa kwenye mikataba ili kulinda maslahi ya kibeberu ya makampuni ya nje yanayokuja kuwekeza katika nchi yetu. Ukiisoma mikataba kuanzia ya Madini ya Mgodi wa *Resolute* Nzega ambako mimi natokea, ya Bulyanhulu majirani zangu kule Kahama, ukisoma Mkataba wa *Pan African Energy*, ukisoma mikataba yote hauoni uhalali wa sisi kuingia katika mikataba hiyo. Unashindwa kuelewa hivi kweli hawa Watanzania waliosomeshwa kwa kodi za wananchi, waliwezaje kukubali kusaini mikataba kandamizi kama hii? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, inasikitisha na bado watu hawa wapo, wamo kwenye *system* ya Serikali wanaendelea kuliingiza Taifa katika giza, wanaendelea kuuza nchi yetu, wanaendelea kuuza migodi bila huruma yoyote ile.

Mimi leo hii nasema, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Nzega, na ninasema kwa niaba ya Watanzania wenzangu kwamba hatuwezi kunyamaza huku nchi yetu ikiuzwa, tukiwa katika giza, na hali ya kuwa wachache wanaofikiria kwa kutumbua matumbo yao zaidi, wakiendelea kujishibisha, wakiendelea kupewa kitu kidogo, kufaidi asilimia 10 huku wananchi wakiwa katika giza, uchumi ukiendelea kudodorora na sisi tukiendelea kuwa nao. Wengine tuko nao humu Bungeni na wengine wapo kwenye Serikali na hatuoni hatua zozote zile zikichukuliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama siyo kufikiri kwa kutumia matumbo, basi pengine wanafikiri kwa kutumia *spinal cord.*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge hayo ondoa tu, hebu semea habari za kutumia akili. Siyo hayo mengine. Naomba uendelee.

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA:** Mheshimiwa Spika, nasema kwamba wanafikiria kwa kutumia matumbo kwa maana ya kwamba wanapokwenda kusaini hii mikataba wanakuwa wanaangalia kwanza katika hii mikataba, “kuna nini kwa ajili yangu?” Katika hii mikataba *what is in it for me.”* Hawafikirii uzalendo! Hawamfikirii Mtanzania anayehangaika! Hawafikirii hata watoto na wajukuu zao kwa kuwa wao leo hii wamepata fursa ya kuwa katika Serikali, basi wanaitumia ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama wangekuwa wanafikiria kwa kutumia vichwa, basi wasingesaini mikataba hii. Kwa sababu nashindwa kuelewa inatokeaje mtu anaweza kusaini mkataba ambao utaruhusu ardhi ya Watanzania kuuzwa? Tena inauzwa kwa bei chee na yeye anajengewa nyumba *Mbezi Beach*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba niendelee katika mtiririko wangu kwanza kwa kum-*quote* mwana mikakati ambaye aliishi nchini China katika karne ya 19 na karne ya 20 na yeye alisema kwamba: “*Now the reason the enlightened prince and the wise general conquer the enemy whenever they move and their achievementsurpass those of ordinary men is foreknowledge”*

Mheshimiwa Spika, Sun Tzu alisema maneno haya kwamba ni muhimu katika mkakati wowote ule wa kivita au wa kimapinduzi kuwa na *knowledge* ya mapema zaidi kabla ya adui yako wakati ukiwa unakwenda kukabiliana naye.

Mheshimiwa Spika, maneno haya mantiki yake ni kwamba sasa hivi dunia inatawaliwa na *knowledge economy* inatawaliwa na ufahamu wa watu na ufahamu huu ukiupata mapema kabla ya mwenzako wakati mnakwenda kuandika mikataba, basi maana yake ni kwamba wewe utaweza kumdhibiti vizuri.

Mheshimiwa Spika, mimi nashindwa kuelewa kama kweli, wewe utaweza kumdhibiti vizuriinvestor bla kuwa na *foreknowledge.* Mimi nashindwa kuelewa kama kweli kumekuwa na intelijensia ya kutosha ya kuweza kufahamu mikakati ya kiuchumi ya makampuni ya kimataifa yanayokuja kuwekeza Tanzania, kuja kusaini mikataba na sisi wakati huo huo wanaposaini hiyo mikataba wanaweza kuwarubuni watu wetu pengine kwa sababu ya njaa zao au pengine wanawarubuni watu kwa sababu ya uelewa wao duni.

Mheshimiwa Spika, nadhani intelijensia isiishie tu kwenye kujua kwamba wananchi wa Nzega wanataka kuandamana kupinga mgodi na kuwazuia, intelijensia isiishie kwenye kuangalia tu kwamba Machinga wa Mwanza wanataka kuandamana, wanataka kwenda kupinga kuondolewa katika sehemu zao za biashara, intelijensia isiishie tu kuangalia kwamba wananchi wa Arusha wanataka kugoma kwa sababu ya uchaguzi ambao haukuwa huru na haki. Iende mbele, iangalie, kwa nini uchumi wetu unaanguka? Iende mbele kuangalia wenzetu wanafanyaje kwenye mikataba, iende mbele kuangalia Wazungu wanapokuja kuwekeza katika nchi yetu wana malengo gani yaliyojificha?

Mheshimiwa Spika, makampuni ya kimataifa kwa kutumia *tax heavens,* yamekuwa yakituibia rasilimali katika nchi yetu, yakikwepa kodi na mfano mzuri ni Taarifa ya Shirika la Wanaharakati la *Action Aid* ambayo imetolewa wiki iliyopita kule nchini Sweden, ambayo inasema kampuni ya *Pan African Energy*, ambayo inauza gesi asilia ya kule Songosongo, imeweza kukwepa kodi toka 2004 mpaka leo hii ipatayo dola za Kimarekani milioni 65. Dola milioni 65 kwa leo hii ni takribani bilioni 100. Ukiangalia kwa mapato ambayo tumepoteza kwenye Shirika moja tu la *Pan African Energy,* achilia mbali *Resolute* ambako tumepoteza zaidi ya kodi ipatayo bilioni 500. Ukiangalia tu haya mapato ambayo tumepoteza, tungeweza kuanzisha migodi yetu wenyewe, tungeweza kuipa *STAMICO* tukajenga uchumi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mapato haya ambayo tunayapoteza leo hii kwa mfano hizi dola za Kimarekani milioni 65, wao wenyewe Shirika la *Action Aid*, wanasema kwamba inakadiriwa watoto wa kike 175,000 wangeweza kusomeshwa Shule za Sekondari. Makampuni haya makubwa kwa kweli yanaiba sana rasilimali katika nchi hii.

Mheshimiwa Spika, mimi bila kupoteza muda sana, naomba niishauri Serikali, tusiogope kwenda kuvunja mikataba hii, tusiogope kwenda kuya-*Nationalise* makampuni ya migodi, tusiogope kwenda ku-*Nationalise* makampuni ya gesi na mafuta katika nchi yetu kwa sababu, wao Wazungu waliwahi ku-*Nationalise* huko nyuma. Mfano mzuri ni kule Uingereza, waliwahi kuanzisha kodi inayoitwa *Windfall Profits Tax,* waliwahi kuanzisha *Ring Fancing* kwenye miradi mbalimbali ya makampuni pale ambapo kampuni inapata faida kubwa ili kuweza ku-*harness opportunities* zinazopatikana kutokana na faida kubwa ambayo haikutegemewa na makampuni haya. Pia mwaka 1956, Jamal Abdiel Nasa, aliyekuwa Rais wa Misri, aliweza ku-*Nationalise* kampuni ya *Suez Canal Company*. Aliweza ku-*Natinalise* kampuni hiyo na alipambana na Wazungu na hatimaye aliwaletea maendeleo ndugu zake wa kule Misri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi ninaamini tunaweza. Tusiogope, tujifunge mkanda, twende tuka-*renegotiate* hii mikataba na kama wakikataa basi tuifutilie mbali mikataba hiyo, tuzinunue shea zao kwa lazima, tuweze kurudisha rasilimali hii kwa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la mwisho kabla muda haujaniishia, nalisema hili kwa uchungu sana. Waheshimiwa Wabunge wenzangu, naomba tulizingatie hili, ardhi hii yote yenye rasilimali ya madini, gesi na mafuta katika nchi yetu, kwa asilimia kubwa imenunuliwa. Ukifanya utafiti unaweza ukalia, kuanzia Ilagala, Kigosi kwenda mpaka kule Nzega, Isungangwanda, Itobo, Lusu na Matinje. Kote ni leseni ambazo wamepewa Wazungu, ardhi imeuzwa na ardhi yote hii ni tajiri kwa madini! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi sitaunga mkono hoja hii mpaka pale Serikali itakapoamua kutamka rasmi katika Bunge hili kwamba, mwisho wa kuwekeza katika sekta ya madini umefika na kwamba hatutaki hawa Wazungu waendelee kununua ardhi yetu, leseni zote zinafutwa. Nitaunga mkono hoja hii endapo tu Serikali itatamka wazi kwamba inafutilia mbali leseni zote za utafiti katika madini na badala yake majukumu ya utafiti yarudishwe kwenye Serikali ili Serikali yenyewe iweze kufanya utafiti na kuamua ni nani mbia mzuri ambaye tunaweza tukashirikiana naye katika uwekezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitaunga mkono hoja hii endapo nitaambiwa ni vipi Serikali imejipanga kwenda kuzirudisha bilioni takribani 100 zilizoibiwa kwa njia ya *tax heavens* na Kampuni ya *Pan African Energy*. Nitaunga mkono hoja hii endapo tu nitaambiwa ni lini Watanzania watapata umeme wa uhakika, ni lini mawazo mazuri yaliyotolewa na Wabunge hapa, yatafanyiwa kazi ili kuweza kuiwashia mwanga nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii na naomba nimalize kwa kuishukuru Serikali kwa kupeleka umeme kule Nzega katika Vijiji na Kata za Utwigu mpaka kule Ndala lakini nina mashaka kama watu hawa wanaweza kupata huu umeme kwa sababu umeme wenyewe hautoshi. Nashindwa kuelewa inakuwaje tunapelekewa umeme wakati umeme wenyewe hautoshi na hatuna uhakika kama utawaka! Japokuwa tunawashukuru kwa kutuletea milingoti na kufunga mtandao wa umeme.

Mheshimiwa Spika, siiungi mkono hoja hii. Ahsante sana kwa kunipa fursa. *(Makofi)*

**T A A R I F A**

**MHE. DKT. CHARLES J. TIZEBA:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Taarifa, wapi?

**MHE. DKT. CHARLES J. TIZEBA:** Mheshimiwa Spika, naomba kumpa tu taarifa Msemaji aliyekaa, kwamba kampuni ya *Pan African Energy* hawakutuibia hizi fedha kwa msamaha wa kodi isipokuwa kwa udanganyifu wa moja kwa moja katika gharama za uzalishaji. *(Makofi)*

**SPIKA:** Naona ndio hivyohivyo anavyosema.

**KUHUSU UTARATIBU**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, UWEKEZAJI NA UWEZESHAJI:** Mheshimiwa Spika, Kuhusu Utaratibu!

**SPIKA:** Kuhusu Utaratibu, upi?

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA:** Mheshimiwa Spika, hata huo aliousema Mheshimiwa Mbunge, ni wizi tu! *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa, sijakuruhusu, yaani hapa hasimami mtu mpaka nimemwita, sasa wewe vipi? Mimi nimesema pengine inalingana hivyohivyo, si basi! *(Kicheko)*

**KUHUSU UTARATIBU**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, UWEKEZAJI NA UWEZESHAJI:** Mheshimiwa Spika, Kuhusu Utaratibu.

**SPIKA:** Ndio!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, UWEKEZAJI NA UWEZESHAJI:** Mheshimiwa Spika, Kanuni ya 68 na Kanuni ya 64(g).

Mheshimiwa Spika…

**SPIKA:** Naomba usome hiyo (g).

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, UWEKEZAJI NA UWEZESHAJI:** Mheshimiwa Spika, Kanuni ya 68 inasema:-

*“Mbunge anaweza kusimama wakati wowote na kusema maneno Kuhusu Utaratibu”* na ndicho nilichosema.

Mheshimiwa Spika, halafu Kanuni ya 64(g) inasema:-

*“Hatatumia lugha ya kuudhi au inayodhalilisha watu wengine.”*

Mheshimiwa Spika, mimi nakubaliana kabisa na Bunge lako Tukufu kwamba humu ndani kazi ya Bunge ni kuishauri Serikali na kuilekeza. Hilo tunakubali na ni jambo zuri na kwa hivyo tuendelee, Bunge letu liishauri Serikali na lituelekeze lakini pale ambapo panastahili, naomba basi kuna maneno mengine yanahitaji kwa kweli kuwa na ushahidi. Kwa mfano, Mheshimiwa Mbunge, Mheshimiwa Dokta Kigwangala, amesema kuna wengine wamejengewa nyumba *Mbezi Beach.* Tuko wengi humu ndani, si sahihi kwa umma wa Watanzania kufikiria kwamba wote walio kwenye Serikali wamejengewa nyumba *Mbezi Beach!*

Mheshimiwa Spika, naomba basi kama ana ushahidi anaweza akakupa wewe kwa namna yoyote anayoijua, lakini naomba Waheshimiwa Wabunge, wanaposemea jambo ambalo linaweza kumdhalilisha na kuifanya Serikali yako isionekane kama ni kitu, kumbe ni mtu mmoja au wawili basi ushahidi utolewe. Naomba tuendelee kuishauri Serikali na kuilekeza, kwa sababu nchi hii ni yetu sisi wote na pale tunapojenga, kama tunaongelea makampuni ya nje ni kwa maslahi ya nchi yetu…

**SPIKA:** Mheshimiwa, useme utaratibu kwa kifupi, maana tena tukipata hotuba, muda hautoshi.

Waheshimiwa Wabunge, ni kweli kwamba unaposema hapa, nimeshawaeleza mara zote, yaani huniambii mimi peke yangu, unaiambia Dunia nzima! Kwa hiyo, mtu ukiwa na kaushahidi kako jiandae vizuri. Mbunge mzuri ni yule anayejiandaa vizuri, akiwa na hicho kitu anacho kabisa kwamba mimi nina ushahidi huu na huu na huu na sisi hatutaupuuza ushahidi huo lakini tusiseme tu kwa sababu ya hamasa ya kusema kumbe kitu chenyewe huna! Wewe mwenyewe unajivunjia heshima lakini kama una ushahidi, wewe leta ndio kazi yenyewe, ndio kazi yenyewe hapa. Kwa hiyo, tunaendelea, Mheshimiwa Kaihula!

**MHE. NAOMI A. M. KAIHULA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia kwenye *speech* hii ya Nishati na Madini, ahsante.

Mheshimiwa Spika, kabla ya yote, napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunirudishia afya yangu kwa sababu hapo juzi niliteteteka. Namshukuru na Utukufu namrudishia yeye.

Mheshimiwa Spika, pia napenda kuwapongeza ndugu zetu wa CCM, kwa kukubali maandamano ni silaha mojawapo ya kufikisha ujumbe kwa wananchi na

wenyewe walifanya hivyo kwa kufanya maandamano Mbeya. Kwa hiyo, naomba *spirit* hii iendelee. Napenda kuwaomba kwamba, kama ambavyo wameweza kuona kuna vitu vingine vya Upinzani vinaweza vikawa vizuri, pia waone vizuri kwamba hii bajeti ya Nishati na Madini kwa kweli tusiipitishe kwa umoja wetu kwa sababu ina matatizo makubwa sana. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, yameshazungumzwa na watu wengi na mimi napenda nichangie katika masuala matatu ya msingi. La kwanza kabisa ambalo nafikiri isingekuwa vizuri kwa hii bajeti kupitishwa ni lile linalohusu umeme. Umeme imekuwa ni tatizo, mimi nashindwa kuelewa, wananchi wanapotupa mamlaka tunapaswa pia tukubali kuwajibika. Nashangaa ni kwa nini mpaka sasa, wakati huu, bado wahusika wote wa umeme hawajawajibika inavyopaswa kuwa! Kwa sababu, kusema ukweli kwa akili tu ya kawaida Mungu aliyotupa ni kwamba umeme umeua uchumi wa nchi na kwa bahati mbaya sana umemalizia kabisa kwa watu wanyonge kwa sababu ukianza kwenye nyumba za kawaida, matumizi ya kawaida ya nyumbani, ukija matumizi ya vyuoni, matumizi ya hospitalini, matumizi ya viwanda, yaani hakuna mahali popote penye nafuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi sioni kwa sababu gani hatuwezi kuwaonea huruma, ni maneno yaani kila wakati tunapewa ahadi, hazitekelezwi! Mara kina cha maji kimekuwa hivi! Mara kina kikapanda, kikashuka! Mara tumeleta gesi! Mara tumeleta mitambo! Mambo yote yanaisha kienyeji tu bila kuelewa kwamba sasa mlipoleta maji yakashindwa, mkaleta umeme ukashindwa, mlifanya nini? Hakuna kitu kama hicho! Sisi Waheshimiwa Wabunge, sisi wawakilishi wa Watanzania, tunaonekanaje katika ulimwengu huu kwamba sisi akili zetu ni finyu kiasi gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hii miaka *almost* 20 tumeshindwa kuwa na mipango endelevu, *sustainable!* Yaani mtu ukipata kitu hiki, si unapanga na cha baadaye! Kwa nini tumeshindwa kupanga mipango ambayo kama maji hayapo tutakuwa na upepo, kama upepo haupo tutakuwa na jua! Tena bahati nzuri, Mwenyezi Mungu alivyotupendelea nchi yetu ya Tanzania, ametupa jua bwerere, hatuhitaji upepo, yaani useme nini, lakini tunashindwa na bado tunataka tubaki kwenye madaraka na bado tunataka tuendelee kupitisha hii bajeti, wananchi wazidi kutuona kwamba sisi ni watu ambao tuna matatizo ya kiakili! Nawaomba ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge, kwa heshima ya sisi wote kwa kadri tulivyo, hii bajeti tusiipitishe kwa sababu, tunawapenda wananchi wetu. Tusipitishe sio kwa sababu tunawachukia, ila kwa sababu tunawapenda, tunataka wakafanye kazi vizuri, waache kutudanganyadanganya, ni aibu kabisa! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sijui watudhihirishie vipi kwamba tutapitisha. Kwanza, walianza na *RICHMOND, RICHMOND* hiyo ikawa *RICHMOND!* Ikabeba mabilioni yetu ikapeleka kwa watu binafsi, mpaka leo hatujajua ni nani aliyekuwa anapata yale mamilioni 152 na ushee, hatujapata hilo jawabu! Mara *RICHMOND* ikaisha hivihivi kienyeji na tatizo la umeme wala halikutatuka, ikaja tena *DOWANS! DOWANS* nayo hivihivi, watu tukasikitika *DOWANS* imekuwaje jamani? Kwa sababu, *DOWANS* hawezi akazaliwa na haramu *RICHMOND,* halafu akaendelea kuwepo, sisi tukakubali, tumekaa tu! Kwa kweli sisi tuna akili timamu jamani! Si wananchi watatuona ni watu wa ajabu!

Kwa heshima yetu jamani, naomba siku ya leo iwe mwisho kuvunja heshima yetu, tusipitishe bajeti hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mara wakaja *SYMBION!* Sasa hapa ndio nikawa hoi kabisaa! Waheshimiwa Wabunge, Waheshimiwa wenzetu tuliowapa heshima ya kutufanyia jambo hili, kwa kweli tunaomba sana mtufunike, yaani mturudishie heshima. Kwa sababu, *SYMBION* ilivyoingia kwa *DOWANS* sisi hatuelewi! Bunge ndilo ambalo linapaswa kuamua hayo mambo *especially* yanapokuwa na utata kama haya. Kwa kweli, hili ndio kubwa kwamba sitakubali kupitisha bajeti hii. Nawaomba na ndugu zetu jamani, siku ya leo itikadi tuweke kando, tufanye kama tulivyofanya kwenye yale maandamano, tukubaliane tusipitishe. Samahani sana ndugu zangu, naomba mnisamehe, hilo moja. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, la pili, ni suala la madini. Suala la madini mimi linanitia huzuni sana. Linanitia huzuni sana kwa sababu kama tunavyojua, nchi yetu yote hii Mungu alivyotubariki, akatupa madini karibu dunia nzima! Yaani tukisema Duniani hii Tanzania kwa lugha rahisi ya wananchi wanayoielewa ni madini. Tatizo sio hilo, tatizo ni sisi wenyewe jinsi ambavyo tunatekeleza Sera zetu na jinsi ambavyo tunajipanga kuwatumikia watu wetu. Sisi tuko hapa kutunga Sheria ambazo zinawalinda wananchi, sisi ndio sauti ya wananchi, jicho la wananchi, sisi ndio kila kitu cha wananchi lakini kinyume chake jamani, tumewafanyia vibaya sana Watanzania kwa mambo tunayofanya.

Mheshimiwa Spika, wewe fikiria mtu anakutwa kwenye ardhi yake kuna madini, badala ya wewe kuwa upande wake unapofanya mikataba, umsaidie kuona kwa sababu yeye hawezi kuona vizuri, wewe ndio unamkandamiza! Hii haiingii akilini, mimi sielewi! Inakuwaje kila wakati ukisema huu mkataba tuutengue, ooh, watatufanya hivi! Hivi, unapoingia kwenye mkataba si ni lazima na wewe ujiangalie! Kwa mfano wakisema, nichukue mfano wa maji; anasema mimi nitaleta maji, sawa tumekubaliana, lakini na wewe ni lazima useme na ukishindwa kuleta maji tutafanyaje? Mbona vitu kama hivyo havipo? Au mimi nitachimba madini kiasi hiki, sasa na wewe uwaambie kwamba lakini je ukipitiliza au je ukiua watu wetu! Mbona hivyo vitu hamuweki? Vitu kama hivi ndio vinapelekea wananchi wetu kufikiri kwamba wale watu wanaokwenda kufanya mikataba, wanafanya mikataba ya *40%*, yaani wanajiangalia wao badala ya kuangalia umma, badala ya kuangalia nchi yao na ndio tumefikia hapa mpaka tumekwama! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ndugu zangu wananchi, hivi hatujifunzi sisi kwenye historia? Kuna wakati nilisimama nikasema, tena humu bahati nzuri wamo wasomi tu wengi na historia wanaijua. Hivi mnafikiri migogoro ya Zimbabwe, migogoro ya *South Africa*, migogoro ya wapi, ilikujaje? Ilikuja kwenye mikataba mibovu kama hii. Sasa kwa mfano, hii nchi mmeuza, ardhi mnauza tu, mnatoa tu, sasa hao watu wakikataa kutoka, tutafanya nini?

Mheshimiwa Spika, ngoja niwaambie, suala la madini ni tete sio rahisi kama tunavyofikiria na sasa hivi kuna mtindo umeingia ambao ndio Serikali inapaswa itutetee, lakini inaingia mikataba mingine hatuijui! Juzi, tulipokuwa kwenye Kampeni Sangara, bahati nzuri Kiongozi wetu mahiri, Mheshimiwa Freeman Aikaeli Mbowe, katika kutu-

*train, on job training* kwa sisi Wabunge wa Viti Maalum, alisema msizungumze mambo ambayo hamuyajui! Ni lazima mzunguke nchi hii, muwaone wananchi halisi na wa kila mahali kwa sababu ninyi ni wa Taifa, hiyo kazi ni nzuri sana nawaambieni, tumekwenda tukakuta kule Tunduru wanachimba *Uranium,* khaa! Kumbe na *Uranium* imo humu Tanzania! Kitu hicho hakijulikani. Tulivyotoka huko tukajiuliza hivi kuna Sera ya *Uranium?* Hakuna!

Mheshimiwa Spika, sasa vitu kama hivi, Sera yenyewe haipo, Wabunge wengi hawajui kama *Uranium* nayo imeingia katika orodha ya madini ya kutuharibia, sasa vitu kama hivi vinaleta wasiwasi! Ni kwa nini watu wanazunguka? Kuna vitu vingine sitaki kuvisema hapa kwenye Bunge, lakini siku nyingine nitakuja kusema, Mataifa mengine makubwa yanaingia kwa ujanja hapa. Nilishangaa kusikia kwamba Marekani ndio ambao wanachimba *Uranium* kule*!* Nilishangaa sana. Kwa sababu Marekani anapaswa kujua sheria na taratibu zote, anapaswa ajue pia Sera, lakini wananchi hatujui! Inakuwaje Marekani anaingia kule mikataba? Sasa mataifa makubwa kama haya yakija yakatuweka poni sisi, yakatugeuka, yakatupiga, tutafanya nini jamani? Kwa sababu watu wachache wamekubaliana nao huko, watu wengi hata nchi hatujui, Wabunge wenyewe hawajui, kwa kweli suala hili lilisikitisha, kwa sababu *uranium* kama mnavyojua ina hatari sana huko mbele inakokwenda. Kwa kweli suala hili kama lipo tunaomba lisitishwe, tunaomba lisitishwe kabisa, *uranium* siyo kitu cha kushughulikia kwa kinjanja. Tunaona hata Japan nchi ambazo zimeendelea, wanashindwa hata kukabiliana nayo, je, sisi Tanzania si tutakwisha nchi nzima? Kwa hiyo hili suala naomba sana kwamba lishughulikiwe linavyopaswa na lisitishwe kama kweli lipo na naomba kwa heshima ya Wizara inayohusika, suala hili tulio wengi limetushtua.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuzungumzia hilo, nilikuwa nafikri kwenye madini pengine wale wananchi wawe wanapewa hisa. Ushauri wangu wawe wanapewa hisa kwenye ardhi yao, kwa sababu sasa hivi inavyoelekea Watanzania wote wataondoka, watakuwa hawana ardhi, wawe wanapewa hisa katika madini yoyote yanayochimbwa.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabla kengele haijanigongea, kuna jambo la kusikitisha la kwamba inaelekea wafanyabiashara wametuweka sisi Waheshimiwa mfukoni. Inakuwaje sisi tukakubali kupandisha bei ya mafuta ya taa *on the expense* ya *diesel*, sasa unaona kinachofanyika, wao wanafanya wanavyopenda. *Diesel* imeshindwa kushuka bei lakini mafuta ya taa yamekwishapanda, hiki kitu kinakuwaje? Serikali inashindwa kuwashika wafanyabiashara hata wawili ikaonyesha mfano halafu wengine wakaacha kufanya hivyo? Serikali gani inayoshindwa kusimamia mambo ambayo imepewa, tumewapa mamlaka Serikali mfanye kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kweli kutokana na haya mambo matatu muhimu hata mimi sikubali kama tunapaswa kuipitisha hii bajeti ya leo. Tusiipitishe ndugu zangu, nawaomba sana ndugu zangu wa CCM, tafadhali hili suala tuwe pamoja, sisi wote ni kwa ajili ya wananchi, tusipitishe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**MHE. SILVESTRY F. KOKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii niweze na mimi kutoa mchango wangu kwa niaba ya Wananchi wa Jimbo la Kibaha Mjini.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wamezungumza mengi kuhusu suala umeme na mimi kwa kifupi nataka kuishauri Serikali kwamba tayari ilishafanya makosa kwa kuhimiza na kuchochea uwekezaji huku ikiwa haijajipanga vyema katika kuhakikisha umeme wa kutosha upo kwa ajili ya kuendeleza uwekezaji huu. Sasa kwa ujumla wake, naiomba sasa Serikali, suala hili kwa ujumla wake i-*pull up resources,* rasilimali zote za Serikali izilete kwa pamoja kuhakikisha umeme unapatikana na lifanyike haraka bila kuiachia Wizara ya Nishati na Madini. Hili si suala la Ngeleja, tutampiga ngumi, makofi, lakini ukweli utabakia palepale kwamba Serikali haikuwekeza vya kutosha katika nishati huku ikijua kabisa uwekezaji wa viwanda, makazi na kadhalika unaendelea kupanuka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii kusema kwamba bado tunazo nafasi nyingi za kutosha. Pamoja na mipango mizuri niliyoiona ya kuhakikisha umeme unapatikana wa kutosha, lakini sikuona uwekezaji muhimu katika *geothermal*, kwa maana ya uwekezaji katika kuzalisha umeme kwa kutumia gesi ya *volcano* iliyoko chini ya ardhi. Tunalo Bonde la Ufa, tunayo milima ambayo ina *volcano* iliyolala na *active* na hakika *investment* ni kubwa lakini umeme huu ni rahisi baada ya kufanya *investment*. Naiomba Wizara husika na Serikali itupie macho, tutumie rasilimali hizi tulizonazo tuhakikishe tunaendelea kupata umeme wa kutosha.

Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii kuzungumzia Jimbo langu, ninayo maeneo katika Jimbo langu la Kibaha Mjini, ambayo sasa ni Mji, katika mitaa mbalimbali hawajaweza kupata umeme. Mtaa wa Maili 35 kwa takribani miaka saba wamehangaika kupata umeme hadi leo hawajapata umeme. Kuna mitaa ya Mwalakani, Chang’ombe, Kitende, wameomba umeme kwa zaidi ya miaka saba hawajaweza kupata. Niishukuru Serikali katika bajeti hii nimeona sasa maeneo ya Mbwawa, Mkoleni, Miso Chini na Juu wanategemea kupata umeme kwa kuwa walikuwa wanalinda na kutizama umeme unaokwenda kuzalisha maji Ruvu Chini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niombe Wizara hii itupie macho na kuhakikisha wananchi walioko Mikongeni, Sagale, Viziwaziwa hawabakii kutizama mradi wa umeme unaoelekea katika shamba lililokuwa la mkonge linaloitwa Alavi, lakini nao wanahusishwa na kupatiwa umeme ili waweze kufanya shughuli zao za maendeleo. Mji wa Kibaha Mjini unapanuka, maeneo ya Pangani, Kidimu, Vikawe na wenyewe wapatiwe umeme ili kukidhi haja ya kukua kwa mji wa Kibaha. Ifahamike wazi kwamba sasa Kibaha ni Mji na siku zote nimekuwa nikisema ni *next destination* ya Dar es Salaam, kwa hiyo ipewe kipaumbele kuhakikisha nguvu za umeme zinapatikana za kutosha ili uwekezaji wa viwanda na makazi uweze kuwa wa kuridhisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii kuzungumzia kwa kifupi kuhusu madini, gesi pamoja na mafuta, ni jambo ambalo limekuwa linatupa wasiwasi mkubwa na limekuwa ni kero kwa wananchi. Ukiangalia upande wa madini, ni wazi kwamba

wawekezaji tunawakaribisha lakini utaratibu mzima wa kuhakikisha wananchi wanapewa kipaumbele na wenyewe cha kufaidi madini yaliyoko katika ardhi yao umekuwa ni hafifu. Napenda kujiuliza na tuiulize Serikali, kuna tatizo gani linalofanya wachimbaji wadogowadogo na wananchi hawa wanaendelea kugombana na wawekezaji? Serikali kupitia Wizara hii wameshafanya *geological survey*, wanajua maeneo mbalimbali yaliyo na madini mbalimbali, kwa nini kusiwe na utaratibu wa kuhakikisha wananchi hawa, wachimbaji wadogowadogo kamwe wasiingiliane na hawa wachimbaji wakubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wachimbaji hawa wadogo hawana hata uwezo wa kwenda nusu kilomita moja au kilomita moja chini ya ardhi kutafuta madini lakini hawa wakubwa wanakwenda mpaka kilomita tatu, tano, kumi chini ya ardhi, sasa kwa nini kusifanyike utaratibu wa kuhakikisha mwananchi huyu ambaye haya maeneo ni yao ya urithi na wenyewe wanafaidika, wanapewa maeneo tofauti, hawaingiliani na wawekezaji wakubwa ili kuondoa maafa na matatizo makubwa yanayojitokeza bila sababu za msingi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumejionea makampuni makubwa haya yanayowekeza sehemu mbalimbali hususan katika gesi na katika mafuta, ni wazi kwamba kumekuwa na kero nyingi sana ambazo zinawafanya wananchi wanaichukia Serikali yao kwa ajili ya mambo madogomadogo. Makampuni haya yanayokuja kufanya utafiti katika mafuta, wanakuja wakiwa na wafanyakazi pamoja ya makampuni yao wenyewe ya kigeni. Nitatoa mfano, makampuni yanayofanya utafiti wa mafuta yanakuja tayari yana wafanyakazi, wengine wanatoka Kongo, Ghana na wanakuja kufanya kazi ambazo tayari kuna Watanzania wanaweza wakazifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo hili linawafanya vijana wa Tanzania wasiokuwa na kazi kama wale wa kwangu pale Kibaha Mjini, Maili Moja, kujaa chuki na kuona sasa rasilimali hizi haziwafaidishi Watanzania. Wakati Sheria ipo wazi inayosema kwamba kazi zote zinazoweza kufanywa na Watanzania katika uwekezaji lazima ziende kwa Watanzania, kwa nini Serikali inakigugumizi katika jambo hili? Naishauri Serikali sasa itupie macho, iwe *active*, ihakikishe shughuli zote zinazoweza kufanywa na Watanzania, Watanzania wanapata fursa hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, juzijuzi nimekutana na vijana wanajiita Oiloti, sijui Oga. Wako hapa wanatembea kwa miguu wanasema wana uwezo wa kwenda kufanya kazi lakini hawapewi kazi, wanaujuzi katika mafuta lakini hawapewi kazi nafikiri hata Waziri husika walimuona na barua zao.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo kumekuwa na tabia ya makampuni haya ya kigeni kuyapa makampuni ya kigeni kufanya kazi ambazo zinaweza zikafanywa na makampuni ya Kitanzania. Mfano mzuri mwezi ujao kampuni ya *British* Gas inategemea kufanya kazi kubwa ya *exploration* ya gesi kule Mtwara lakini kazi ya kuwalisha wafanyakazi, kazi ya kusafisha nyumba za kukaa wafanyakazi na kuwa *gardener*, imepewa kampuni ya Kifaransa. Sasa katika utaratibu huu ni wapi Watanzania

wanafaidika na rasilimali hizi? Katika utaratibu huu ni wapi faida inayotokana na shughuli hizi inabaki Tanzania na kuijenga Tanzania? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, uzalishaji wa gesi, pesa na faida iende nje, hata kusafisha vyumba vya kulala, hata kupika ugali, mchele nao tuwatumie wageni? Naiomba Serikali itizame suala hili na ukweli ni kwamba sheria iko wazi, kwa nini Serikali inapata kigugumizi kusimamia Sheria hii? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile katika ajira, tumesomesha Watanzania lakini sasa hawapati nafasi hizo. Ukienda kuangalia kule *Immigration* utakuta *expatriate*, unaambiwa huyu ni mtaalamu mkubwa wa mitambo ambapo Tanzania hakuna lakini ukienda kwenye *actual sense,* kwenye *field* utamkuta huyu ndio anayesimamia kusafisha ofisi. Ukweli uko wapi na Serikali yetu tunayo? Kwa hiyo, hayo ni mambo ambayo kimsingi yanawachukiza Watanzania, yanawafanya Watanzania wanaiona Serikali yao haiwaangalii, chuki bila sababu wakati Serikali ina mipango mizuri na imeweka Sheria, hii Sheria isimamiwe ili jambo hili lisiendelee kuwadhalilisha na Watanzania waweze kushiriki katika rasilimali hizi tulizopewa. Kwa sababu *issue* kubwa hapa *is how we are sharing the national cake*, ndiyo *issue* kubwa, lazima Watanzania washirikishwe katika ku-*share national cake*. Yaani keki iliyoko ya Watanzania ikiwa ni pamoja na rasilimali za madini, Watanzania wahusishwe, washirikishwe na wenyewe wafaidi, tunakaribisha uwekezaji lakini tunataka uwekezaji huu uwashirikishe Watanzania. Tunayo mashirika kama *TPDC* na mengine, kwa nini yasipewe uwezo yakaelimisha Watanzania, yakasomesha Watanzania wakawa na ujuzi wa kutosha haya makampuni yanapokuja ya kuchimba gesi, madini wakaambiwa jamani sisi tunao Watanzania hawa wapewe kazi na Sheria ipo wazi. Sasa hili suala la kusema hatuna *capacity*, hatuna *capacity* litakwenda mpaka lini? Naiomba Serikali yetu itoe kipaumbele katika suala hili kuhakikisha kwamba Watanzania wanafaidi rasilimali hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, bado kuna tatizo la mawasiliano kati ya Serikali na wananchi, wananchi wanalalamikia mambo mengi sana, lakini hawapati majibu. Kwa mfano, kabla hata mimi sijawaza kuja Bungeni, nimekuwa nikisikia malalamiko kuhusu makontena yanayobeba dhahabu, lakini Serikali haijawapa wananchi majibu. Inawezakana huu utaratibu ni mzuri na pengine Serikali inafaidi vizuri na pengine hata nchi nyingine zinafanya hivyo kwa sababu ambazo ni za kimsingi lakini wakati hakuna mawasiliano kati ya Serikali na wananchi, kuwaelimisha kwamba ni kwa nini mwananchi siku zote anazidi kuona kwamba huu ni wizi, kwa hiyo siku zote ataendelea kuichukia Serikali yake bila sababu yoyote, kwa nini wananchi hawaelezwi ukweli katika mambo ambayo wana wasiwasi nayo? Hawa walioko hapa ndiyo Wabunge wanaowawakilisha, wanapozungumza jambo hapa maana yake wamezungumza kwa niaba ya wananchi wao. Kwa hiyo, hata navyoongea hapa siyo mimi ni wananchi wa Jimbo la Kibaha Mjini wanaongea, kwa hiyo, tunaomba Serikali iwe na mawasiliano mazuri, iwaeleze wananchi vizuri mambo yanayoendelea na yale ya kimsingi wananchi wajue ili hata pale ambapo ungejenga chuki ambayo si ya sababu isiwepo kwa manufaa ya Serikali yetu na kwa manufaa ya Taifa letu zuri la Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niseme kwamba pamoja na matatizo tuliyo nayo, lakini bado katika uwekezaji huu kuna makampuni ambayo sasa yameanza kuonyesha mfano mzuri, maana Waswahili wanasema mnyonge mnyongeni lakini haki yake mpeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nizungumze kidogo kuhusu baadhi ya makampuni ya madini na hususan *Barrick African Gold* na *Shamte* ambayo ina migodi ya Geita. Haya ni mambo ambayo lazima tuwaeleze wananchi na kiukweli tukiangalia uchumi na faida za haya madini kwa hawa Watanzania ni nyingi, si lazima tu faida ya yale madini yanayochimbwa kama chuma, lakini kuna faidi nyingi zinazotokana na shughuli ile. Kwa mfano, huduma zinazotokana na zile kazi, kama kweli zikipewa Watanzania kama Sheria inavyosema, tunao uwezo mkubwa wa kufaidi madini haya, si kwa kufaidi tu ule uchimbaji wa madini yenyewe.

Mheshimiwa Spika, naomba ninukuu kwa ruhusa yako, kwa mfano mwaka 2009, kampuni ya *African Barrick Gold* ilitumia jumla ya dola 340 milioni, ambayo ni sawasawa na bilioni 440 kwa manunuzi ya vitu mbalimbali na katika manunuzi hayo, asilimia 20 zililipwa kwa makampuni ya Kitanzania, ambapo ni takribani dola milioni 70 au bilioni 110 lakini asilimia 37 zililipwa kwa makampuni ya nje yaliyosajiliwa Tanzania, makampuni ambayo faida yake haiwekwi hapa Tanzania wana *invest* nje, ambayo ilikuwa ni sawasawa na dola milioni 124 ambayo ni sawasawa na bilioni 190 kwa hela ya Kitanzania. Kwa hiyo, jumla ya asilimia 57 ya manunuzi yote yaliyofanywa na *African Barrick Gold* yaliweza kubakizwa kwenye makampuni ya Kitanzania na yaliyosajiliwa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa ukitizama kuna faida ambazo zinapatikana lakini tuna jukumu la kuwaelimisha wananchi wajue na hawa wamekwenda zaidi hata wamefika katika suala la *social responsibility* na hata wameweka kitengo kwa ajili ya *community development*, wamewasaidia wananchi wanalima mboga, wanazalisha mazao mabalimbali kwa ajili ya kuhakikisha yale maeneo yanayowazunguka na wenyewe wanafaidi katika hili.

Mheshimiwa Spika, sasa huu ni mwanzo mzuri lakini tunachosema…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa…

**MHE. SILVESTRY F. KOKA:** Hatutaki kisingizio cha kusema ni kampuni za kigeni zilizosajiliwa Tanzania.

**SPIKA:** Nimekusimamisha saa imepita.

**MHE. SILVESTRY F. KOKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naunga mkono endapo haya tunayozungumza yatafanyiwa kazi na Serikali. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya tunaendelea, tunajaribu kupata muda ili wengi wapate kuongelea suala hili, Mheshimiwa Lolesia Bukwimba.

**MHE. LOLESIA J.M. BUKWIMBA:** Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kukushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia Wizara hii ya Nishati na Madini ambayo ni Wizara muhimu sana hasa katika Jimbo la Busanda.

**SPIKA:** Mheshimiwa Koka, kwa mujibu wa Kanuni ya 61, una chochote cha ku-*declare* kuhusu Makampuni?

**MHE. SILVESTRY F. KOKA:** Mheshimiwa Spika, ndiyo! Nafanya biashara na baadhi ya makampuni haya ya madini, ya wauzaji wa madini.

**SPIKA:** Kwa hiyo, kwa mujibu wa Kanuni zetu, kabla hujamwaga sera zako lazima u-*declare interest* zako katika maeneo haya. Kwa hiyo, kwa mujibu wa Kanuni ya 61, itabidi suala hilo tuliangalie. Mheshimiwa Lolesia Bukwimba!

**MHE. LOLESIA J.M. BUKWIMBA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia hotuba hii ya Wizara ya Nishati na Madini. Katika Jimbo la Busanda, mara nyingi huwa nasema kwamba ni Jimbo ambalo tumebarikiwa sana na Mwenyezi Mungu kuwa na madini na madini ni chanzo cha uchumi katika eneo husika. Kwa hiyo, katika sekta hii ya madini, Wizara ya Nishati na Madini kweli ina kazi kubwa kuhakikisha kwamba wananchi wa Jimbo la Busanda wanapata haki yako ya msingi.

Mheshimiwa Spika, katika maeneo ya Nyarugusu, ni kweli kabisa wananchi hawa walipewa maeneo lakini maeneo haya yalikuwa ni ndani ya mji wa Nyarugusu, ambapo hawawezi kabisa kuchimba, leseni zenyewe ni ndani ya makazi ya watu. Kwa hiyo, nichukue nafasi hii kuomba Wizara ya Nishati na Madini iangalie uwekezekano wa kuwapa maeneo mapya wananchi hawa wa Nyarugusu na imekuwa ni malalamiko ya muda mrefu sana, kila naposimama nazungumzia suala hili. Kwa hiyo, niseme kwamba katika bajeti hii Mheshimiwa Waziri ahakikishe kabisa anapotoa majumuisho yake aelezee wananchi wa Nyarugusu kwamba ni maeneo gani atakuwa amewatengea kwa ajili ya wachimbaji wadogowadogo. Maana imekuwa ni kero ya muda mrefu, hata Mheshimiwa Rais alipokuja Nyarugusu mwaka jana alisema atatenga maeneo kwa ajili ya wachimbaji wadogowadogo hata siku ile ambapo alitembelea Wizara ya Nishati na Madini, Mheshimiwa Rais alimuuliza Mheshimiwa Waziri kama tayari amekwishakutenga maeneo haya kwa ajili ya wachimbaji wadogo lakini mpaka sasa hakuna chochote kinachoendelea.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ni kweli kabisa wananchi hawa wana shida sana, wanahitaji kupata maeneo ya uchimbaji na maeneo haya ndiyo rasilimali katika eneo lile ambapo wananchi wanatakiwa kufaidika kutokana na kuwepo katika eneo hilo. Wengi wamezaliwa hapohapo, wana watoto wao, wajukuu zao lakini wanategemea uchimbaji wa madini, hawajui kazi nyingine yoyote ile. Kwa hiyo, naiomba Serikali kwa kweli

iangalie changamoto hii kwa umakini mkubwa ili kuhakikisha kwamba wananchi hawa wanapata maeneo ya kuchimba madini.

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa eneo la Nyakagwe, Serikali imejitahidi sana kuhakikisha kwamba wananchi hawa wanapata maeneo na tayari sasa hivi wanaendelea kuchimba, tena wana amani ya kutosha kwa sababu tayari Serikali imewatengea eneo ambalo wanachimba bila wasiwasi. Vilevile katika eneo la Rwamgasa, pia eneo hili ni sehemu muhimu ambalo wananchi wengi wanahitaji kupata maeneo. Maeneo waliyopewa na Serikali bado hayatoshi. Kwa hiyo, naendelea kuiomba Serikali hasa katika maeneo ya Bingwa Reef, eneo hili liko wazi. Naomba kwa kweli Serikali itoe tamko kuhusiana na eneo hili. Kuna wananchi ambao wameomba leseni katika eneo hili hawajapewa mpaka sasa. Naomba kweli wananchi wafikiriwe kupewa maeneo haya ili waweze kufaidika na raslimali zilizopo katika maeneo yao. Kumbuka mji wa Katoro na Rwamgasa, miji hii inajengwa kutokana na rasilimali ya dhahabu inayopatikana katika machimbo haya ya wachimbaji wadogowadogo.

Mheshimiwa Spika, katika eneo la Tembo Mine hata siku ya hotuba ya Waziri Mkuu nilizungumzia suala hili. Lengo la wachimbaji wadogowadogo kuchimba ni kujinufaisha katika mahitaji yao ya kila siku. Wanahitaji kusomesha watoto wao, wanahitaji kula na mwaka huu kuna njaa iliyokithiri katika eneo hilo na wananchi wanahitaji kuchimba madini ili waweze kujinufaisha katika maisha yao. Eneo hili la *Tembo Mine* ni eneo ambapo wananchi wengi walikuwa wakichimba madini na wakijipatia madini haya kwa ajili ya mahitaji ya familia zao lakini cha kushangaza Serikali imeamua kuwaondoa wachimbaji wadogowadogo bila hata kuwapa eneo mbadala. Kwa hiyo, naiomba Serikali kweli iangalie namna au uwezekano wa kuweza kuwapa maeneo mbadala la sivyo migogoro katika maeneo ya madini haitakwisha.

Mheshimiwa Spika, naiomba pia Serikali iendelee kunisikiliza hata mimi mwakilishi au Mbunge wao ambaye wananchi wananipa kilio hiki kila wakati na ninapowasilisha kilio hiki kweli naiomba Serikali na Mheshimiwa Waziri anisikilize lakini pia asikilize sauti za wananchi hawa kwa sababu wananchi hawa wanategemea uchimbaji wa madini, hawana kitu kingine wanachokitegemea. Kwa hiyo, naomba pale ambapo majumuisho yanafanyika nisikie wale walioondolewa katika machimbo ya *Tembo Mine* hatma yao ni nini? Nisikie wamepewa eneo lingine jipya mbadala ili waendelee kuchimba madini katika maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, mwaka jana katika bajeti tulipitisha mfuko kwa ajili ya wachimbaji wadogowadogo, lakini mfuko huu umekuwa ndoto. Kule Nyarugusu, Rwamgasa na Katoro hatusikii na hatujaona mfuko huu sasa sielewi kwamba mfuko huu unatumika wapi, milioni 525 zimetumika kwa ajili ya kuwaelimisha na kuwawezesha wachimbaji wadogowadogo lakini wachimbaji wa Rwamgasa na Nyarugusu kweli hawajaona mfuko huu. Kwa hiyo, nachukua nafasi hii kuiomba Serikali kwamba kwa vile katika bajeti ya mwaka huu pia tumepitisha kuna mfuko wa wachimbaji wadogowadogo, naomba iangalie uwezekazo ili hawa Wanyarugusu waweze kufaidika na mfuko huu, wasifaidike watu wengine tu.

Mheshimiwa Spika, nina ombi kuhusiana na hii sekta ya madini. Katika Halmashauri ambazo kuna madini, naomba kuwepo na Afisa Madini wa Wilaya ili aweze kuwajibika hata katika vikao vya Halmashauri. Mara nyingine Madiwani na Wabunge tunakuwa na maswali lakini hatuna mtu wa kumuuliza, Afisa Madini Mkazi ambaye anakuwepo Wilayani yupo kwa ajili ya Wizara lakini hayupo kwa ajili ya Halmashauri. Kwa hiyo, nachukua nafasi hii kuomba kwamba awepo Afisa Madini katika Halmashauri ambazo zina madini ili pia tuweze kuuliza na kuhoji na kwamba afuatilie zile *cooperate social responsibility* ambazo mashirika makubwa kama GGM wanatakiwa kuchangia katika maeneo yetu ili tuweze kumuhoji mtu huyu kwa sababu sasa hivi hatuna mtu wa kumuuliza kuhusiana na jambo hili. Nadhani tukiwa na Afisa Madini katika Halmashauri nina uhakika mambo yetu yatakwenda vizuri kwa sababu mtu huyu atakuwa na muda mzuri wa kuweza kufuatilia na pia kuweza kujua kwamba Sekta ya Madini katika Halmashauri ina mchango gani kwa ajili ya uchumi na mapato ya Halmashauri husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niseme kwamba migodi mikubwa kwa mfano *GGM*, ni migodi ambayo iko katika Wilaya ya Geita na sehemu nyingine kama *Barrick* kule Kahama lakini migodi hii kusema kweli ipo tu kwani hatuoni kitu chochote kile, kweli wanachangia kwa kiasi fulani lakini hatuoni mchango wao kiuhakika. Mfano tu, kuna ile barabara ya mgodi kutoka Geita kwenda Ilogi kule Kahama, mimi kwa maoni yangu, nashauri watu wa *GGM* watusaidie kuweka lami kwa sababu wananchi wanateseka sana na vumbi linalotoka na magari mengi yanayobeba vifaa kupeleka kwenye mgodi wa *GGM*. Kuna wananchi wengi wanaoishi katika maeneo ya Ikina kule Bukori pamoja na Nyarwanzaja na Buyagu, kwa kweli wanateseka na vumbi lakini wakiweza kuweka lami mimi nina uhakika kwamba matengenezo yake baada ya kuweka lami yatakuwa ni kidogo sana. Sasa hivi kila mwaka wanatumia fedha nyingi kwa ajili ya kuboresha hizi barabara. Kwa hiyo, naomba kweli hata sisi wa Nyaraguru tuone kweli madini yetu yametusaidia kwa njia moja au nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la umeme, nichukue nafasi hii kuishukuru Serikali kwa mradi wa *MCC* ijapokuwa bado sijaona utekelezaji wake, kweli kuna hatua zinazoendelea. Nichukue nafasi hii kusema kwamba ni wakati muafaka sasa kuona utekelezaji wake katika maeneo yaliyotajwa hasa ya Nyarugusu, Rwamgasa na Bukori, tuweze kuona basi umeme unawaka kuliko hivi sasa ambapo tunapewa tu ahadi lakini hakuna kinachoendelea. Vilevile matatizo ya umeme hasa katika Wilaya ya Geita imekuwa ni tatizo, huu mgao mbona mimi naona kama umezidi sana Geita? Siku tatu hakuna umeme? Juzi nimewasiliana na Hospitali ya Wilaya wanasema hata maji imeshindikana ku-*pump* kwa sababu hakuna umeme, siku tatu! Wagonjwa wanateseka sana pale Hospitali. Kwa hiyo, nachukua nafasi hii kuomba na kwamba tuangalie hata hii migao kwa kweli sehemu nyingine kama Geita hali ni mbaya sana.

Mheshimiwa Spika, vilevile naomba kusema kwamba katika maeneo ya madini kwa mfano Mji wa Geita, nafikiria kwamba Mgodi ungeweka lami kuzunguka Mji wa Geita kwa sababu vumbi linasababishwa na magari mengi ya mgodi, lakini wakiweka lami hakika wananchi wa Geita watafurahia na watanufaika na kuwepo kwa mgodi huu kuliko hivi sasa ni vumbi jekundu.

Mheshimiwa Spika, sitaunga mkono hoja mpaka Mheshimiwa Waziri atakapozungumzia habari za Rwamgasa, Tembo na sehemu nyingine zinazohusika na madini wapewe maeneo ya kuchimba. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Beatrice Shelukindo atafuatiwa na Mheshimiwa Faith Mitambo na Mheshimiwa Dunstan Mkapa ajiandae.

**MHE. BEATRICE M. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwanza, naomba niseme kwako na wananchi wote wanaonitazama kwamba naomba Mungu anisimamie kwa nitakayoyasema.

La pili, nimeombwa sana nisichangie bajeti hii lakini naomba radhi watu wote mlioniomba, mimi niliapa kuingia hapa aidha nisimame niseme kweli au ninyamaze nisiongee kabisa. Nimeamua nisimame ili niseme kweli.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, kwa niaba ya wananchi wa Kilindi, nichukue fursa hii kuwashukuru sana *REA*. Hapa namtaja Mwenyekiti wa Bodi hiyo Ndugu Ami Mpungwe pamoja na Mwakahesya Mkurugenzi Mkuu na Watendaji wote. Wametusaidia sana umeme Kilindi lakini pamoja na kutusaidia ninatoa raia moja kwamba *Transformer* maeneo ambayo umeme umepita kama Mkuyu, Mgera, Msanja, Kwamaligwa, Kwamande na maeneo mengine mengi kwa sababu ya muda siwezi kuyataja yote lakini wananchi wa Kilindi muelewe yote hayo nimeshayawasilisha kwa maandishi, sasa hivi ni msimu wa mavuno, watu wanavuna, wanaomba kuunganishiwa umeme, nguzo fupi za *distribution* hazipo. Naomba watu wa *REA* pamoja na kazi hii mliyoifanya lakini mtusaidie kwa hilo. Nawapongeza sana kwa kutusaidia umeme wa kuendesha jenereta za maji yasonge Makao Makuu ya Wilaya, ilikuwa haina maji lakini sasa tumepata umeme tunaishukuru sana *TANESCO*, Mhando nakushukuru pamoja na watu wa *REA*.

Mheshimiwa Spika, katika kabrasha la Mheshimiwa Waziri, naomba Mheshimiwa Waziri nikuambie wewe na ofisi yako ingawaje unajua lakini najua kinachotokea pale kwako. Kilindi ni Wilaya tangu mwaka 2004, katika makabrasha yako tumeonekana kama Kata ya Handeni. Hili ni kosa kubwa sana kwetu sisi, tunaomba mambo yetu yote yaonekane kama Wilaya ya Kilindi na siyo chini ya Handeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la madini, natoa shukrani sana kwa kutengewa maeneo ya wachimbaji wadogowadogo, wananchi wa Kilindi wanashukuru lakini maeneo ya wachimbaji wadogowadogo wangapi wa Kilindi? Hawazidi 12 ingawaje zimetolewa leseni zaidi ya 1500 lakini zaidi ya 12 hakuna na wamewezeshwa, kila siku tunasikia vifo kwa sababu hawana uelewa na hawana njia yoyote. Kwa hiyo, haya yote nimeona niyaseme kwa niaba ya wananchi wa Kilindi.

Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii kumshukuru sana Kamishna wa Madini, Bwana Kafumu na Bwana Samaje pamoja na baadhi ya Maafisa. Wamekuwa wakitusaidia, nawaita hata usiku kwa ajili ya *crisis* zinazotokea Kilindi na nimekuwa nikipata ushirikiano wao, nashukuru sana. Tatizo kubwa ni kwamba mliahidi miaka

mitatu iliyopita, Mheshimiwa Waziri ulitamka kwamba tutakuwa na ofisi ya Madini Kilindi lakini hadi leo hakuna kinachoendelea. Mmesema sasa hivi ukusanyaji wa mapato Halmashauri zijitahidi, sisi Wilaya nzima imegawanywa kwenye *PL* za wachimbaji wakubwawakubwa. *PL* kutokana na Sheria yenu hawalipi mapato yoyote basi liangalieni suala hili, sisi tunaumia. Madini tunayo kila kona ya Wilaya lakini hatuwezi kupata fedha.

Mheshimiwa Spika, nije kwenye nishati. Watanzania wanataka umeme, sasa haya naongea ni mambo niliyoyapata *weekend* hii. Wanasema tunashangaa, Mzee mmoja anaitwa Mzee Salehe, anasema ninyi mnaongea vitu vingi lakini mbona hatuwaelewi? Sisi tunataka umeme, hizo hadithi nyingine ni za kwenu, tunataka umeme.

Mheshimiwa Spika, mimi naomba niseme Mheshimiwa Naibu Waziri na Naibu Waziri, kipindi kilichopita cha miaka mitano ambacho mimi nilibahatika kuwa kwenye Bunge hili, yaani mlikuwa wazuri. Mheshimiwa Ngeleja nadhani ulikuwa una-*rank* wa kwanza katika Mawaziri wote, unasoma *speech with confidence* na mambo yako yote yalikuwa yanakwenda vizuri, wewe ni kiongozi mzuri sijui pametokea nini. Safari hii hata kusoma *speech* ulikuwa una…

**SPIKA:** Mheshimiwa Shellukindo, *we are talking about a Minister* wa *Energy* na Madini, naomba iwe hivyo.

**MHE. BEATRICE M. SHELLUKINDO:** Sawa!

Mheshimiwa Waziri, safari hii hata *speech* yenyewe ulikuwa unasomwa kwa wasiwasi kwa sababu unajua vitu vingi havijakamilika, nyingi ni ahadi na nyingi hazijatekelezeka na hazitekelezeki. Kwa hiyo, yote haya mimi nikajua kwamba ni lazima kuna tatizo mahali. Hili suala la dharura, unajua kwa heshima kabisa kitu kama Kilimo Kwanza siyo cha dharura lakini umeme ni kitu cha dharura.

Mheshimiwa Spika, nimepokea simu za uchungu sana, watu wanasema sisi tumemaliza Chuo Kikuu hatuna kazi wala ajira, tumebahatisha tumechukua mikopo tumeanzisha *Internet Café* na *Stationery* lakini tunashindwa, hatuna majenereta. Sisi tunaongea kwa sababu wenzetu kutokana na stahili zao pengine wana majenereta na yanawekwa mafuta ndiyo maana tunaongea kwa uchungu, tunaelewa tatizo pengine siyo Mheshimiwa Waziri wala Naibu Waziri, tatizo ni *system* nzima iliyopo pale inabidi iangaliwe upya. Miradi karibu yote uliyotusomea itaanza mwaka 2014-2015, hapa katikati tunafanyaje?

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri atakumbuka mwaka 2008 walituambia hapa na ninadhani Mkuu wa Nchi pia aliwahi kulisema hilo kutokana na ushauri wenu kwamba baada ya miezi 18 kutakuwa na umeme tena umeme wa kudumu, uko wapi? Sasa mimi naona kabisa kwa kweli kuna jambo la kuliangalia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kiwira, *STAMICO* walikuwa na *TANESCO* wapewe ile waendeshe kwa mkopo sijui wa China milioni 400, sina kumbukumbu sahihi, lakini

ndiyo ilikuwa hivyo, hadi leo hakuna kilichofanyika. *Geothermal* walikwenda Addis Ababa wakaelekeza Tanzania iwe ndiyo *pilot area* kwa ajili ya *Geothermal.* Mheshimiwa Naibu Waziri alikuwepo na alisaini lakini mpaka leo hakuna kilichofanyika, wenzetu Kenya sasa hivi wana-*win* kwa umeme wa *Geothermal. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kweli nasema vifaa vinaungua, nimepokea simu kwamba Mama hebu tuulizie huko, vifaa hivi vinavyoungua na huu umeme unaokuja na kukatika nani anayetufidia? Tunawapa Watanzania umaskini na wawekezaji wanakimbia. Jumuiya ya Afrika Mashariki sasa hivi tunakwenda kwenye hatua ya mwisho, tumeshamaliza Ushuru wa Forodha wa pamoja, Soko la Pamoja, Fedha ya Pamoja na sasa hivi tunakwenda kwenye Shirikisho moja, Watanzania bado tunahangaika na umeme, wawekezaji wanakimbia sisi wenyewe tunazidi kuwa maskini, haiwezekani! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa utafiti wangu mdogo japo matatizo ni mengi, Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri ninyi kama nilivyosema sijui kama ninyi ndiyo tatizo lakini Watendaji wenu wanawaangusha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mara baada ya kuongea kama utanitaka nitaweka Mezani hii barua, sisi hapa tunahangaika tufanyaje kuhusu gharama za umeme, kuna barua ambayo imetoka kwa Mtendaji Mkuu inasema:-

Yahusu kuchangia gharama za kukamilisha maandalizi ya uwasilishaji wa hotuba ya bajeti ya Wizara 2011/2012 Bungeni Dodoma. Anaielekeza Taasisi na Vitengo na Idara zote zilizopo chini ya Wizara yake, anaeleza mafanikio kwamba Wizara imefanikisha mpango na bajeti kwa mwaka huu na imeshapitishwa na Kamati ya Kudumu ya Nishati na Madini. Katika kukamilisha mchakato huu, hotuba ya bajeti inatarajiwa kuwasilishwa Bungeni tarehe 14 na 15 Julai, naruka *paragraph* inayoendelea, ili kufanikisha mawasilisho ya hotuba ya bajeti unaombwa kuchangia jumla ya shilingi 50 milioni. Fedha hizo zitumwe *Geological Survey of Tanzania (GST)* kwenye Akaunti Namba 5051000068, *NMB*, Tawi la Dodoma. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Aondoke huyo!

**MHE. BEATRICE M. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Spika, sasa hizi fedha zote shilingi 50 milioni kwa kila Taasisi na kila Idara ni shilingi ngapi? Nimefanya utafiti, nimegundua hizo fedha nadhani zinazidi shilingi bilioni moja, zimekwenda wapi? Kwa utafiti wangu wa karibu nimeuliza hizi Taasisi zimekuja kwa fedha zao, wamejigharamia wenyewe *per diem*, kama kuna fedha zote hizi zimekwenda wapi? Waziri atuambie hizi fedha na imesainiwa, sijamaliza, inasema, nashukuru kwa ushirikiano wako, David K. Jairo, Katibu Mkuu.

Mheshimiwa Spika, barua nitaiweka, Mezani ninayo hapa. *(Makofi)*

Jamani hivi kweli jina la Mkuu wa Nchi linatumika ovyoovyo mle ndani kwa vitu ambavyo si vya kweli! Kitu kidogo Mkuu wa Nchi kaagiza, mara Mkuu wa Nchi kasema hivi, kazi itakwenda? Maskini ndugu zangu Waziri na Naibu Waziri wanaogopa,

wameteuliwa na huyo Mkuu wa Nchi wakisikia hivyo ndiyo wanakuwa wanafanya vinginevyo. Tatizo lipo pale kwako Mheshimiwa Waziri na naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu asikie na Mkuu wa Nchi wasikie kwamba tatizo liko pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hii barua nitaiweka Mezani, fedha zimekusanywa tujue zimekwenda wapi kwa sababu Katibu Mkuu Kiongozi alishapitisha fedha zisitolewe kabisa kwa Wabunge na kadhalika, sasa hii imekuja vipi? Sasa mimi naomba fedha hizo tujue zimekwenda wapi? Mafuta ya taa yamepanda bei, wananchi wameshindwa kununua shilingi 2,000/= kwa mwananchi wa Kilindi haiwezekani lakini hapa kuna mabilioni yamechukuliwa sijui na mtu au nini maana yake amesema iende *GST*, kwa hiyo *GST* inabidi tuichunguze vizuri, ndiyo ya kupelekewa fedha za hivi? Mheshimiwa Waziri kazi kwako, chunguza kwa nini ziende *GST* fedha ambazo hazina kichwa wala mkia?

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nakwenda kwenye ufilisi wa *IPTL,* muda unakwenda haraka, *IPTL* sasa hivi tayari imeshafika *RITA*, *RITA* ndiyo mfilisi lakini unashangaa kwa nini hawamalizi *process* na huko eti kila mwezi yananunuliwa mafuta kwa ajili ya kuendesha *IPTL*. Nadhani kama sijakosea taarifa nilizopata kama sijachanganya ni shilingi bilioni mbili kwa mwezi.

**MBUNGE FULANI:** Bilioni 17.

**MHE. BEATRICE M. SHELLUKINDO:** Bilioni 17 kwa mwezi, badala ya kufilisi hili linakumaliza bado inaendelea na hapa naambiwa Mtendaji Mkuu na yeye yuko hapohapo anayajua hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kweli mimi nimeona watu wengi wamezungumza kuhusu hili, waliounga mkono kama nimewaona wote ni *with reservation*. Mimi nakusudia leo jioni kabla Mheshimiwa Waziri haja-*wind up* kutoa hoja na nitaomba Waheshimiwa Wabunge wote mniunge mkono kwamba hoja hii isipitishwe, irudishwe, wakaifanyie kazi na baada ya wiki mbili au tatu kwenye Bunge hili la Bajeti irudishwe hapa ikiwa imekamilika na mkakati wa mpango wa dharura uwe umeshakuja hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, leo nimesema sina mengi ya kusema kwani yote yameshasemwa na kila mtu. Turudishe ili wananchi wawe na imani na Bunge lao bila kujali itikati, wajue sisi tuna uchungu nao. *(Makofi)*

**SPIKA:** Tunaendelea na Mheshimiwa Faith M. Mitambo na Mheshimiwa Dunstan Mkapa ajiandae, Mheshimiwa Hamadi utafikiwa.

**MHE. FATMA A. MIKIDADI:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Faith Mtambo ana dharura.

**SPIKA:** Basi tunaendelea na Mheshimiwa Dunstan Mkapa.

**MHE. DUNSTAN D. MKAPA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia katika bajeti hii ya Wizara ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Spika, najua wenzangu kama Mheshimiwa Shellukindo ameongea vizuri sana na wengine waliochangia hoja hii kwamba suala kubwa hapa wananchi wanataka umeme na ni umeme wa uhakika. Kwa hiyo...

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, mtulie ili kusudi tumsikilize Mheshimiwa Mkapa. Haya Mheshimiwa Mkapa endelea!

Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini pamoja na jopo lako lote la Wizara tunachoomba hapa ni umeme wa uhakika, tumechoka kupita Dar es Salaam na kusikia kila mtu ana jenereta linaunguruma utafikiri mji umevamiwa na nyuki. Watu wanashindana pale kwa ukubwa wa jenereta, mwingine kubwa, mwingine ndogo, mwingine la kati, ili mradi tu mji wenyewe umechafuka, mkiongea hamsikilizani sababu ya kelele za jenereta. Kwa hiyo, tunamwomba Mheshimiwa Waziri atafute suluhisho la mwisho kuhusu tatizo la umeme. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba nije kwenye hotuba ambayo aliitoa Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, ukurasa wa 65, aya ya 131 naomba kunukuu: "Katika mwaka 2011/2012, Serikali itaendelea na utekelezaji wa miradi ya kupeleka umeme kwenye Makao Makuu ya Wilaya" mojawapo ya Wilaya ni Nanyumbu. Nitoe shukrani kubwa sana kwa Serikali kwa kusikiliza kilio changu, kwa sababu nilikwishawahi kuuliza swali hapa kwamba, ni lini umeme utakuja Nanyumbu? Nadhani hili sasa ni suluhisho kwamba tunategemea kupata umeme wa uhakika katika mwaka wa fedha huu wa 2011/2012, nami kwa niaba ya wananchi wa Wilaya ya Nanyumbu naomba nishukuru kwa Serikali kusikia wito huu na wananchi wa Nanyumbu wanategemea kupata umeme huu ili uweze kuwanufaisha.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo, naomba umeme huu utakapokuja basi hizo nyaya zisipite juu ya vijiji ambavyo utapita huu umeme. Naomba umeme huu uwafikie wananchi kuanzia pale Namatundusi, Kilosa, Nangaramo, Nangomba, Ndwika mpaka Mangaka ili waweze kunufaika na na umeme huu ambao utapita kwenye vijiji vyao, waweze na wao kufanya miradi yao midogo midogo ambayo inatokana na nishati hii ya umeme.

Mheshimiwa Spika, lakini pamoja na hayo, naomba, baada ya kupata umeme huu pale Mangaka ambapo ni Makao Makuu ya Wilaya, uweze pia kusambazwa katika maeneo mengine kwa mfano, Kituo cha Afya cha Michiga ambapo panajengwa jengo la upasuaji ili liweze kufanya mambo yake kiutaalam zaidi kwa kupata umeme wa uhakika. Vilevile umeme huu ufike kwenye Kituo cha Afya cha Nanyumbu ili pia shughuli za hospitali zisiweze kukwama. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vilevile umeme huu ningeomba ufike kule Mtambaswala, pale kuna daraja la Umoja ambalo limejengwa, kuna *TRA*, Uhamiaji na Polisi. Hivyo, hawa wote pamoja na wananchi wa Mtambaswala, wanufaike na umeme huu ambao tumeahidiwa kwamba utakuja.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Nanyumbu hatuna viwanda, vijana wanakaa tu vijiweni kwa kukosa viwanda na hii inatokana na kukosa umeme wa uhakika. Naomba Wizara ihakikishe kwamba, tunapata huo umeme wa uhakika ili vijana wetu wa Wilaya ya Nanyumbu na wenyewe waweze kupata viwanda vidogovidogo kwa mfano vya kubangua Korosho ili waweze kujinasua katika lindi kubwa la umaskini.

Mheshimiwa Spika, kuhusu madini. Wilaya yetu ya Nanyumbu yapo madini lakini sijaona juhudi yoyote ya Serikali ya kutafuta madini hayo. Wananchi wanajitafutia tu hayo madini kwa kubahatisha hapa na pale, lakini cha ajabu ni kwamba tumesahauliwa sana, utafiti haujafanywa pale wa kutambua sehemu za madini. Mheshimiwa Waziri naomba sana Wizara yako itume wataalam wa kuweza kutafuta madini katika Wilaya yetu ya Nanyumbu. Kuna maeneo mengi tu, kuna miamba mikubwa mikubwa pale katika Kata za Napacho, Likokona na Mkangaula. Nadhani miamba hiyo haiwezi kukosa madini. Utafiti ufanywe ili Serikali na wananchi waweze kunufaika kutokana na madini ambayo yanaweza kupatikana pale.

Mheshimiwa Spika, vile vile nahisi kwamba, katika mbuga au misitu hii ya uwindaji panaweza kuwa na madini hapo, lakini kwa sababu ya sheria zilizopo wananchi wanashindwa kwenda kuchimba kujipatia riziki kwa ajili ya kupunguza makali ya maisha.

Mheshimiwa Spika, sasa nichangie kuhusu mafuta ya taa, tumepitisha sheria hapa ya kuongeza bei ya mafuta ya taa, lakini kwa mtu wa kawaida wa Wilaya ya Nanyumbu, kumwongezea bei ya mafuta ya taa kwa kweli ni kumwongezea makali ya maisha. Naomba kama walivyosema wachangiaji wengine kwamba *revenue* itakayopatikana kutokana na ongezeko hili la bei ya mafuta liweze kupeleka umeme vijijini ili wananchi waweze angalau kuona tofauti kubwa baada ya kuongezwa kwa bei hii ya mafuta. Kwa kweli nimeombwa na wananchi wa Nanyumbu kwamba ongezeko la bei ya mafuta ya taa ni mzigo mkubwa kwao.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo nirudi tena kwenye suala la umeme. Naomba umeme huu ukija, basi uwe wa bei nafau. Tuliahidiwa kwamba umeme huu utaunganishwa kwa wanavijiji kwa bei ya shilingi elfu sitini (60,000/=), lakini sijaona juhudi zozote zinazofanywa na kampuni hii kama ni *TANESCO* au nyingineyo, za kuunganisha umeme katika majumba ya wanavijiji. Pale Msimbati umeme unapita juu tu, wananchi wanauangalia tu na umeme huu unatoka kwao pale pale, hawajaunganishiwa umeme na umeme umepita kwao. Naomba sana sana bei hizi zipunguzwe ili wananchi wa pale Msimbati na maeneo mengine umeme huu unakopita, Nangoo, Ndanda, Chigugu na kwingineko waweze kunufaika na umeme huo kwa bei nafuu. Hatujaona juhudi yoyote, sijaona kijiji chochote kati ya hivyo ambacho kimekwishaunganishiwa umeme tayari, wakati umeme upo na unapita kwenye vijiji vyao.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii na naunga mkono hoja hii kwa sababu Serikali imeahidi kutuletea umeme katika Wilaya ya Nanyumbu. Ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA**: Nashukuru kwa kunigawia muda. Sasa nitamwita Mheshimiwa Christopher O. Ole – Sendeka, halafu Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed ajiandae na Mheshimiwa Esther Bulaya atafikiwa.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE–SENDEKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja ya Waziri wa Nishati na Madini mchana wa leo, Wizara ambayo ni muhimu sana kwa maendeleo ya nchi yetu, lakini muhimu pia kwa Jimbo langu la Simanjiro.

Mheshimiwa Spika, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema, lakini nakushukuru wewe mwenyewe pia kwa jinsi unavyoliongoza Bunge letu na kuendelea kwa kweli kuwakomaza Wenyeviti wa Bunge letu ambao ni wapya na ambao kwa sasa hivi hata wanavyoliendesha Bunge wanaonekana kama wana uzoefu mkubwa kabisa. Hongera sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimerejea leo hapa Dodoma nikitokea Mbeya kufanya kazi moja ambayo wasiojua historia ya nchi hii wanaweza kupata tabu. Miaka ya 1980 Chama Tawala, Chama cha Mapinduzi kilikuwa na mpango na programu ya chama ambayo kuna kazi ya Chama ndani ya Chama, kazi ya Chama nje ya Chama ndani ya umma na kazi ya Chama nje ya Chama ndani ya umma dhidi ya maadui. Nilikuwa nafanya kazi ya Chama, ndani ya umma jambo ambalo wengine wanafikiri tumekwenda kuiga kutoka kwao. Unajua ninyi mliiga maana hamkuwepo miaka ya themanini (1980) (*Makofi*/*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo, naomba niendelee. Najua mapigo haya ni mazito kidogo kwa makada wenzangu waliopewa dhamana katika Wizara hii, lakini nianze na yale ambayo nisipoyaanza huenda nikayasahau na Wanasimanjiro hawatanielewa. La kwanza, ni kuwashukuru kwa kuipongeza Serikali ya Chama cha Mapinduzi (CCM) kwa kusikia kilio cha muda mrefu cha wananchi wa Kata ya Msitu wa Tembo, katika Vijiji vya Msitu wa Tembo, Kiruani, Majengo, Magadini hadi Korongo, kupelekwa kwa umeme wa gridi ambao kwa mara ya kwanza tangu kuumbwa kwa dunia na wao watapata fursa ya kuwasha umeme. Nataka niwapongeze sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Wasaidizi wao.

Mheshimiwa Spika, nataka pia niwashukuru kwa jinsi ambavyo katika bajeti yenu mmekumbuka Korongo la Disuza lililoko katika Migodi ya *Tanzanite* pale Mererani ambalo kwa vipindi viwili tofauti limesababisha vifo vya Watanzania wapatao 200 na kwamba katika bajeti ya mwaka huu mmetamka katika hotuba ya Waziri kwamba mtatenga fedha kwa ajili ya kuhakikisha kwamba mtaro huo unarekebishwa kwa namna ambayo haitaleta tena vifo vya wapiga kura, wangu wa Simanjiro kama ilivyotokea huko nyuma. Nampongeza Mheshimiwa Waziri katika hilo.

Mheshimiwa Spika, nina rai moja muhimu sana kwao kwamba, pamoja na tatizo la umeme nchini, haja ya umeme pale Mererani na mgao unaotolewa usiozingatia ratiba, unahatarisha maisha ya wachimbaji wadogo wadogo pale Mererani, maana wakati mwingine wakijua kwamba umeme utakuwa katika sehemu yao ya migodi kati ya saa 6 –

10 watakuwa wanaingia katika migodi ile, lakini kama ratiba ile isipoheshimiwa na umeme ukakatika unatishia usalama wa wachimbaji walioko katika eneo hilo. Natoa rai kwamba, ratiba mnazozitoa nazo mziheshimu ninyi wenyewe. Bado ni rai yangu kwamba pamoja na kuwepo kwenye programu ya Wakala wa Umeme Vijijini (*REA*), Vijiji vya Naberera, Lendanai na Namalulu, umeme uendelee katika Kata za Terati na Oljoro Na. 5 na Komolo, umeme unaotoka Oljoro, JKT. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nihitimishe na lingine moja la Simanjiro, nalo ni kuungana na Kamati yangu ya Nishati na Madini ambayo mimi ni Mjumbe, katika kuendelea kuishauri Serikali kuwa na kanuni mahsusi kwa ajili ya uchimbaji wa madini ya vito ya *Tanzanite* kutoka jiolojia ya uchimbaji wa madini ambayo inakwenda mshazari. Jiolojia ya uchimbaji wa madini ya *Tanzanite* inayokwenda mshazari inahitaji kuwa na kanuni tofauti na uchimbaji wa madini mengine ya vito au aina nyingine ya madini.

Mheshimiwa Spika, bado ni rai yangu kwa Waziri mwenye dhamana kuja na kanuni ambayo ni shirikishi itakayohakikisha kwamba wachimbaji wa *Tanzanite* Mererani, wanawezeshwa kuchimba kwa kufuata kanuni moja, wachimbaji wadogo na wachimbaji wakubwa na siyo kuwa na kanuni inayoheshimu tu maeneo ya wachimbaji wadogo, lakini wakubwa wanawekwa pembeni.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiofichika kwamba tumeunda Tume nyingi katika kushauri Sekta ya Madini; Tume ye Jenerali Mboma, Tume ya Meja Jenerali Mang'enya, Tume ya Masha, Tume ya Kipokola na Tume ya Jaji Mark Bomani, lakini bado yako mambo ya msingi yaliyopendekezwa na Tume hizi ambayo bado hayajafanyiwa kazi. Naamini kwamba, yale tuliyopitisha katika Sheria ya Madini ya Umilikaji wa Madini ya Vito kwa Watanzania kwa asilimia mia moja (100%) haitafanyiwa mzaha, itatekelezwa kwa vitendo na huko mbele itakapofika mwaka ujao nadhani tutaelewana vizuri kwenye hili.

Mheshimiwa Spika, nataka niseme, uvumilivu una ukomo na hili ndiyo jambo ambalo nataka nilizungumze na hasa katika suala zima la hali ya umeme nchini, hususan suala zima la mikataba tunayoingia. Tunajua wazi kwamba sasa hivi tuko kwenye mgogoro wa ukosefu wa umeme nchini, Watanzania wanachotaka kuona ni vitu vikubwa viwili; kwanza wanataka sisi tuliopewa dhamana tuonekane kuhuzunika nao, tuonekane kwamba tunaguswa na tatizo hili, lakini tuonekane pia kwamba hatuiingizi nchi katika mikataba ambayo haina maslahi kwa nchi. Haiwezekani tukawa tunalia kwa habari ya tatizo la umeme wakati bado uwekezaji wetu ni kuiachia sekta binafsi iendelee kuwekeza ili tuendelee na mitambo ya kukodi ambayo ina *capacity charge* inayoipunguzia *TANESCO* uwezo wa kutoa huduma kwa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, ni kwa nini Serikali yetu msichukue hatua za makusudi kabisa kuhakikisha kwamba mnatenga fedha hata kama ingetoka kwenye *OC* ya bajeti ya mwaka huu, mkahakikisha kwamba kama mahitaji ya kuleta mitambo ya kuzalisha *MW* 200 au *MW 300* tunayohitaji ni shilingi bilioni 500 au 600, tukaamua kutenga na wote tukafunga mikanda kuhakikisha kwamba ufumbuzi wa tatizo la umeme unapatikana. Kwa nini mnang'ang'ania na mitambo ya kukodi? Maana mnapong'ang'ana na mitambo

ya kukodi ndipo mnapoweka hisia za kuaminika kwamba, katika mitambo ya kukodi ya watu binafsi, pengine kuna manufaa binafsi yanayopatikana huko. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya Tume ya Mheshimiwa Harrison Mwakyembe, Bunge hili liliazimia kwa kauli moja kwamba, Serikali iondokane na mitambo ya kukodi na ihakikishe inakuja na mpango mahususi wa kununua majenereta au mitambo yake ya kuzalisha umeme badala ya kutegemea mitambo na majenereta ya watu binafsi. Kinachoonekana hadi sasa bado mnaendelea, mlitoka *Richmond*, mkaja *Dowans*, leo mnaye *Symbion*, hapa sioni ikizungumzwa sana habari ya *Symbion* kana kwamba wewe Mkatoliki ukiamua kushahadia na kusilimu, hata kama ulikuwa na madhaifu yako, basi unakuwa umetakasika. Hili leo silizungumzi lakini huko mbele nitatafuta muda wa kulizungumzia vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nina hoja ya kuzungumzia pia juu ya baadhi ya mapendekezo ambayo yametolewa katika bajeti ya Waziri wa Nishati na Madini kuhusu fedha zilizokuwa zimetengwa, shilingi bilioni 1.1 za kuwasaidia wachimbaji wadogo. Hili kwa kweli ni dhihaka, kama mnaweza kutenga shilingi bilioni moja kwa wachimbaji wadogo wa Tanzania nzima, hili bado ni dhihaka. Bado nafikiri kwamba ipo haja ya kuhakikisha kwamba tunatenga fedha nyingi kwa ajili ya kuwasaidia wachimbaji wadogo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini jambo lingine ambalo ni muhimu ni kuhakikisha pia kwamba, fedha zile zilizotengwa shilingi bilioni 1.8 kwa ajili ya kujenga Kituo cha Polisi, kama Kamati ya Nishati na Madini ilivyoshauri kazi hii ya kujenga Vituo vya Polisi siyo dhamana ya Wizara ya Nishati na Madini, iachiwe Wizara ya Mambo ya Ndani, fedha hizi zielekezwe kwenye maendeleo ya gesi. Bado nina rai yangu pia kwamba, hata lile jengo mnalotaka kulijenga Dar es Salaam la Makao Makuu ya Wizara, ondokeni Dar es Salaam njooni Dodoma. Someni Ilani ya Uchaguzi, katika ukurasa wa 250, majengo yote ya Wizara yanatakiwa yajengwe hapa Dodoma, mnang'ang'ania Dar es Salaam kuna nini?

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ni fedheha na nataka niungane na Mheshimiwa Beatrice Shellukindo, ni kitendo hiki cha barua ya Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Madini. Nililetewa pia barua na nilikusudia kuizungumzia, lakini namshukuru sana Mheshimiwa Beatrice Shellukindo kaizungumza. Mnakusanya shilingi milioni 50 kwa kila Idara iliyo chini ya Wizara kwa kazi gani? Ni kwa nini watu wasifike mahali wakafikiri uvumi uliokuwa ukienezwa kwamba pengine kulikuwa na mgawo wa fedha usiokuwa rasmi na kwamba pengine fedha hizi zimeelekezwa huko? Tunataka ukaguzi ufanyike leo, nashauri Waziri Mkuu amuagize *CAG* afanye ukaguzi wa dharura katika ukusanyaji wa fedha hizo na iangaliwe kama kuna misingi ya kisheria ya kukusanya shilingi milioni 50 kutoka kila Taasisi na fedha hizi zinalenga kufanya nini? Maana Wakuu wenyewe wa Idara wanaokuja Dodoma wako wangapi, wanahitaji kulipwa nini? Wanalipwa posho ndogo ndogo hizo kwa siku mbili ambazo wako hapa, waondoke wanatuacha sisi. Shilingi milioni 50 mara Idara zote hizo kama ni shilingi bilioni moja, ni ya kazi gani? Tunataka kujua kama hizo fedha ziko kwenye akaunti hiyo au zimechakachuliwa kuelekezwa katika maeneo mengine na baada ya hapo hata mimi

nitamuunga mkono Mheshimiwa Beatrice Shellukindo, katika hoja yake ya baadaye. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, yako mambo ya msingi mengine ambayo ni muhimu sana kuyaangalia kama Wizara. Leo mnaleta mtambo wa MW 100, mwingine wa gesi mnataka kuuweka Ubungo wakati hata ule wa *Symbion* wenyewe hamna gesi ya kutosheleza. Mmeacha ukiritimba wa gesi kwa *Pan Africa Energy* na ndiyo maana Kamati yetu ya Nishati na Madini tumependekeza Kamati ndogo iundwe ili tuangalie mgogoro wa ukiritimba uliopo katika sekta hiyo ya gesi ambao unafanya hata baadhi ya wachimbaji wengine wasifaidi miundombinu ya kusafirishia gesi kutoka katika vyanzo vyake.

Mheshimiwa Spika, haiwezekani mkawa na *monopoly* kwenye gesi kwa watu ambao fedha zenyewe walizoziwekeza ni mkopo ambao Serikali tumekopeshwa na wao walipaswa kubaki tu kwenye Menejementi, fedha hizi zingine zikawa sisi ndiyo tunasimamia rasilimali hiyo. Leo mkiachia gesi ikawa mikononi mwa watu binafsi hatari yake kwa nchi ni kubwa sana na mkitaka kuona athari hiyo someni mapendekezo ya Kamati ya Nishati na Madini kama tulivyopendekeza. Hatutaomba sana mtuunge mkono, taarifa ya Kamati yetu ndogo ya Nishati na Madini itakapowasilishwa hapa Bungeni hata kama itapelekea kuundwa kwa Kamati Teule ya Bunge ili tuhakikishe kwamba dola milioni sitini (US$ 60,000,000) ambazo ni karibu shilingi bilioni mia moja (Tsh. 100,000,000,000/=) zirejee hapa nchini kupitia *TPDC* iweze kusaidia katika sekta ya gesi na mafuta ili tuweze kujitegemea sisi wenyewe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ni ukweli pia usiofichika kwamba *MW* 60 za mafuta mazito kule Mwanza, huo kwa kweli nawaambieni utakuwa ni ufisadi wa pili. Haiwezekani mkawa mmeshindwa mtambo wa *IPTL* ambao uko hapo pua na mdomo na bahari, mmeshindwa kuweka mafuta leo mpeleke mtambo wa *MW* 60 Mwanza. Mnaleta kashfa (*scandle*) nyingine kama ile ya *ALSTOM Power Rentals* ya Mwanza, huu utakwenda kukaa pale na balaa sasa itakuwa ni mtoto wako ambaye huwezi kumwondoa tena maana ni wa kwako *TANESCO*. Hapa naona *due diligence* haijafanyika.

Mheshimiwa Spika, nataka kusema kwa heshima ya wananchi wa Simanjiro na maelekezo waliyonipa hoja hii sitaiunga mkono mpaka nitakapopata maelezo mengine ambayo yatatolewa huku na Waziri baadaye. (*Makofi*)

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Kwanza nianze na madini halafu nitakuja kwenye umeme. Rais Kabila mwaka juzi aliivunja mikataba yote ya madini mpaka pale alipohakikisha kwamba wazalishaji wa madini wanakubaliana na masharti mapya ya Serikali yake ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kwamba hayasafirishwi madini ambayo hayakukamilika. Wengi ambao walikuwa wakinunua shaba na kadhalika wote walisimamishwa mpaka pale madini yote yanayotoka Congo yasafishwe. Nataka kuiuliza Serikali hivi Rais Kabila alikuwa na meno gani ya kuvunja mikataba ile na akabaki salama, sisi Watanzania tusibaki salama.

Mheshimiwa Spika, nalisema hilo kwa sababu mwaka 2004 Bunge lako liliunda Kamati Ndogo kuchunguza *Williamson Diamond.* Kamati ikatoa mapendekezo, kwanza tulikuta kuna dola milioni mbili ziko London, ziko kwenye akaunti ya Williamson na haziko kwenye akaunti ya Serikali. Tukaiomba Serikali fedha hiyo irudishwe na mpaka leo sina hakika kama imerudishwa. Juzi niliuliza je, ile fedha imerudishwa, bado hajanipa majibu.

Mheshimiwa Spika, lakini la pili tukasema kile Kitengo Tansort kilichoko pale kiweze kuimarishwa ili almasi inayochambuliwa ipate thamani halisi. Kwa kusikitika sana pamoja na vijana wetu kuishauri vizuri Serikali, Serikali ilikivunja kile Kitengo kule kilikuwa na watu watano kikaletwa Dar es Salaam hapa wakaajiriwa watu wawili. Uwezo wa kuchambua watu watano, ulikuwa unachambua almasi kwa asilimia 25. Watu wawili waliopo wana uwezo wa kuchambua almasi asilimia 10, nisikilizeni Waheshimiwa Wabunge. Kampuni mpya *Patra* iliuchukua mgodi wa Mwadui, imenunua asilimia 75 ya hisa kwa dola milioni 10 kutokana na *financial statement* waliyoitoa wenyewe ambayo kwenye *metal exchange* ya London. Sisi asilimia 25 tuliuza kwa dola 138,000. Juzi wamesafirisha almasi kwa takwimu za Serikali ni kareti 101,030.83. Wao walipokwenda kwenye ***Antrepo*,** mnada baada ya kubadilisha utaratibu wa soko ni kareti 82,000 zilizofika kwenye *Antrepo*. Kareti 16,000 hazijulikani zimekwenda wapi? Nikauliza Serikali, Serikali wakasema mzigo ulipotea wa kareti 14,000, kwa hiyo zile 2,000 nyingine hazijulikani.

Waheshimiwa Wabunge yanayotokea mambo haya ni yafuatayo. La kwanza, katika kuchambua almasi kuna mambo manne lazima yaonekane. Moja ni rangi, jiwe lenye rangi ya juu bluu linapata fedha nyingi. Jiwe lenye rangi ya pinki linapata fedha kidogo nzuri, jiwe lenye rangi nyeupe linapata fedha nzuri kidogo. Tanzania kuna jiwe moja lenye kareti 455, limepata dola laki sita. Sasa unapokuwa huna wachambuzi wako wa kuchambua almasi mnawaacha wenyewe wachambue hayo mawe yenye thamani, huwezi kuyaona. Ndio maana mgodi huu toka uanzishwe mpaka leo haujalipa kodi Serikalini. Baya zaidi ni kwamba kuna mkataba wa muda ambao naiambia hii Kampuni sasa isafirishe almasi moja kwa moja mpaka mnadani *Antrepo*. Zamani angalau zilikuwa zinakwenda London, vijana wetu wanazichambua ndio na sisi tunajua *royalty* yetu. Sasa hivi wakishalipa *royalty* kwa hii thamani ya huku, *royalty* halisi ni ile ambayo wamepata kule mnadani. Wakati vijana wetu wanachambua walikuwa kareti moja wakipata dola 156 kwa kareti, hawa wakichambua wanapata dola 126. Kwa hiyo *royalty* wanayolipa huku wakienda waki-*declare* zile ambazo wameuza maana yake wakirudi huku lazima uwarudishie fedha yao ya ziada. Kwa hiyo, itakuwa ile *royalty* ya asilimia tano haipatikani na ndiyo maana kitabu cha *revenue* hiki, kinaonesha fedha zinazopatikana ni kidogo sana.

Mheshimiwa Spika, hivi tutafanya haya mambo mpaka lini? Vijana wetu, wataalam wetu wanatuelimisha kasoro hizi, lakini hatutaki kusikia maana yake nini kwa Watanzania? *Patra* hawa walipata jiwe moja la bluu pale Afrika ya Kusini wameuza dola 35,000,000 kwa mujibu wa *financial statement* zao. Jiwe moja tu, lakini sisi tunaambiwa mgodi kila siku una hasara. Nimefurahi juzi nasoma katika taarifa yao wanasema ile Kimberite iliyoko pale Shinyanga ina uwezo wa kutoa almasi kwa miaka 40. Walipokuwepo Williamson tulipokwenda walisema huu mgodi hauna faida. Leo

wao wenyewe Kampuni yao mama, (*subsidiary company)* yao inasema hapana, huu mgodi mzuri na utatoa almasi kwa muda wa miaka 40. Sasa swali, hivi wale Wanashinyanga pale wanafaidika nini na mgodi? Waliozungukwa na migodi ya dhahabu wanafaidika nini?

Mheshimiwa Spika, wenzetu wa Ghana, Alaska na wengine baada ya kugundua makosa haya na kuona wananchi hawaridhiki walianzisha utaratibu unaitwa *cash distribution.* Kwa mfano, Ghana wanazalisha mafuta *barrel* laki moja hivi sasa. *Barrel* 33,000 zinakwenda katika *cash distribution* kwa Waghana, kila Mghana anapata dola kutoka 60 mpaka 80. Hivi sisi Watanzania tuna maradhi gani tusipate chochote katika migodi yetu na almasi zetu. Sasa nasema haya mambo yapo duniani. Kwa hivyo, bado sisi tunaingia katika mikataba mipya, tunaendelea na matatizo yale yale tukidhani kwamba watu hawawezi kuja kuwekeza hapa nchini. Sio kweli?

Mheshimiwa Spika, ukishakuwa na rasilimali, ukishakuwa na utulivu na amani katika nchi *investor* atakuja. Asikudanye mtu kama wanakwenda Congo kwenye vita kwa nini wasije Tanzania? Haiwezekani. Lakini tumekuwa waoga tukakaa na mikataba yetu tukaifanyia kazi. Ushauri wangu, Kamati ya Nishati na Madini, Kamati ya Fedha na Uchumi, Kamati ya Katiba na Sheria tuikalie kitako Sheria ya Madini ili tuifanyie marekebisho, tusiingoje Serikali. Kanuni zetu zinaturuhusu sasa Kamati kufanya hiyo kazi. Tumekuwa tunalalamika humu ndani ya Bunge kama hakuna *power*, Kamati zina *power.* Tutumie Kamati zetu sasa turekebishe sheria hizi ili Watanzania wa-*enjoy* rasilimali zao vinginevyo tutaendelea kupiga kelele humu ndani.

Mheshimiwa Spika, kuhusu umeme. Nilishtuka niliposoma kitabu cha hali ya uchumi, nikakuta umeme unaozalishwa ni *megawatt* 6,688.81. Lakini uliopotea ni 1,686. Kwa hiyo, uliokwenda ndani ni megawatt mbili tu. Kama kuna upotevu wa umeme huu wote *unless* hiki kitabu cha Serikali taarifa yake sio sahihi. Kwa hiyo, kuna upotevu mkubwa sana wa umeme, hebu tutafute *solution*. Huu umeme unapotea bure, lakini kwa leo nataka niwashauri Waheshimiwa Wabunge na tukubaliane katika tatizo hili ambalo tumekubaliana kwamba ni janga la Kitaifa na sote tulionyanyuka ndani humu tunajua hili ni janga la Kitaifa na kwa uwezo wa Serikali yetu katika kulitekeleza inaonekana wanahitaji msaada wetu.

Mheshimiwa Spika, nashauri Kamati ya Madini, Kamati ya Fedha na Uchumi na Kamati ya Katiba na Sheria tupate watu tisa, tulisimamie jambo hili ili tuagizie *barge* ambayo inaweza kutuletea umeme wa *megawatt* 100 na tupate na gesi. Kama gesi itashindikana kwa sababu ya matatizo haya yaliyopo tutaagizia *liquid gas* kutoka Qatar au Oman ambapo Serikali yetu ina mahusiano ili tupate umeme haraka kwanza. Tuwasaidie wenzetu watoke hapa tulipo, wakati tunatatua matatizo mengine ya ndani wananchi wapate umeme. Waheshimiwa Wabunge naomba kabisa, Rais ni sehemu ya Bunge akishirikiana na Kamati hii kwa madaraka yake aliyonayo nakuhakikishieni miezi miwili tutatatua tatizo la umeme angalau *hundred megawatts* zitapatikana *barges* zenye umeme ziko tele.

Mheshimiwa Spika, lingine juzi ulipotupeleka Malaysia, Balozi anasema ameiandikia Serikali juu ya *IPTL*. Hali yao waliyonayo kule ni mbaya. Mradi uliobaki wa kupatia fedha ni hapa Tanzania. Balozi barua yake haijashughulikiwa mpaka leo. Tunaendelea kunyonywa na *IPTL*. Kwa nini maeneo ambayo tunapoteza rasilimali bado tunaendelea kuyakalia kila siku. Ushauri wangu, shauri la *IPTL* limalizike ili lijulikane moja au mbivu. Lakini suala la mikataba la gesi nalo vile vile lishughulikiwe. Jambo la aibu, Mwanasheria yule yule anayetumika kwenye Kampuni zile za Gesi ndiye Mwanasheria huyo huyo anayetumika Serikalini. Hivi kweli itakuwa. Jaji Msomali, Mshtakiwa Msomali au Mpemba, Mwenyekiti Msomali mtafika wapi? Mtu huyo huyo mmoja anashauri huku na huku na Serikali inamtumia huyo, huyo na *TANESCO* inamtumia huyo huyo, hatuwezi kufika pahali! Tunahitaji kuwa *more transparent* ili tuweze kuendeleza uchumi wa nchi yetu. Nawaomba sana Waheshimiwa Wabunge tukubaliane, tupate *solution* ya dharura. Kamati ndogo ya watu tisa ipatikane, ifanye kazi kwa haraka na nawaomba ndugu Wabunge muiunge mkono hoja yangu hiyo. (*Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

**SPIKA:** Hiyo hamuiungi mkono, huyo hajatoa taarifa, sasa mnaunga mkono! Yeye anatoa kusudio, hajatoa hoja yoyote hapa.

Tunaendelea, nashukuru sana, kwa hiyo, tunaweza kupata nafasi mbili, Mheshimiwa Esther Bulaya anaweza kupata nafasi na Mheshimiwa Augustino Manyanda Massele pia anaweza kupata nafasi.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia Wizara hii muhimu ambayo imebeba uhai wa Taifa letu. Kwanza kabisa, napenda kuwapongeza vijana wenzangu ambao Ijumaa walitoa hotuba zao nikianza na Mwenyekiti wa Kamati ya Nishati na Madini, kaka yangu January Makamba, lakini pia na Waziri Kivuli Mheshimiwa John Mnyika kwa hotuba zao kama Serikali itazichukulia kwa umakini ni hotuba ambazo zimejaa uzalendo, zilikuwa hazina ushabiki, lakini ni hotuba ambazo zinaleta mawazo ya kutafuta *solution* ya matatizo yanayoikabili Taifa letu katika sekta ya umeme pamoja na madini.

Mheshimiwa Spika, pili, nitoe tu angalizo kwamba sina tatizo na Waziri wala Naibu wake. Lakini kwa niaba ya vijana wenzangu wa Tanzania, kwa niaba ya vijana wenzangu kutoka Mkoa wa Mara wale wote ambao wanapata matatizo katika migodi kule Nyamongo, kwa niaba ya vijana wenzangu ambao wamemaliza elimu ya juu wameamua kujiajiri wenyewe, lakini sasa hivi wanakwama kutokana na matatizo ya mgao wa umeme wamenituma nisiunge hoja mkono.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, naomba niongelee kwa upande wa sekta ya madini. Nilikuwa nasoma taarifa ya Kamati ya Jaji Bomani, kuna mapendekezo mazuri ambayo aliyatoa yenye lengo la kuondoa migogoro inayojitokeza sasa hivi katika sekta ya madini. Labda nianze kuzungumzia katika ushirikishwaji wa umiliki wa hisa kwenye Serikali za Mitaa katika migodi. Tumeona migogoro ikiwa inatokea mara kwa mara lakini napenda nitoe pendekezo langu kungekuwa na umiliki wa hisa katika kijiji

ambacho ardhi yake ina madini kwenye Makampuni ya Madini. Hili linawezekana kwa sababu sisi ndio tunaotunga sheria tuna uwezo wa kurekebisha haya.

Mheshimiwa Spika, nchi ya Papua New Guinea ilifanya marekebisho ya sheria na ikahakikisha kijiji ambacho ardhi yake ina madini inamiliki hisa ya asilimia tano katika Makampuni ya Madini kwa nini sisi tunashindwa. Hebu tutoe fursa tufanye marekebisho ya sheria zetu ili Kijiji cha Nyamongo kiwe kina hisa katika mgodi, ili kule Geita wawe wana hisa kwenye mgodi. Nilikuwa napitia Sheria ya Madini, ilikuwa inazungumzia umiliki wa hisa kwa Serikali. Lakini tunajua fedha zikienda kule juu kushuka chini huko ni tabu. Kwa hiyo, kama tunazungumzia Serikali iwe na hisa basi hiki kijiji ambacho kina madini na wenyewe wawe na mgao wao. Hapa tutaona kabisa manufaa ya kuwa na madini kwenye ardhi yao na kwenye vijiji yatakuwepo moja kwa moja.

Mheshimiwa Spika, napenda kuzungumzia suala la mabadiliko ya mrabaha. Mheshimiwa Zitto amelizungumzia pia. Tunajua baada ya kufanya mabadiliko ya Sheria ya Madini Serikali ilipendekeza asilimia nne. Lakini cha kushangaza hii Sheria haijaanza kutumika sasa hivi haiyagusi Makampuni ya Madini ambayo tayari yameshaingia mikataba, inagusa Makampuni mapya. Lakini haya Makampuni yameshachuma na mikataba ya madini inachukua miaka mingi. Wenzetu wa Zambia walipoamua kufanya mabadiliko kutoka asilimia 0.6 mpaka asilimia tatu waliya-*include* Makampuni ya zamani, sisi tunashindwa nini? Tunapata kigugumizi cha nini katika rasilimali zetu wenyewe. Baada ya Zambia kufanya mabadiliko waliwaambia kuanzia sasa hivi sheria yetu inasema hivi, mkitaka fuateni hamtaki ondokeni, tuachieni madini yetu. Kwa nini sisi tunashindwa na Kamati ya Bomani ilipendekeza asilimia tano. Lakini sheria imebadilisha imekuwa asilimia nne, lakini bado haifanyi kazi.

Mheshimiwa Spika, kama hili ongezeko la asilimia moja lingefanya kazi tulikuwa na uwezo wa kukusanya zaidi ya bilioni 126 tofauti na shilingi bilioni 63 ambazo tunapata sasa hivi. Kuna haja ya hii Sheria ya Madini tuipitie upya. Mama yangu pale Mama Anna Kilango alisema, madini hayaozi, Baba wa Taifa alishatuambia na hii ni mali yetu, tufanye marekebisho Watanzania wanufaike na rasilimali zao. Tuliunda Kamati, imetushauri, lakini hatukuyafanyia kazi moja kwa moja, tumeyaweka tu kabatini, bado Watanzania wanalalamika. Tunaomba Serikali sasa hivi isikie kilio cha Watanzania. Tumechoka kuona vijana wenzangu Nyamongo kule Tarime wanapata matatizo, kila siku wanapata matatizo kwa sababu ya rasilimali zao hawanufaiki nazo. Napendekeza, hebu tuanze na asilimia tatu ili hivi vijiji ambavyo ardhi yao ina madini waanze kunufaika. Naongea haya kwa uchungu, vijana wenzetu wanakufa, lakini wanakwenda kujitafutia riziki kwa sababu hakuna mazingira mazuri yanayowafanya waweze kunufaika na rasilimali zao.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naomba niongelee upande wa umeme. Tunajua kwamba umeme ni janga la Kitaifa na Wabunge wenzangu wanakubaliana na mimi. Lakini cha kushangaza bajeti ya Wizara haionyeshi kwamba umeme ni kipaumbele. Tunajua zaidi ya Watanzania milioni 40 waliounganishwa kwenye gridi ya Taifa ni asilimia 14 tu. Asilimia 12 mijini, asilimia mbili ndio vijijini ambako ndio zaidi ya asilimia 80 ya Watanzania wanaishi. Lakini mwaka jana zilitengwa shilingi bilioni 58

kwa ajili ya Mfuko wa Umeme Vijijini. Leo hii ambapo tunasema umeme ni kipaumbele tumetenga shilingi bilioni 57, *which is which?* Ni kweli kipaumbele. Lakini hapo hapo mwaka jana mbali ya kutenga shilingi bilioni 58 walipata shilingi bilioni 13 tu, sawa na asilimia 23. Sasa nahitaji *commitment* ya Serikali katika hili, hizi shilingi bilioni 57 zitapatikana zote ili Watanzania waendelee kupata umeme. Lakini je, hii *solution* ya umeme kuwaka, kuna Mbunge hapa alikuwa anasema sasa hivi, watu wamegeuka machizi umeme ukiwaka wanashangilia.

Mheshimiwa Spika, Watanzania wamechoka kusikia orodha ya miradi, wanataka umeme, vijana wenzetu wamefunga *saloon*, watakwenda wapi? Inatia uchungu. Tunaomba Serikali itusikie, vijana ndiyo asilimia 60 ya Watanzania milioni 40, wanashindwa kufanya kazi, ajira hakuna, wameamua kujiajiri wenyewe na umeme hakuna wafanyeje? Wameniambia nisiunge mkono hoja mpaka haya majibu yapatikane katika sekta ya madini na kwenye nishati. Tumechoka na hatutaki tena kusikia orodha ya miradi tunataka umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa leo naishia hapo. *(Makofi)*

**MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Sina muda kwa sababu muda wenyewe umebakia kidogo nataka kumpa nafasi Mheshimiwa Maselle, nasikia hayupo anayefuata Mheshimiwa Hussein Nassor Amar. Mwongozo utapewa baadae mpaka nimalizie hawa. *(Makofi)*

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia hoja hii ya Wizara ya Nishati na Madini. Kwanza napenda niseme kwamba siungi mkono hoja mpaka hapo nitakapopewa majibu ya usahihi kabisa kutokana na yale nitakayouliza na kuyachangia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tatizo la umeme ni janga la Kitaifa. Tatizo la umeme haliendani na mpango wa miaka mitano wa Taifa kwa sababu Mpango wa Taifa wa miaka mitano ni kumkomboa Mtanzania aweze kuwa na hali nzuri lakini ukiangalia Bajeti ya Nishati na Madini haiendani sawa, kwa nini nasema haiendani sawa. Leo kuna Watanzania ambao wamechukua mikopo kutoka sehemu mbalimbali ikiwemo kwenye mabenki, kwa watu binafsi ili waweze kujikomboa na waweze kufanya biashara na kulipa. Leo hii kina mama ntilie wamekopa mikopo watailipa vipi? Wananchi mbalimbali wamekopa mikopo watailipa vipi? Wamenunua vifaa mbalimbali vikitegemea umeme, wamekopa mikopo kwa ajili ya kuendeshea shughuli mbalimbali zinahitaji umeme. Lakini umeme haupo watalipa vipi madeni yao kama sio kuwafilisi? Benki inahesabu kila siku, haihesabu kwamba leo kuna umeme au hakuna umeme. Mkopaji iliyekopesha ama mkopeshaji aliyekopesha hahesabu kwamba leo kuna umeme, ana hesabu siku. Hii Wizara ya Nishati na Madini iangalie upya tatizo hili na husasan Serikali iliangalie kwamba hili ni tatizo la dharura, ihakikishe umeme unapatikana kwa haraka ili kuwakomboa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuangalie Serikali imeweza kuchukua dharura kwa kumsafirisha Mheshimiwa Freeman Mbowe kumtoa Dar es Salaam kumpeleka Arusha kwa kutumia ndege, leo Serikali inashindwa vipi kulichukulia udharura jambo hili la kuleta mitambo ya haraka kuweza kukomboa tatizo la umeme. Mwaka 1999 Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi Mzee John Malecela alikuja Jimboni kwangu akawaahidi wananchi wa Jimbo la Nyang'hwale kwamba watapata umeme ndani ya miezi minne. Lakini umeme haukuwaka, mwaka 2008 Naibu Waziri Mheshimiwa Adam Malima alikuja na kuahidi wananchi wa Jimbo la Nyang'hwale baada ya kuanzisha vurugu na kutaka kuchoma milingoti iliyopo ambayo inapeleka umeme kwenye Mgodi wa Kahama. Alikuja akawatuliza wananchi wa Jimbo la Nyang'hwale na kuwaambia kwamba umeme utawaka ndani ya miezi mitano, lakini haukuwaka mpaka leo.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2010 Mheshimiwa Rais alikuja na akaahidi kwamba umeme utawaka muda si mrefu, mwezi wa pili 2011 Mheshimiwa William Ngeleja alinijibu hapa na akasema mwezi wa tano umeme unawaka. Je, leo utawaeleza nini wananchi wa Jimbo la Nyang'hwale? Mimi na wao tunapoteza matumaini. Tunakuomba Mheshimiwa Ngeleja hatupitishi Bajeti hii ni lini umeme utawaka?

**SPIKA:** Naomba mtumie Waziri wa Nishati na Madini.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Nizungumzie suala la madini. Tatizo la migodi iliyoko katika Jimbo la Nyang'hwale, Kahama, Geita na Nyamongo matatizo haya yanafanana. Wananchi ambao tumezunguka maeneo hayo umaskini tumepigika kuliko. Wanakuja kuchimba migodi hiyo na kutuachia makorongo marefu wakati sisi hatupati chochote. Ninaomba katika Bunge lako Tukufu mikataba hii iangaliwe ni vipi na sisi tutanufaika na uchimbaji huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hapa ninapozungumza Mgodi wa Kahama hivi sasa wamechimba kwenda chini kuelekea Geita kilomita 25 ardhi inaning'inia na hao hao wametuahidi kutuchimbia visima na mambo mengine hawajatufanyia hivyo mpaka leo. Migodi hii hatufaidiki nayo, wanafaidika hao waliokuja kuwekeza. Upande wa ajira watumishi waliopo migodini wameniambia kwamba kuna unyanyasaji wa hali ya juu, unyanyasaji huo unaanzia kwenye mishahara. Baadhi ya wageni ambao wameletwa kufanya kazi pale wanalipwa kwa pesa za kigeni. Watanzania wanalipwa kwa pesa za Tanzania wakati dhahabu inauzwa kwa fedha za kigeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nizungumzie kuhusu leseni za utafiti wa madini. Kwa kweli tunaomba sera hiyo iangaliwe upya kwa sababu kuna unyanyasaji wa hali ya juu namna ya kutoa leseni za uchimbaji na utafiti. Hivi ninavyozungumza katika Jimbo langu la Nyang'hwale hakuna hata sehemu moja ukienda kugusa ukakuta hakuna *PL*. Maeneo yote yameshauzwa je, huyu mwananchi wa Jimbo la Nyang'hwale, mtoto na mjukuu wake atakuja kufanya kazi gani? Nyang'hwale yote imeshagawiwa kwa wawekezaji. Kwa hiyo, ninaomba mikataba hii ya madini iangaliwe upya. Pia katika uchimbaji wa madini ninathubutu kusema kwamba wanatuibia kwa kushirikiana na wataalam wetu waliosomeshwa na kodi za wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tulifanya ziara na Mheshimiwa Naibu Waziri wa TAMISEMI kule *Geita Mine,* tumekwenda pale tukazungushwa. Matokeo yake tukaenda kuonyeshwa korongo kubwa sana ambalo wameshachimba, ukikusanya Dar es Salaam, Morogoro na Dodoma ukavunja nyumba zote kifusi hicho hakiwezi kujaa kwenye hilo korongo. Nikamuuliza yule Afisa Uhusiano kwamba hili korongo baada ya uchimbaji wenu mtafanyaje anajibu kwamba hili linaweza likatengenezwa watu wakawa wanakuja kuangalia kama vile watalii. Nikamuuliza na tukiwa na Naibu Waziri mnapata kiasi gani kwenye kila tani moja ya mawe? Ananiambia kwamba katika tani moja wanapata gramu mbili, ni uongo. Mimi nimezaliwa kule na nimeanza uchimbaji mdogo mdogo tangu mwaka 1973 ninaelewa tani moja inatoa kiasi gani. Pamoja na kwamba sikusoma sana ninaomba Waziri anitafute nimueleze wanatuibia namna gani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo hii nimepata taarifa kuna wananchi ambao wamepigwa risasi kwenye maeneo hayo hayo ya mgodi. Wameenda kuzoa zile takataka ambazo wao wanasema hazifai. Lakini wananchi wanasafisha kwenye kilo 30 wanapata robo gramu. Wao wanasema tani moja wanapata gramu mbili ambapo wanakwenda chini na kwa kutumia mitambo. Ni uongo na wizi wa hali ya juu kupitia wataalam wetu tuliowasomesha kwa kodi zetu. Pia tukafanya kikao na yeye tukamwambia huu uharibifu unafanyika, tunafaidika nini, mmeahidi ahadi ngapi hapa? Wameahidi kujenga shule ya sekondari leo miaka nane hawajamaliza kuijenga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *Kahama Mine* wametuahidi katika Jimbo langu visima saba, leo miaka sita hawajachimba, wanatuibia kiasi gani. Ninaomba mikataba hii iangaliwe upya na ninakuomba Mheshimiwa Waziri uilete mikataba hiyo tuiangalie imeanza lini na inaishia lini. Tujue wananchi wetu adha hii ya kupigwa risasi na maandamano yao, wanafukuzwa tujue yataisha lini. Kama ni miaka kumi tujue, miaka kumi ikiisha wananchi wetu watapumzika kupigwa risasi. Leo hii hatujui mikataba hii inaisha lini. *Underground* iliyopo pale kuanzia Kahama kwenda Geita kilomita 25 chini kwa chini. Baada ya miaka 50, matetemeko ya ardhi je, sisi wana Geita na Nyang’hwale tutabaki salama? Jaribuni kutuhurumia nyie viongozi mlioko juu. Kama kuna uwezekano Bunge hili lipitie upya mikataba. *(Makofi)*

Pia kuna unyanyasaji wa hali ya juu. Katika maeneo yetu hawahitaji kununua hata bidhaa zetu tunazozalisha sisi wenyewe. Tunafaidiki nini na wao, hata maembe wanaagiza kutoka Afrika Kusini, mchicha wanaagiza Kenya, tutafaidika na nini? Tunaomba mikataba hii ipitiwe upya na kama kuna uwezekano ipunguzwe na kama kuna uwezekano waondoshwe. Mwalimu Nyerere alisema dhahabu haiozi na sisi tutasubiri mpaka tuwe na uwezo tutakuja kuchimba hata kama miaka mia moja kuliko sasa hivi tunaibiwa na tutabakiziwa makorongo ambayo yatakuwa na athari kwetu.

Mheshimiwa Spika, nikuachie muda na nasema kwamba siungi mkono hoja mpaka kieleweke. Mheshimiwa Ngeleja ni jirani yangu na ninathubutu kusema kwamba Bajeti yake hii nadhani wamemsurubisha viongozi wake ama watendaji wake. Ahsante sana. *(Kicheko/Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mnyaa kuhusu Mwongozo.

**MHE. MOHAMMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa tulitengua Kanuni ya 101 ambapo Bunge lako hili likikaa kama Kamati Mbunge atakuwa na nafasi moja ya ufafanuzi ambapo hatopata nafasi nyingine, na kwa kuwa *complication* ya Wizara hii na Bajeti yake ina mapungufu hata ya kihesabu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Usiingie kwenye mifano, sema unachotaka kusema.

**MHE. MOHAMMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Spika, ninachosema kwa kuwa kuna mapungufu mengi ya kimahesabu na kuna upotevu wa pesa ambazo hazionekani hata katika randama na katika Idara 21 za Wizara.

**SPIKA:** Sema unataka tufanye nini?

**MHE. MOHAMMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Spika, ninachotaka kusema ni vyema kabla ya kuingia na kwa kuwa Wabunge wengi wameshaikataa, kabla ya kuingia katika Kamati ya Matumizi hapo baadae kwa nini usitoe Mwongozo wako kuepukana na aibu ya kukataliwa hapa Bungeni, wakapewa muda waende warekebishe hata haya mahesabu na Wizara au Idara kwa mfano *TPDC* iliyopewa shilingi bilioni tatu kwa kuhudumia miradi mingi wakapata aibu hapa waende wakajitayarisha zaidi na watengeneze mahesabu halafu wakaja tena na kuipitisha Bajeti hii kuliko aibu hii ya kukataliwa hapa? Naomba Mwongozo wako. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, wakati ni mali na wakati lazima tuutumie vizuri. Kuanzia sasa mpaka saa kumi na moja kama hayo mnataka yarekebishwe yatarekebishwa kama ni mahesabu. Kwa hiyo, hilo halimo kwenye utaratibu wetu.

Kwa mujibu wa Kanuni nilikuwa nimemwambia Mheshimiwa Silvestry Koka, kwa mujibu wa Kanuni ya 61 kwamba angepaswa kutangaza *interest* zake au maslahi yake aliyokuwa anazungumzia. Hili nawaambia wote kwa sababu adhabu yake ni kali, kwa sababu tunazungumzia Wizara nyeti kama hii utakuta wengi wenu mna maslahi ndani ya mambo yote haya. Sasa ukija kugundulika na mtu mwingine kwamba wewe huku-*declare* maslahi yako tunakuondoa kwenye Bunge kwa siku kumi au kikao kizima tunakutoa. Kwa hiyo, ni vizuri kabisa msije mkawa wasemaji wazuri wakati hamjatimizi masharti yanayohusika.

Kanuni hiyo inasema kama ifuatavyo: “Wakati wa majadiliano Bungeni au kwenye Kamati yoyote ya Bunge, Mbunge hataruhusiwa kuzungumzia jambo lolote ambalo yeye mwenyewe ana maslahi binafsi nalo ya kifedha isipokuwa baada ya kusema jinsi anavyohusika nalo na kutaja kiwango cha maslahi hayo na kwa sababu hiyo itakuwa ni lazima kwa Mbunge yeyote anayetaka kuzungumzia jambo hilo Bungeni au kwenye Kamati yoyote ya Bunge kusema kwanza jinsi anavyohusika na jambo hilo na kutaja kiwango cha maslahi ya kifedha aliyonayo kuhusiana na jambo hilo kabla ya kuanza kulizungumzia.” *(Makofi)*

Kwa hiyo, hii ni Kanuni na najua wengi hapa msije mkajitia wasemaji wazuri wakati hili hamja-*declare*. Kwa suala la Mheshimiwa Silvestry Koka kwa sababu amekubali kwa hiyo, kosa hilo kwa mara ya kwanza tunamsamehe na wengine sasa wasije wakarudia kwa sababu ikiwa ni kosa la kwanza hili mimi nikipeleka kwenye Kamati yangu ya Maadili, kosa la kwanza asihudhurie vikao vya Bunge visivyozidi kumi. Halafu kama ni kosa la pili au zaidi asihudhurie vikao vya Bunge visivyozidi ishirini. Sasa hapo ni kama huyu angekataa mimi ningepeleka hilo kwenye Kamati ya Maadili wangefanya *investigation* yao na wakigundua hapo anapata adhabu ya kwanza na kama ni ya pili basi inaendelea hivyo. Kwa sababu amekubali hapa sasa nasema wengine msije mkafanya kosa kama hili. *(Makofi)*

Nimeombwa na Katibu wa *caucus* ya CCM kwamba Wabunge wote wa CCM watakuwa na kikao saa saba hii Jengo la Msekwa. Huo ndiyo utaratibu wa Mabunge, ni kama vile CHADEMA watakutana saa tisa, CCM saa saba na nusu. *(Makofi/Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa kumi na moja jioni.

*(Saa 6.59 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, wakati tunasitisha shughuli za Bunge kipindi cha asubuhi, nilikuwa nimesema nitaanza kuwaita watoa hoja waanze kutoa ufafanuzi wa mambo mbalimbali. Kwa hiyo, naendelea, Mtoa hoja! Mheshimiwa Waziri, Mkuu! *(Makofi)*

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwamba ameniwezesha niweze kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu jioni hii kwa ajili ya kutoa maelezo mafupi kwa nini nimeona nisimame mbele yako na mbele ya Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, najua tumezoea mara nyingi mtoa hoja anakuwa ni wa sekta inayohusika, lakini Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni ni Waziri Mkuu na kwa uzito wa jambo hili nimeona bora niifanye kazi hiyo mimi mwenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumekuwa na mjadala wa siku mbili na leo ilikuwa ndiyo siku ya kuhitimisha hoja. Waheshimiwa Wabunge, tukianza na Mwenyekiti wa Kamati, kuja Mwakilishi wa Upande wa Upinzani Bungeni, Wabunge wote kwa ujumla wenu, mmetoa michango mizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwangu mimi na Serikali kwa ujumla tunataka tuipokee michango yenu yote kwa dhati na kwa ujumla tunaizingatia yote na tutajitahidi sana kuhakikisha tunatekeleza yale ambayo mlidhamiria tuweze kuyatekeleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mjadala mzima umegusa maeneo yote mawili ambayo yanahusu sekta hii muhimu. Upande mmoja ni suala zima la nishati, upande mwingine ni suala zima la madini. Sekta zote hizi ndogo mbili zina umuhimu mkubwa sana kwa Taifa letu na kwa Watanzania wote. Kupitia michango yenu, yapo mawazo mazuri sana, zipo busara kubwa sana zimetolewa katika kuisaidia Serikali iweze kutumia michango hiyo kuja na maelezo ambayo yatasaidia kweli kushughulikia maeneo haya mawili kikamilifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka nitumie muda wako kidogo, nichukue eneo moja ambalo kwangu nadhani ndiyo limechangiwa kwa nguvu sana, si kwa kudumaza au kupuuza sehemu ya pili, hapana; nalo ni hili la mgao wa umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, umeme ni uhai kwa Taifa letu, msingi wa maendeleo kwa nchi yetu na kwa vyovyote vile hatuwezi kuzungumza juu ya kupunguza umaskini kama eneo hili la umeme halikupewa nafasi kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tatizo hili la umeme tulianza hasa kulipata kwa nguvu sana mwaka 2006 wakati tulipopata ukame mkubwa sana na matokeo yake ukawa ni mgao mkali sana ambao ulitufanya tukayumba sana. Serikali iliamua baada ya pale kuanzia mwaka 2007/2008 kwamba ni lazima Serikali sasa ianze kuachana na kutegemea chanzo cha maji kama ndiyo msingi wa upatikanaji wa umeme.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Serikali ikasema sasa tujikite katika suala la gesi asilia, tutazame vilevile uwezekano wa makaa ya mawe na pale itakapobidi hata upepo utumike hasa katika maeneo ambayo yana fursa kubwa ya upepo. Na ili tuweze kulifanikisha hili, kupitia Bunge lako Tukufu na nawashukuru sana kwa jambo hili, mkakubali kabisa kwamba ni vizuri tuwe na sheria inayoruhusu hata sekta binafsi kuweza kupata umeme kwa njia zao wenyewe ili mradi uwe ni umeme utakaosaidia kupunguza kero kwa Watanzania. Sheria ile imepitishwa na Bunge hili na bahati nzuri tumeshaanza kuitazama, inatumika sasa katika baadhi ya maeneo ili kuwezesha kupunguza tatizo hili kwa kiasi kikubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba hali ya umeme ilivyo sasa si nzuri hata kidogo. Katika chanzo cha maji, leo tunavyozungumza tunaweza tu kuzalisha *MW 132* kati ya *MW 536* zinazohotajika. Na kwa hali ya ukame tunavyoiona, mwelekeo tunakokwenda ni vigumu sana kubashiri nini kitatokea baada ya hapo. Ndiyo maana Serikali ikaona uamuzi huu wa kutumia gesi lazima tuukazanie.

Sasa tumeanza tulivyoweza, *MW 100* zile za Ubungo, tukapata *MW 45* zile za Tegeta, *Songas* nao pamoja na matatizo yao, lakini ndiyo wanaotupa gesi inayozalisha umeme kwa *MW 180.* Lakini tumeona chanzo hiki ni kizuri kwa sababu katika kipindi hiki kifupi tumeweza angalau kupata *MW 325* ukilinganisha na *MW 500* na zaidi za upande wa sehemu ya kwanza. Kwa hiyo, si haba ulikuwa ni mwanzo mzuri na mwelekeo mzuri.

Mheshimiwa Spika, lakini, tumefanya tathmini kama Serikali na tukasema pamoja na hali hiyo ambayo inaonekana ina mwelekeo mzuri, ni lazima tufanye kazi ya

ziada. Kwa hiyo, tumekubaliana kwamba hebu tujipange tuone mpaka tarehe 31 Agosti, 2011 tunaweza kuwa tumewafikisha Watanzania wapi kwenye mgao wa umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumeitazama *IPTL* pamoja na matatizo yake, tumetazama *Symbion* na matatizo yake, lakini vilevile tukasema *Aggreko* watakapoingia na wenyewe watatupa nini katika eneo hili. Tulipiga tathmini ya kina, tukasema tunaweza kabisa ifikapo 31 Agosti tukawa na uhakika Watanzania kuwa na karibu *MW 770*. Tutakuwa bado hatujamaliza hadithi maana bado tutakuwa na *short fall* kubwa tu ya umeme, karibu *MW 65*.

Mheshimiwa Spika, tukasema potelea mbali, nini kingine tufanye? Kwa hiyo, Serikali ikaamua kwa makusudi kwamba lazima tununue mtambo sasa wa kuzalisha umeme wa *MW 100*. Mtambo huu tumesema tukichelewa sana mpaka 31 Desemba, *MW 100* zote zitakuwa tayari, tunaanza na *MW 50*, zitafuata *MW 50* zilizobakia. Tukasema tukifika Desemba kwa Watanzania tutakuwa tumeshaondoa ile *deficit* ya *MW 65* na tunaweza kuwa na vi-*MW* kidogo katika *reserve* yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini tathmini imetuonyesha kwamba hata tukifika hapo, bado hatujawafikisha Watanzania mahali pake. Bado hatujawa na uhakika kwamba wanaweza wakaendesha shughuli zao kwa raha bila vikwazo vya mgao. Tukasema hapa ndiyo kwenye mtihani mkubwa. Tukapiga mahesabu, tukasema kwa vyovyote vile lazima tupate *MW* zisizopungua 300 ndani ya kipindi hiki mpaka Desemba mwaka huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tukiweza kufikisha *MW 300*, tutakuwa tuna uhakika mgao haupo, umeme wa kutosha upo na tukasema tukiweza kufika *MW 500*, maana yake tunaongelea katika hali ambayo ni ya uhakika zaidi na hiyo inaweza ikazingatia hata lile ongezeko la mahitaji ya asilimia 14 ambalo linajitokeza kila mwaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimepata nafasi ya kuwasikiliza Waheshimiwa Wabunge na mimi nakubaliana na ninyi kabisa. Haya niliyoyaeleza ambayo yanatupa ahueni mpaka tarehe 31 Agosti na tukienda mpaka Desemba, bila kuwa na zaidi ya *MW 300* nyingine, itatuwia vigumu sana kuwahakikishia Watanzania neema tunayoitafuta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa niaba ya Serikali nikasema nimepokea rai ya Waheshimiwa Wabunge ya kuitaka Serikali itazame, ikae upya na ione hizo *MW* za ziada tunazipata namna gani ndani ya kipindi hiki kifupi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ushauri mlioutoa ni wa msingi sana. Moja; mmesema Serikali nunueni mtambo na tusitafute visingizio vya fedha. Kwamba tafuteni kila mbinu huko, kateni posho zenu, kateni vitu gani, nendeni mkatazame magari mnayotumia haya, punguza huko. Tazameni *OC* yenu kikamilifu, mtaona kule ndani yako matumizi mengine ambayo mkiamua kwa dhati mnaweza kabisa mkayaondoa huko, yakaenda yakanunua mitambo ya uhakika, yakawasaidia hata kuongeza uwezo wa mafuta kwa ajili ya mitambo inayotumia mafuta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ushauri huu ni wa msingi. Katika hali tuliyonayo ni wa msingi kabisa na mimi nimesema nakubali kwa niaba ya Serikali. Wakati huo huo, mmesema ili mturidhishe, mkashauri Serikali ikubali kwamba hatupendi mje hapa mbele, Mheshimiwa William Ngeleja aje hapa, unatuambia Mheshimiwa alisema hivi, Mheshimiwa Freeman Mbowe alisema hili, ah, ah. Tunataka Serikali ije hapa ituambie ina mpango gani wa dharura kwa maana ya kuwapatia Watanzania amani, umeme wa *MW 300* na zaidi ni huu tunawaletea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na wengine mmekuwa wakali kweli kweli, mnasema hamtaki kusikia kitu kingine chochote isipokuwa uhakika wa umeme. Mimi na Serikali yote kwa ujumla na Watanzania wote, nadhani ni kweli wote lazima tuseme Serikali ikubali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimelifanya hili kwa nia njema tu, Rais wangu najua yuko njiani saa hizi anakwenda *South Africa*. Lakini nikasema katika hili, sidhani kama ataniambia Waziri Mkuu kwa nini umekubali hilo, sababu ni jambo jema. Nikimweleza atasema hukukosea mdogo wangu, ulichoamua ni sawa kabisa. Nimekubali na nitatoa hoja hapa kuliomba Bunge lako kwa maana hiyo muikubali Serikali ndani ya kipindi tutakachokuwa tumependekeza, Bunge litukubalie litupe hiyo kazi twende tukalifanyie kazi, tulete hapa maelezo ambayo angalau baada ya pale mtasema aha, sasa tumeridhika na kazi mliyoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini liko jambo lingine ambalo Waheshimiwa Wabunge wamelisema. Wamesema Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Madini kawaudhi, kawatibua kweli kweli Wabunge. Lazima nikiri kwamba na mimi niliposikia Bungeni hapa nikashituka sana tu wala siyo kidogo kwamba kama ndiyo utaratibu wenyewe huo ambao Katibu Mkuu alidhani ni mzuri, lakini utaratibu ambao umegubikwa na maswali mengi, hakuna namna ambavyo utaweza kuutetea hata kidogo! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kikwazo pekee nilichokipata ni kwa sababu Rais hajatua *South Africa* na mwenye mamlaka ya kuteua Makatibu Wakuu ni Rais mwenyewe. Nikatamani sana nije hapa mimi niwaambieni nimeshachukua hatua, nimeamua hivi. Lakini nikaambiwa utakuwa unaingia katika maeneo ambayo si ya kwako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa hili, naomba niwaombe Waheshimiwa Wabunge, kwa dhati kabisa kwamba kwa sababu sina mamlaka juu ya mtu huyu ya kumtimua kazi leo au kumwambia ondoka, mwenye mamlaka ni Rais mwenyewe, kwa hili mnipe baraka zenu, akifika *South Africa* jioni ya leo mimi nitawasilisha maelezo haya kwake. Kwa bahati nzuri si jambo ambalo halina maelezo, lipo dokezo limeandikwa, limesomwa. Sasa basi tumefika hapo, kazi yangu mimi ni kusema nitajaribu kumshauri Rais aweze kuliona kwa mtazamo chanya kwa sababu lina lengo zuri sana. *(Makofi)*

**KUAHIRISHA MJADALA WA BAJETI YA WIZARA YA NISHATI NA MADINI**

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, kutokana na maelezo hayo, naomba basi kupitia Bunge lako Tukufu, kwa kutumia Kanuni ya 55(3)(b) nikachanganya na Kanuni

ya 69(1) mkubali Serikali tuweze kuliomba Bunge lako Tukufu tuahirishe hii hoja kwanza…

*(Hapa Wabunge walishangilia kwa makofi na vigelegele)*

**WABUNGE FULANI:** CCM! CCM!

**WABUNGE FULANI:** *Peoples' Power! Peoples'Power!*

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, nimeomba haya kwa imani kubwa kabisa tu kwamba Bunge kwa nia yake njema na dhamira yake nzuri ya kutaka jambo hili tulishughulikie kwa pamoja, watanikubalia. *(Makofi)*

Baada ya kusema haya, tutahakikisha katika mchakato mzima wa namna tutakavyokwenda, tunashirikisha Kamati za Bunge kwa kiasi cha kutosha ili kwa pamoja tuweze kulimaliza jambo hili kwa njia nzuri kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, naomba sasa kutoa hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**WABUNGE FULANI:** *Peoples' Power! Peoples' Power!*

**WABUNGE FULANI:** CCM! CCM!

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maneno, maneno hayana maana yoyote! Sasa mnisikilize. Hoja iliyotolewa ni kwa mujibu wa Kanuni ya 69(1), Waheshimiwa Wabunge, naomba nisome Kanuni hiyo inasema; "Mbunge anayependa mjadala unaoendelea juu ya hoja yoyote uahirishwe hadi wakati wa baadaye, anaweza kutoa hoja kwamba mjadala sasa uahirishwe na atataja…(narudia neno hilo) atataja mjadala huo uahirishwe hadi wakati gani" (narudia hilo neno) "atataja mjadala huo uahirishwe hadi wakati gani na pia atalazimika kutoa sababu kwa nini anataka mjadala uahirishwe."

Hivyo ndiyo masharti yanavyotaka, muda na nini tunachokitegemea wakati tumeahirisha. Mheshimiwa Waziri Mkuu!

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, nadhani kwa maelezo niliyoyatoa nimejaribu kujenga hoja juu ya sababu. Ninaloweza kuliomba Bunge lako Tukufu, mkituruhusu ndani ya wiki zisizozidi tatu tunaweza kuwa tumeshamaliza kazi hii na kuwarejesheeni hapa. Tarehe utakayoona inafaa ukitupangia, basi tutakuwa tayari. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, naafiki! *(Makofi)*

**SPIKA:** Kwa hiyo, kwa mujibu wa Kanuni inayofuata ya 69(2), "Kama Spika atakuwa na maoni kwamba kuwasilishwa kwa hoja hiyo ni kinyume cha uendeshaji bora

wa shughuli za Bunge, atakataa kuitoa ili iamuliwe, vinginevyo, papo hapo atawahoji Wabunge juu ya hoja hiyo kadri atakavyoona inafaa.” Sasa na mimi lazima nieleze kuona inafaa ama haifai kwa nini.

Waheshimiwa Wabunge, suala hili limevuta hisia za Watanzania wengi na wengine fikra ni kwamba imewakasirisha, imewavurugia uchumi wao, imesababisha Serikali yenyewe kukosa mapato na hata kama kuna *issue* zingine, lakini hili linaonekana ni *paramount*. Kwa hiyo, mimi nakubaliana na hoja iliyotolewa kwamba tuwape muda wa wiki tatu ili wakajipange vizuri, walete kitu ambacho kitakuwa kimeingia kwenye ahadi za Serikali na ambacho kinatekelezeka. Kwa hiyo, kwa misingi hiyo mimi nitawahoji.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Hoja ya kuahirisha mjadala wa Bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini mpaka baada ya wiki tatu ilipitishwa na Bunge)*

*(Hapa Waheshimiwa Wabunge walishangilia kwa kupiga makofi na vigelegele)*

**SPIKA:** Mjadala huu kwa masharti hayo katika wiki tatu tupewe kitu ambacho kinatekelezeka na kinaleta matumaini kwa Watanzania na kitajibu hoja zao. Kwa maana hiyo, nitaomba Kamati ya Uongozi tukiahirisha hapa tunaenda kukutana ili kusudi tukapange hizi tarehe, wiki tatu ni tarehe gani na vile vilivyopangwa katika kipindi hicho viingie katika siku nyingine zipi. *(Makofi)*

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, sina lingine la ziada isipokuwa kesho ni mazishi ya Bibi yake Naibu Spika yatafanyika kipindi cha asubuhi na tunafikiria kwamba tutakuwa na usafiri kwa wale wanaotaka kwenda. Lakini lazima wote kipindi cha jioni wawepo hapa ndani. Kwa hiyo, utaratibu utapangwa na katika Ofisi ya Bunge. Sasa naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi. *(Makofi)*

*(Saa 11.25 jioni Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Jumanne, Tarehe 19 Julai, 2011 saa tatu asubuhi)*